

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 5 Julai, 2010

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILSHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

SPIKA: Kabla sijamwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, napenda natumaini Waheshimiwa Wabunge mlikuwa na *week end* njema siyo kama niliyokuwa nayo mimi ambaye nimerudi kifua kinawasha kwelikweli kutokana na vumbi ya huko Saba saba na mambo mengine ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, mtanisamehe leo sauti yangu siyo ya kawaida. Lakini mniombee ili niweze kupona haraka kwa sababu naelewa wengi wenu mnanipenda na mnazo sababu za kunipenda, basi muendelee kuangalia kwenye masanduku ya barua kuna mambo kidogo mazuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto!

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII): Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu ni muhimu niweke kwenye *record* nzuri kwamba tunampongeza sana Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, nadhani hii ni mara ya kwanza katika Bunge letu tangu Uhuru kwamba Mbunge asiyehona ameweza kuwasilisha hati mezani.

Lakini pia hongera pia kwa Mwenyekiti kwa kutoa fursa kwa Mheshimiwa Zuleikha Y. Haji. Ahsante sana. (*Makofi*)

Sasa ni zamu ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 166

MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. STEPHEN J. GALINOMA) aliuliza:-

(a)Je, Serikali inaweza kutoa takwimu ya watumishi wa Serikali Kuu upande mmoja na Serikali za Mitaa upande mwagine hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2009?

(b)Je, kulikuwa na watumishi hewa wangapi na Serikali ina mpango gani wa kudumu wa kumaliza tatizo hilo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Stephen Galinoma kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na mimi niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji kwa kuwasilisha mezani hoja ya Kamati yake, na nipa ninakupa pole kwa mafua na karibu tena.

Sasa ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma Mbunge wa Kalenga swali lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2009 idadi ya watumishi katika orodha ya malipo ya mishahara (*Payroll*) walikuwa 382,701. Kati ya hao, watumishi wa Serikali Kuu walikuwa 100,248 na watumishi wa Serikali za Mitaa walikuwa 282,453.

(b)Mheshimiwa Spika, katika uhakiki uliofanywa katika Sekta ya Elimu mwaka 2007, jumla ya watumishi hewa 1,413 ambao waligundulika. Hali kadhalika, uhakiki uliofanywa katika Sekta ya Afya mwaka 2008 jumla ya watumishi hewa 1,511 waligundulika. Jumla ni watumishi hewa 2,924 na wote hao sasa wamefutwa kwenye orodha ya malipo ya mishahara (*Payroll*).

Tatizo la watumishi hewa linachangiwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa uwajibikaji mionganoni mwa Maofisa wenye dhamana ya masuala ya kiutumishi katika Taasisi za Umma. Ili kukabiliana na tatizo hili Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma sasa imeamua kuendesha zoezi la uhakiki raslimaliwatu kwa waajiri wote mara kwa mara ili kuhakikisha watumishi hewa wanaondolewa katika *Payroll* ya Serikali.

Aidha, mbali na kufanya uhakiki wa kila mwezi wa orodha ya malipo ya mishahara (*Payroll Audit*) Ofisi yetu inahusisha mfumo wa kompyuta wa taarifa za kiutumishi na mishahara na kazi hii itakapokalika itaondoa kabisa tatizo la watumishi hewa.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunashirikiana na vyombo vingine vya Dola kwa madhumuni ya kuwachukulia hatua mbalimbali za kisheria na kinidhamu wahusika walioshiriki katika kufanikisha kukwepo kwa watuhimi hewa kwenye sekta ya Utumishi wa Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa kupitia Bunge lako tukufu ninapenda kutoa rai kwa waajiri wote nichini kuangalia suala zima la watumishi hewa katika orodha za malipo ya mishahara kwa watumishi wao ili kuondoa upotevu wa fedha nyingi za Serikali zinazolipwa kwa watu ambao hawalitumikii Taifa kwani wakigundulika Watendaji Wakuu wa maeneo ya kazi yanayohusika watachukuliwa hatua kali za kisheria na kinidhamu.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa, kila Wizarana Idara wana ikama ya watumishi, na Menejimenti ya Utumishi wa Umma wanapotoa kibali wanakuwa wanajua kwamba idara inahitaji watumishi wangapi. Sasa inakuwaje kuwe na Watumishi hewa? Hiko la kwanza.

Lakini la pili, kwa kuwa hili ni tatizo la muda mrefu pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri sasa watachukuliwa hatua wale wanaohusika. Je, sasa kwa nini hizo hatua zisingechukuliwa mapema ili kupunguza gharama ya Serikali kulipa mishahara hewa?

SPIKA: Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kujibu swalii la Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma ninapenda mtambue Viongozi wetu humu ndani kwa upande wa Serikali ni Mhesimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya ndiye anayeshikilia uongozi wa shughuli za Serikali. Sasa mkiwa na shida basi huyo ndiye anaweza kuwasaidia. (*Makofi*)

Lakini kwa upande wa pili Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji ni Kaimu Kiongozi wa Upinzani. (*Makofi*)

Tunaendelea na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza ni kwamba inakuwaje tunakuwa na watumishi hewa.

Tanzania ni nchi kubwa na shughuli zote za Serikali zinakuwa zikifanyika Makao Makuu kwa lugha ya Kingereza ni kwamba *Tanzania is a highly centralized State*.

Katika Wilaya za pembezoni watumishi wote wanaajiriwa na Serikali na wanalipwa na Serikali, katika hali kama hiyo ni rahisi sana watumishi kutoku-report kwenye maeneo ambapo wameajiriwa hasa Wilayani na Mikoani na hivyo wakati mwingine mafanikisho pia na Wakuu wa Idara amba siyo waaminifu na ndiyo maana tumesema sasa hatua kali zitachukuliwa kwa wale Viongozi wa maeneo ya utawala katika Halmashauri na pia katika Mkoa. Ni kwa nini hatua hizi hazijachukuliwa hadi leo? Hatua zinachukuliwa ndiyo maana kitu hiki kinafanyika mara kwa mara lakini kama tulivyosema pale awali sasa tunataka kutumika teknolojia ya TEKNOHAMA kwamba idadi yote ya watumishi wa Umma itakuwa kwenye computer na mishahara yao yote itakuwa ikifuatiliwa kwa kutumia teknolojia ya *computer*.

MHE. RISHED MOHAMED ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swalii moja la nyongeza.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amegundua kwamba katika ukaguzi wake kuna ushirikiano kati ya Halmashauri, Wizara ya Elimu kama Wafanyakazi ni Walimu pamoja na Wizara ya Fedha wana-coordinate ndiyo maana inawezekana kuchukua hizi fedha kwa watumishi hewa.

Je, Serikali itatua vipi tatizo hili kwa ushirikiano wa hizi Wizara tatu katika kutatua kabisa suala la watumishi hewa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Rished Abdallah Mbunge wa Pangani, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Tatizo hili linaweza kutatuliwa kwa kushirikiana hasa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na ndiyo maana tunafahamu hata ni fedha kiasi gani ambazo zilikuwa zinalipwa kwa ajili ya mishahara hewa. Niseme tu ni fedha nyingi kidogo zaidi ya bilioni 7 ambazo zimegundulika zikilipwa hadi mwaka juzi wa fedha na nimeeleza kwamba pia sasa watumishi wote watakuwa na takwimu zao katika *computer*. Kwanza katika Idara Kuu ya Utumishi lakini pia Hazina na kutakuwa na uhakiki wa mara kwa mara.

Na. 167

Faida za Kujiunga na SADC

MHE. JACKSON M. MAKWETTA (K.n.y. MHE. YONO STANLEY KEVELA) aliuliza:-

COMESA, SADC na Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) ni vyombo muhimu sana kiuchumi na Kisiasa, lakini vyombo hivyo vina mgawanyiko mkubwa sana kiuanachama kama vile Tanzania kuwa Mwanasheria wa *SADC* na Kenya na Uganda kuwa wanachama wa *COMESA*:-

- (a) Je, Serikali za nchi hizi zina mpango gani wa kuondoa tofauti hizo?
- (b) Je, kuna faida gani Tanzania inazipata kutokana na kujiunga na *SADC*?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikupe pole kwa mafua na pili nimpongeze Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, kwa kuweza kuja kuweka mezani Hati ya Kamati yake pamoja na hali aliyonayo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Jimbo la Njombe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali za nchi wanachama wa Jumuiya zote tatu, *COMESA, SADC* na *EAC* zimechukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto za nchi wanachama kuwa katika Jumuiya zaidi ya moja kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kwanza kuwa na vikao vya pamoja vya wakuu wa nchi na Serikali na vya Mawaziri wa Jumuiya zote tatu ili kupokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa maamuzi yanayogusa Jumuiya zote na hasa kuhusiana na makubaliano ya kibiashara kikanda na kimataifa. Hii inasaidia kuondoa migongano.

(ii) Pili katika mkutano wao wa tarehe 22 Oktoba, 2008, mjini Kampala, Uganda, Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC*, *EAC* na *COMESA* walikubaliana mambo ambayo yataondo matatizo ya nchi moja kwa mwanachama wa jumuiya zaidi ya zaidi ya moja. Wakuu hao walikubaliana kwamba:-

· *SADC, EAC* na *COMESA* zianzishe Soko Huru la Pamoja. Hatua za maandalizi zimeanza kwa lengo la kuanzisha Soko Huru ifikapo Januari, 2012.

· *SADC, EAC* na *COMESA* zibuni na kutekeleza *program* za pamoja na kuimarisha ushirikiano katika Sekta za Miundombinu yaani(barabara, reli, bandari, usafiri wa anga na TEKNOHAMA.

· Baada ya kuanzisha Soko Huru la Pamoja, Ushuru wa Forodha mmoja uanzishwe. Aidha, Jumuiya hizi zimeazimia kuungana.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu faida za ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), ni pamoja na fursa nyingi zinazotokana na kupanuka kwa soko la bidhaa na huduma kuvutia uwekezaji kuendelea hali ya amani na utulivu na kuwa na sauti moja kimataifa.

Aidha, Tanzania kama nchi mwanachama wa *SADC*, inashiriki katika *program* mbalimbali zikiwemo, uendelezaji wa Bonde la Zambezi na Mabonde mengine. Uanzishwaji wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Kanda, Kuanzisha Mfuko wa Kupiga Vita UKIMWI kutangaza vivutio vya utalii kwa pamoja na kuunganisha miundombinu kama ya barabara na umeme.

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa naipongeza Serikali kwa jibu hilo kwa sababu Tanzania ilivyo kwa umbile lake Mikoa ya Kusini yaani Lindi Mtwara na Mbeya iko more *SADC* na upande wa Kaskazini Kilimanjaro mikoa kama Kagera iko *COMESA*.

Kwa hiyo, kutokana na jibu hili je kutokana na kuwa na kitu kama *Mtwara Corridor* barabara kuu ya Kaskazini ambayo sasa mmeamua kuijenga kwa lami na barabara kutoka Mtukula mpaka Tunduma.

Je, hainingkuwa vizuri kuharakisha ujenzi wa njia hizi na kuimarisha njia hizi ili kutekeleza lengo hili la Serikali la kudumisha pande zote mbili kwa lengo la kuunda kitu kimoja?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo;

Ni nia ya Jumuiya ya *SADC* kutekeleza malengo hayo, nia ni kupanua corridors zote ili kuwa na mtandao wa barabara utakaowezesha kunufaisha Jumuiya ya *SADC* kibiashara, kitalii na kadhalika.

KHALIFA SULEIMAN KHALIFA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na pole kwa mafua makali.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la kumwuliza. Kwa kuwa katika taratibu za Kimataifa nchi zinapendelewa kuwa zaidi katika soko moja ili kuimarisha masuala ya kiuchumi.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni wakati umefika sasa wa Tanzania kuachana na haya masoko ya *COMESA* na *SADC* na kuimarisha soko hili la Afrika Mashariki kwa ajili ya ufanisi wa nchi hizi?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, kwanza ni mimi niungane na wewe pamoja na Wabunge wengine kumpongeza Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, kwa kuweka historia aliyoiweka leo asubuhi. (*Makofi*)

Lakini pili naomba nitoe jibu kwa Mheshimiwa Khalifa Khalifa kuhusiana na iwapo Tanzania sasa wakati umefika wa kuachana na kanda nyingine ili tuweze *ku-concentrate* au kujihudumia zaidi kwenye ukanda wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba kwa mujibu wa swali hili ni muhimu Watanzania wakajua kwamba sisi hatukuijunga na *SADC*, sisi ni waanzilishi wa *SADC* kutohana na sababu za kihistoria. Tumemwaga damu yetu kwenye ukanda ule, tumeshiriki katika kuhamisha *frontline states* na tukaunda Jumuiya ya kiuchumi. Kwa hiyo, sisi ni waanzilishi ambao tukiondoka ghafla kwenye ukanda wa *SADC* kila mtu atatushangaa.

Tanzania sababu zake nne za kuijunga na ukanda huu ambao hatuwezi kuuacha sasa ni kwamba pamoja na majibu yote ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa sisi wanaita ni hub tuna nchi ambazo hazipo pwani na kwenye bandari kama vile DRC, Malawi na Zambia zinategemea sana bandari ya Dar es Salaam na kwa taratibu za *SADC* tunanufaika pande zote.

Lakini pia tuna kitu kinaitwa *SADC BRIGED*, sasa hivi tuna jeshi la pamoja la *SADC* ambalo limechukua mtindo wa Afrika kwa hiyo, tukiingiliwa au tukiwa na matatizo katika ukanda huu *SADC BRIGED* watafanya kazi na makao yake makuu yako Botswana. (*Makofi*)

Lakini la tatu tunaajiri wafanyakazi, tunawafanyakazi pale na tuna *quarter* ambayo watanzania wataalamu wanaajiriwa. Achilia mbali tuna kitu kinaitwa Regional Early Warning System na kwa hiyo, kwa kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa ni kwamba kwa sasa hivi siyo wakati muafaka kwa Tanzania kuachana na Jumuiya nyingine na kuingiza kwenye Afrika Mashariki peke yake, hakuna tunalolipoteza, masuala ya utalii ni kwamba sasa watalii wanatoka Afrika Kusini wanakwenda Zanzibar, masuala ya huduma ya hospitali yameenea kote na kwa hiyo si dhambi kwa sasa kwa Tanzania kushiriki katika kanda hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho *SADC Region* ndiyo the strongest Regional Grouping katika Bara la Afrika na sauti ya *SADC* ndiyo sauti ya *AU* sasa hivi, kwa hiyo, mpaka hapo tutakapokuwa na Serikali ya Afrika tuendelee kuwa wanachama wa *SADC* na wakati huohuo ni Wanachama wa Afrika Mashariki na mwaka 2012 tunaweza kuwa na hilo soko kubwa ambalo litaunganisha *SADC, COMESA* na Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, lazima tukubali kwamba ni raha kumsikiliza Waziri ambaye anajua shughuli za Wizara yake. (*Makofi*)

Sasa ni zamu ya Wizara ya Fedha na Uchumi na swali linaulizwa na Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mbunge wa Nungwi.

Na. 168

Hitaji ya Tawi la Benki Nungwi – Zanzibar

MHE. AME PANDU AME aliuliza:

Vigezo vyote vinavyotakiwa ili kuweka tawi la Benki viro Mjini Nungwi – Zanzibar.

Je, ni lini Serikali itajenga tawi la Benki ya *NMB* au *CRDB* huko Nungwi Zanzibar ambako ni kitovu cha utalii, biashara mbalimbali, hoteli n.k. na kwamba kutokuwepo kwa huduma hiyo ya kibenki kunawasababishia wananchi ushumbufu mkubwa.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mbunge wa Jimbo la Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa shughuli za utalii na biashara mbalimbali zimekuwa sana katika Mji wa Nungwi. Aidha, licha ya kukua kwa shughuli za kiuchumina kuwepo kwa miundombinu kama vile umeme, maji, mawasiliano, barabara katika mji wa Nungwi lakini bado mji huo hauna huduma ya Benki.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kuzishawishi Benki za *CRDB* na *NMB* kuangalia uwezekano wa kufungua tawi la Benki katika mji wa Nungwi baada ya kufanya tathmini ya hali ya uchumi na kuona kwamba kuna mahitaji ya Benki. Aidha, napenda pia kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kuwa, *NMB* mnamo mwaka 2008 imefungua tawi Mjini Zanzibar na Benki ya *CRDB* kuanzia Aprili, 2010 nayo pia imefungua tawi Mjini Zanzibar. Hatua hii imetokana na kilio cha baadhi ya Wabunge kutaka benki hizi zifungue matawi Zanzibar. Vilevile, hii inaonyesha dhahiri juhudhi na nia ya Benki hizo kusogea huduma zake karibu na wananchi wa Zanzibar. Kwa sasa sitaweza kusema ni lini Benki hizo zitafungua tawi katika Mji wa Nungwi, lakini jitihada zaidi za kuzishawishi Benki hizo kufungua tawi katika Mji wa Nungwi na sehemu nyingine nchini zitachukuliwa kwa nguvu zaidi na kasi zaidi. Namwomba Mheshimwa Mbunge avute subira kwani jambo zuri halitaki haraka.

MHE. AME PANDU AME: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa ruhusa ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Ni tathmini gani iliyopo zaidi ya miundombinu?

Swali la pili, je kuna uwezekano wa kuanzishwa Benki ya Wananchi ?

SPIKA : Ahsante sana kwa maswali mazuri na mafupi. Mheshimiwa Naibu waziri majibu tafadhali !

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ame Pandu Ame, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeeleza katika jibu langu la msingi kwamba mji wa Nungwi una miundombinu ya uhakika ya kuweza kuanzisha benki. Lakini kama nilivyosema kwamba kuna haja ya kufanya utafiti wa kiuchumi, utafiti ambao sasa hivi unahitajika ni kuweza kuona *to what extent* mzunguko wa fedha unavyokwenda katika mji huu ili kuweza kuweka tawi la Benki hapo Nungwi.

Mheshimiwa Spika, mimi naufahamu sana mji wa Nungwi, mji wa Nungwi ni kilomita 40 kutoka mjini Zanzibar, kuna uwezekano mkubwa ikawa wafanyakazi wa pale hawaishi pale wanaishi mjini kwa vile wana uhakika wa kuweka fedha zao mjini kuliko kuweka katika benki ya Nungwi. Kwa hiyo, mzunguko wa fedha ni muhimu sana kuweza kuuelewa kwamba upo wa uhakika kuweza kuwa na tawi.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili nataka nimweleze Mheshimiwa Ame kwamba fursa ya kufungua benki ya wananchi katika mji wa Nungwi ipo, kinachohitajika ni kwamba mtaji uwe si chini ya shilingi milioni 350 lakini vilevile *a single shareholder* asizidi 20% ya *share* katika kuanzisha benki hiyo.

Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge atashirikiana na Wizara yangu ili kuweza kuwashawishi wananchi wa Nungwi waanzishe benki yao ya wananchi, basi tutafanya hivyo ili benki hiyo wananchi waweze kuifungua kama watakuwa tayari kufanya hivyo yaani kutoa shilingi milioni 350 kama ndiyo kianzilishi cha kufungua benki ya wananchi. (*Makofi*)

Na. 169

Mfumo wa Bajeti Katika Mipango ya Maendeleo

MHE. HERBERT J. MNTANGI aliuliza:-

Kwa kuwa, majukumu makubwa ya Mipango ya Maendeleo kwa wananchi yamewekwa chini ya Halmashauri za Wilaya , Manispaa na Jiji na hivyo Wizara ikabaki na majukumu ya kuandaa sera na usimaizi.

Je, ni kwa nini katika Mfumo wa Bajeti, bado Wizara zinatengewa fedha nyingi za Utawala na Uendeshaji wa Idara mbalimbali wakati Halmashauri zinapata mafungu madogo ya mishahara ya watendaji na utekelezaji wa mipango michache ya maendeleo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa James Herbert Mntangi, Mbunge wa Jimbo la Muheza, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa lengo la Serikali ni kutekeleza Sera ya ugatuaji wa madaraka na raslimali (*Decentralisation by Devolution*), kwa maana ya kutoka Serikali Kuu kwenda katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Hata hivyo, ugatuaji huo utalenga katika kuiachia Serikali Kuu majukumu yake kuandaa na kusimamia Sera, kuratibu, kufanya utafiti na ufuatiliaji, kuandaa mipango ya kitaifa pamoja na kusimamia utekelezaji wake. Vilevile, kusimamia kujenga uwezo, viwango, tija na ufanisi wa watoaji wa huduma kwa lengo la kuwasaidia zaidi wananchi.

Mheshimiwa Spika, majukumu hayo ya Serikali Kuu kwa maana ya Wizara mbalimbali ndiyo yanayopelekea kubeba sehemu kubwa ya Bajeti. Hata hivyo, kutokana na azma hiyo ya Serikali, Bajeti ya Serikali za Mitaa imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka , kutoka Shilingi 981 bilioni mwaka 2007/2008 sawa na asilimia 18 ya Bajeti yote ya Serikali hadi kufikia Shilingi 2.63 trillioni mwaka 2010/2011 sawa na asilimia 27

ya Bajeti yote ya Serikali (ukiondoa deni la Taifa) wadau wa maendeleo wameitaka Serikali kutenga asilimia 25 ya Bajeti yote ya Serikali kwa ajili ya Serikali za Mitaa ukiondoa deni la Taifa ifikapo mwaka 2010/2011, lengo hilo limefikiwa katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 na kwa mwaka wa 2010/2011 ni zaidi ya lengo hilo. (*Makofii*)

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa. Lakini vilevile kwa picha hii kwamba ongezeko lipo kila mwaka katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, zipo bado Halmashauri nyingi ambazo hazijakuwa na vitengo vingi ambavyo vinaonekana viro katika Wizara lakini katika Halmashauri havipo. Kwa mfano, Wizara ya Maliasili na Utalii, katika Halmashauri nyingi kitengo cha utalii hakipo, ukienda Wizara kwa mfano ya Viwanda na Biashara, eneo la viwanda katika Halmashauri nyingi halipo japokuwa tuna biashara na yenyele iko chini ya Idara ya Mipango na hivyo hivyo ukienda katika Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Kitengo cha Umwagiliaji kiko zaidi katika kanda na siyo katika Halmashauri zenyele.

Sijui Mheshimiwa Waziri anatueleza nini hapo katika kuendelea kuimarisha Sekta hizo nilizotitaja na kuzipa nguvu zaidi Halmashauri zetu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza na Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, kama ifuatavyo.

Jukumu la Wizara ya Fedha ni kutafuta fedha kabla, kuzisaidia Halmashauri na Taasisi mbalimbali kuendeleza majukumu yake. Mimi nataka nimshauri Mheshimiwa Mbunge pamoja na Halmashauri zote, kama hawana vitengo ambavyo wao wenyele wanaona kwamba ni muhimu kwa maendeleo ya Halmashauri hizo ni vema wakakaa pamoja na TAMISEMI pamoja na Wizara husika ili kuona uwezekano wa kuanzisha vitengo hivyo na Wizara husika itakuwa tayari kutoa fedha kwa ajili ya kuendeleza vitengo hivyo na kuziendeleza Halmashauri hizo. (*Makofii*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, viko vyanzo vingine vya mapato ndani ya Halmashauri zetu za Wilaya na Miji kwa mfano usambazaji wa televisheni kama ilivyo katika Manispaa ya Singida na kwa kuwa chanzo hicho kinalipiwa moja kwa moja Wizarani badala ya kulipiwa kwenye Halmashauri husika.

Je, hamwoni kwamba kwa kufanya hivyo ni kuzinyima Halmashauri vyanzo vingine vya mapato ambavyo ni muhimu sana kwao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, katika Kanuni za Fedha kuna vyanzo vinge na vimeviwekwa *very clear* kwamba hivi vitakusanywa na Serikali Kuu na hivi vitakusanywa na Halmashauri kwa maana ya kuendeleza Halmashauri.

Ninachotaka kumshauri Mheshimiwa Diana Chilolo, ni vema Halmashauri ambazo wana vyanzo ambavyo mapato yake yanapelekwa Wizarani, ni vema wakakaa na Wizara husika na kuona jinsi gani ya kuweza kuandaa utaratibu wa vyanzo hivyo kuviachia Halmashauri ili Halmashauri ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Sisi kama Wizara ya Fedha tumeshatoa mwongozo ni vyanzo gani tutakusanya Serikali Kuu na ndivyo vitakavyosimamiwa na Wizara ya Fedha na ni vyanzo gani vitakusanywa na Halmashauri mbalimbali.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo wakae pamoja na Wizara husika ili kuona kwamba waweze kuziachia Halmashauri vyanzo hivyo.

Na. 170

Maandalizi ya Ununuzi wa Mahindi

MHE. PAUL P. KIMITI aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imejitahidi sana kununua mahindi katika msimu huu kwa ajili ya Ghala la Taifa la Hifadhi ya Chakula, na kwa kuwa bado baadhi ya mahindi ya msimu uliopita hayajanunuliwa yote Mkoani Rukwa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusomba mahindi yote toka maghala ya Sumbawanga, Songea na Makambako ili yapelekwe kwenye masoko ya Dar es Salaam na Dodoma ili kutoa nafasi kwa mahindi ya msimu huu?

(b) Kwa kuwa, mwaka huu Mkoa wa Ruvuma unatarajiwा kuvuna tani nyingi za mahindi.

Je, kwa nini Serikali isianze kuandaa magunia na dawa za kuhifadhia mahindi ili kuwa na maandalizi mazuri kuliko msimu uliopita?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Paul Peter Kimiti Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kila mwaka *NFRA* yaani *SGR* kama ilivyokuwa ikiitwa zamani, hununua mahindi kutoka kwa wakulima hususan kwenye maeneo yenyе ziada ya chakula katika Kanda ya Sumbawanga, Makambako na Songea na baadaye kuhamisha nafaka kupeleka kwenye kanda zenyе maeneo yenyе upungufu wa chakula.

Hivi sasa uhamishaji wa mahindi kutoka Kanda za Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ulioanza mwishoni mwa mwaka 2008/2009 bado unaendelea katika mwaka huu wa 2009/2010.

Hadi kufikia Mwezi Mei, 2010, jumla ya tani 125,900 za mahindi zilikuwa zimehamishwa kutoka Kanda za Sumbawanga, Songea na Makambako kwenda Kanda za Arusha, Dodoma, Shinyanga na Kipawa Dar es Salaam. Hatua hiyo inakusudiwa kutoa nafasi ya maghala kwa ajili ya kuhifadhi mazao yatakayoyonunuliwa katika msimu wa 2010/2011.

(b)Mheshimiwa Spika, katika msimu ujao wa 2011/2012 *NFRA* imejipanga kununua mapema vifaa kama vile magunia, maturubai na madawa ya kuhifadhiya akiba ya chakula. Tayari mchakato wa kununua magunia na maturubai umekwishaanza. Mchakato wa kununua mdawa utaanza Mwezi Julai, 2010. Kwa sasa *NFRA* inayo akiba ya madawa ya kutosha kuanzia ununuza msimu wa 2010/2011. (*Makofit*)

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita nilikuwa Sumbawanga na pale Sumbawanga mpaka sasa tani 25,000 za Mahindi hazijasombwa, hivyo Mheshimiwa Waziri naomba anihakikishie huo utaratibu anaosema unaendelea ni kweli wakati kuna tani 25,000 hazijasombwa?

Pili, kwa sasa tunatarajia tutakuwa na mavuno mengi na tulidhani Mheshimiwa Waziri katika kipindi hiki angefanya kila jitihada kushirikiana na Wizara ya Fedha ili fedha zipatikane ili tupate nafasi ya mazao ambayo tutayapata msimu huu ambayo yatakuwa ni makubwa ili tuweze kuwa na mahali pa kuhifadhi.

Je, Waziri anajiandaa vipi kuhakikisha kwamba angalau yale Mahindi yaliyopo pale Sumbawanga kwa sasa yanaondoka ili yawape nafasi wakazi wa Sumbawanga ambao kwa bahati mbaya Serikali imeagiza hawataruhusiwa kuuza Mahindi nje ili *SGR* inunue. Kuna mpango gani katika suala hilo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kusema kwamba miezi miwili iliyopita kulitokea ombi kwamba kuna chakula kingi sana kule Sumbawanga kwa hiyo, *NFRA* iende ikanunue Mahindi yale. Wizara yangu ilitoa shilingi bilioni 5 na Wataalamu wakaenda Sumbawanga lakini hakuna hata gunia moja lililonunuliwa kutoka kwa hao watu anaosema wana Mahindi.

Kwa hiyo, chakula chote ambacho kilikuwa kinunuliwe Sumbawanga kilinunuliwa na hivi sasa Serikali kama nilivyosema tunaendelea na usombaji wa chakula hicho ambacho kiko kwenye maghala ambacho kilishanunuliwa kusudi chakula kile kiweze kwenda maeneo ya Dar es Salaam, Dodoma na Arusha kusudi kuacha nafasi kwa ajili ya mavuno mapya.

Tayari Serikali imekwishatenga fedha na kama nilivyosema maandalizi ya ununuzi wa chakula kingine tayari. Kwa hiyo, napenda kukuhakikishia Mheshimiwa Kimiti kwamba fedha ambazo zimetengwa kwenye Bajeti ya mwaka huu ambayo na wewe umeshiriki kuipitisha basi zitakwenda kununua chakula kule Sumbawanga ili kiweze kwenda maeneo ambayo yana upungufu wa chakula.

Lakini pia kwa kuwa Sumbawanga au Mkoa wa Rukwa, Mbeya na Ruvuma ni mikoa ambayo inavuna sana chakula, tulishatoa ruhusa ya kuuza chakula nje ya nchi kwa wafanyabiashara kuomba vibali kwa kupitia kwa Wakuu wao wa Wilaya maana wale ndio wanajua hali ya mavuno kwenye Wilaya zile kwenda mkoani itufikie Wizarani ndio tunatoa kibali.

Lakini kibali kinaanzia Wilayani na yule anayeuzza lazima awe na leseni ya kuuza chakula ama kusafirisha nje ya nchi. (*Makofi*)

SPIKA: Naona ni Rukwa tupu, Mheshimiwa Said Arfi halafu Mheshimiwa Mwananzila. (*Makofi*)

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru nilikuwa na swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mkoaa wa Rukwa unazalisha hususan mahindi kwa wingi na kwa kuwa tuna viwanda vya kusagisha mahindi kuwa unga tatizo lililokuwa limejitokeza wakulima hawawezi kuuza mazao yao kiwandani moja kwa moja kwa sababu Serikali imeagiza itoze kodi ya asilimia 2 yaani *withholding tax* kwa wakulima.

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya hatua hii ambayo itawavunja sana moyo wakulima wa mahindi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimwa Spika, masuala ya kodi au *Withholding Tax* hayo ni masuala ya mapato yanahusiana na Wizara ya Fedha na Uchumi, masuala ya *Revenue* hayo ambayo yana *implications* katika mapato ya nchi. Kwa hiyo nisingependa kuyazungumzia kwa sasa hivi mpaka yafanyiwe uchunguzi wa kutosha. (*Makofii*)

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimwa Spika, nashukuru kupata fursa hii, ningependa kuuliza swalii dogo. Kwa sababu mahindi haya tunayozungumza kutoka mkoa wa Rukwa ni mengi na uchukuzi unaofanyika ni kwa Makampuni ambayo yanatoka nje ya mkoa wa Rukwa yaani Dar es Salaam, Arusha na sehemu nyingine wakati wafanyabiashara wenye magari pale Sumbawanga hawapati fursa ya kuweza kupata hii tenda za kuchukua hayo mahindi kuyapeleka huko yanakohitajika.

Je, Wizara haioni kwamba ni muhimu sana kuwafikiria wafanyabiashara wa Rukwa wapewe fursa ya kusafirisha mahindi hayo badala ya kwenda kuwachukua watu kutoka mbali wasafirishe mahindi na wananchi wa mkoa wa Rukwa wanakosa fursa hiyo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kusema kweli nakubaliana na Mheshimiwa Mwananzila kwamba ni vyema pia kuwaruhusu na kuwahusisha wafanyabiashara wa mkoa wa Rukwa na maeneo hayoyanayozalisha chakula kusudi na wao pia wapate *opportunity* ya kusafirisha chakula kwa sababu chakula kile kinatoka maeneo yao. Kwa hiyo namwomba RAS wa mkoa wa Rukwa, Ruvuma pamoja na Mbeya waweze ku-*identify* watu hao ambaa wana sifa.

Lakini vile vile niseme kwamba tunavyotangaza tenda hatuchagui eneo lakini pia kuna umuhimu wa ku-*consider* watu wanaotoka maeneo hayo.

Na. 171

Serikali Kuwazuia Wakulima Kuuza Mazao Nje ya Nchi

MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA (K.n.y. MHE. SALIM HEMED KHAMIS) aliuliza:-

Serikali ilipojibu swalii la Mheshimiwa Lucy Mayenga, katika Mkutano wa Kumi na Nane, ilisema kuwa upungufu wa nafaka ulifikia tani 1,348,445 mwaka 2009 na kutohana na hali hiyo Serikali ikasitisha uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi, lakini mwezi Februari, 2010 imeripotiwa na vyombo vya habari kuwa, kuna zaidi ya tani 500 za Mpunga wenye thamani ya zaidi ya shs. Milioni 800 kwenye maghala huko Mbarali zikisubiri soko:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, haikufanya utafiti wa kutosha kabla ya kueleza hali ya chakula nchini?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kuendelea kumzuia mkulima asiuze mazao yake nje ya nchi kunaongeza umaskini na kudumaza maendeleo ya mkulima wa Tanzania?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Khamis kuwa Serikali ilifanya utafiti wa kutosha kabla ya kuelezea hali ya chakula nchini kwa lengo la kuiwezesha Serikali kutimiza jukumu la kuhakikisha usalama wa chakula wakati wote.

Kila mwaka Serikali kupitia Wizara yangu kwa kushirikisha wataalam wa Wizara, Halmashauri za Wilaya na Mikoa yote nchini hufanya tathmini za kitaalam za uzalishaji na upatikanaji wa chakula nchini.

Tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula msimu wa 2008/2009 na upatikanaji wa chakula mwaka 2010 ya mwezi Mei, 2009 ilionyesha kuwepo kwa upungufu wa takriban tani milioni 1.35 za nafaka katika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, napenda kufafanua kuwa, si sera ya Serikali kuzuia mazao ya chakula nje ya nchi hasa katika kipindi hiki cha sera ya soko huria.

Hatua ya Serikali ya kuzuia uuzaaji wa mazao makuu ya chakula nje ya nchi ni ya muda mfupi inayolenga kuhakikisha upatikanaji wa chakula katika nyakati za uhaba wa chakula nchini na kudhibiti upandaji wa bei.

MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, Serikali haioni ni vizuri kujenga maghala ya kutosha na kuhifadhi chakula cha kutosha wakati wa chakula ili kuweka chakula cha ziada na kuwaachia wakulima wauze chakula chao nje? (*Makofsi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na yeche kabiso kwamba kuna haja ya kujenga maghala ya kutosha kusudi tuweze kununua chakula kingi na tuweze kukihifadhi kwa ajili ya matumizi ya baadaye siku za njaa, lakini hata sasa hivi maghala tuliyonayo yanatosha kuhifadhi chakula takriban tani 220,000 ambayo katika miaka 5 iliyopita hatujawahi kujaza maghala hayo.

MHE. FATMA M. MAGHIMBI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kuna kauli mbiu inayosema maisha bora kwa kila Mtanzania.

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kufanya haraka kwenda kuzinunua hizi tani 500 zilizoko Mbarali ili wana-Mbarali nao waweze kuyaona hayo maisha bora?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza kwamba anakubali hii kauli mbiu yetu ya maisha bora kwa kila Mtanzania.

Lakini pili, niseme kwamba hawa wafanyabiashara wa Mbarali walichokifanya ni kununua mchele mwingi na kuuhodhi wakisubiri bei ipande na ndio waliosababisha kupanda kwa bei ya mchele tofauti na mwaka 2008.

Mwaka 2009 imepanda kwa asilimia 35. Wafanyabiashara hawa wamehodhi ili bei iweze kupanda, lakini baada ya kuona sasa mavuno yanakuja kwa wingi ndio wanataka wauze, ndio wanasema hakuna soko.

Kwa hiyo tunapenda kusema na kuwashauri wafanyabiashara kwamba wasihodhi mazao, mazao yale wayaache yaende kule yanakokwenda kwa wakati muafaka kwa sababu wanavyoyahodhi inafikia wakati wanakosa biashara. Lakini kwa sasa hivi tumeshawaruhusu wauze. Kwa hiyo, wanaweza wakauza nje ya nchi bila matatizo yoyote ili mradi waombe vibali kwenye mamlaka zinazohusika.

Na. 172

Kuanzishwa Kwa Benki ya Taifa ya Ushirika

MHE. JANET B. KAHAMA aliuliza:-

Zipo taarifa kutoka Shirika la Vyama vya Ushirika la Tanzania (*TFC*) kwamba, Mchakato Mzima wa kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika iliyopendekezwa katika Mpango Kabambe wa Mwaka 2005 wa kuboresha tija na ufanisi katika mfumo wa Vyama vya Ushirika ili uiendane na mtindo wa kisasa kwa kuendesha biashara ulikamilika Mwaka 2009, na taarifa rasmi kutolewa kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika:-

(a) Je, kama hivyo ndivyo, ni vikwazo gani ambavyo vinachelewa uanzishwaji wa Benki hiyo muhimu?

(b) Je, Serikali inatambua kwamba kuwepo kwa Benki ya Taifa ya Ushirika ni muhimu kwa Maendeleo na uhai wa ushirika nchini na hasa kutokana na mzigoto mkubwa unaobebeshwa Vyama vya Ushirika kutokana na masharti magumu yatolewayo na Benki za Biashara kwa Vyama vya Ushirika?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba Jumuiya ya Wanaushirika nchini kupitia Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) wapo kwenye mchakato wa kuanzisha Benki yao ya ushirika chini ya msukumo wa utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika ya Mwaka 2005. Hata hivyo mchakato huo haujakamilika na kwa hiyo suala hilo halijafikishwa Serikalini kwa ajili ya hatua za utekelezaji.

(b) Serikali inakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, kwamba kuna umuhimu wa kuwepo kwa Benki ya Ushirika ya Kitaifa yenye lengo la kuisogeza huduma za Kibenki na zenyenye gharama nafuu kwa Vyama vya Ushirika na wanachama wake.

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Benki ya Taifa ya Ushirika ilianzishwa na ilitaifishwa wakati wa Azimio la Arusha mwaka 1967 na mali zake zote zile zilichukuliwa zikakabidhiwa katika Benki ya Biashara NBC.

Hapo hapo Shirikisho la Wanaushirika (*TFC*) na lenyewe lilikuwa limepokonywa mali zake ambazo zina hisa ya shilingi milioni 800 na hizo pia baada ya kupokonywa ziliwekwa katika *Cooperative Rural Development* ambayo ni *CRDB* na ilitaifishwa ikawa *CRDB Bank Limited*. Hii inasikitisha kuwa mpaka leo hizo mali za ushirika zote hazijapata fidia mpaka leo, naomba waelewe.

Swali langu la pili, katika kuharakisha kuanzishwa Benki ya Wanawake Serikali iliingia ikajitahidi sana kutoa kimtaji ikajiingiza kusaidia uanzishwaji wa Benki ya Wanawake.

Je, sasa Serikali inaniambia nini katika kuanzisha hii Benki ya Ushirika ambayo itajumuisha wana-SACCOS wengi? Ahsante.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu mimi huwa na utaratibu wa kuwa nachukua *cutting*. *Cutting* hii nimenung'unika kwa sababu tangu Aprili, 2007, mambo haya yameandikiwa mwaka 2007, naomba kujibiwa, ahsante.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, nikiri na niombe kwamba tutafutilia hizi mali zilizokuwa Benki ya Ushirika

ambazo zilitaifishwa mwaka 1967 wakati wa Azimio la Arusha hata kabla sijazaliwa na zile za *TFC* ambazo zilihamishiwa *CRDB*.

Kwa hiyo, hilo tutalifanyia uchunguzi tutasaidiana na Mheshimiwa Kahama naona anaewa sana haya masuala ili tuweze kuangalia kwamba ziko wapi na ni vipi zinaweza zikarudi kama inawezekana. Lakini nadhani zote hizi zimekwenda kwenye Mashirika ambayo yalikuwa ni ya umma lakini hilo tutaliongea baadaye.

Swali lake la pili la kuhusiana kwamba Serikali ilisaidia Benki ya Wanawake niseme kwamba Benki zote hizi ni kwa ajili ya wananchi wetu wa Tanzania. Kwa hiyo, ebu tusubiri ile Kamati ya Shirikisho ya Vyama vya Ushirika ambayo imeundwa Novemba, 2009 na ambayo tayari imeshaandaa Mshauri Mwelekezi na Mshauri huyu ameambiwa aandae Taarifa ya Upembusi Yakinifu pamoja na Mpango Mkakati wa Benki hii na amesema kwamba atakamilisha mwezi Agosti, 2010.

Kwa hiyo, tusubiri miezi miwili hii taarifa hiyo ikishakamilika ikija Serikalini na ikiipelekwa Benki Kuu basi ndiyo tutajua mahali pa kuanzia. Lakini kama Benki ya Wanawake ilisaidiwa kwa nini Benki ya Ushirika isiweze kusaidiwa. Nadhani tupo kwa ajili hiyo. (*Makofi*)

Na. 173

Kuongezeka kwa Idadi ya Wanafunzi Vyuo Vikuu

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA aliuliza:-

Serikali imekuwa ikihamasisha Vyuo Vikuu hapa nchini kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kuijunga na masomo ya Vyuo Vikuu, lakini ndani ya muda mfupi idadi hiyo imeongezeka kwa zaidi ya asilimia mia moja (100%) kwa lengo la kutoa fursa zaidi kwa vijana Watanzania kupata elimu ya juu.

Je, Serikali ina mipango gani madhubuti ya kupanua miundombinu ya Vyuo hivyo kama vile Madarasa, Maktaba, Maabara, Hosteli na kadhalika ili kukidhi mahitaji ya idadi kubwa ya wanafunzi wanaoongezeka kila mwaka?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa idadi ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu imeongezeka kutoka 55,500 mwaka 2005 na kufikia 118,000 kwa mwaka 2010. (*Makofi*)

Ili kukamilisha upanuzi huu, Serikali imeandaa M pango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (MMEJU), (kuanzia mwaka 2011/2012 hadi mwaka 2015/2016).

Katika kutekeleza mpango huu Serikali itakarabati miundombinu mbalimbali ya kujifunzia, kujenga na kupanua huduma za Vyuo Vikuu. Aidha, itaweka vifaa vipya katika maabara na karakana za Wahandisi. Itaongeza vyumba vya miadhara, mabweni ya wanafunzi, kukarabati mabwalo ya chakula (*cafeteria*) na ukarabati wa miundombinu ya TEHAMA.

Sambamba na mpango huu, Serikali inatekeleza Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu (*Science, Technology and Higher Education Project*). Mradi huu unaotumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia, unalenga kuimarisha ufundishaji wa Sayansi na Ualimu, Kusomesha Wahadhiri, kuimarisha Taasisi zinazohusika moja kwa moja na utoaji huduma kwa Vyuo vya Elimu ya Juu, kujenga miundombinu mipy, pamoja na kuimarisha vyuo vikuu katika masuala ya TEHAMA na maktaba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ongezeko kubwa la wanafunzi vyuoni na uhaba wa Wahadhiri, Serikali ina mpango wa kuvunganisha vyuo vikuu vya Umma kwa njia ya mtandao ili viweze kufundisha kwa kutumia mtandao. Awamu ya kwanza ya mpango huu itavihuisha Vyuo Vikuu vya Umma na Taasisi za Utafiti 27. Mtandao huu utawezesha wanafunzi kuungana na kufuatilia vipindi vya masomo hata bila kuwa darasani.

Aidha, mtandao utasaidia wanafunzi na Wahadhiri katika kufanya tafiti mbalimbali na uwasilishaji wa ripoti. Kwa kuvunganisha vyuo kwenye mtandao mmoja, vyuo pia vitaweza kubadilisha taarifa za kitaaluma pamoja na majarida yaliyopo kwenye maktaba zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inavipatia vyuo vikuu vya umma fedha za maendeleo ambazo hutumika katika masuala ya ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya vyuo. Aidha, Mamlaka ya Elimu Tanzania imekuwa ikitoa mikopo kwa Taasisi za Elimu ya Juu ili pamoja na mambo mengine ziweze kujenga na kuimarisha miundombinu, maabara, karakana, kumbi za miadhara na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Awamu ya kwanza ya ujenzi imekwishakamilika na chuo kinadahili wanafunzi. Awamu ya pili ya ujenzi imeanza na inatarajiwa kukamilika mwaka 2015, wakati huo chuo kitakapomilika, kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 40,000.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikihamasisha Taasisi, Mashirika, watu binafsi na wadau wengine wa Elimu ya Juu kuwekeza katika kujenga mabweni na upanuzi wa utoaji elimu ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na Elimu ya Juu. Hadi sasa kuna vyuo vikuu 21 visivyo vya Serikali na ambavyo vimedahili asilimia 25% ya wanafunzi wote walioko vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza wadau wote wa elimu kwa michango yao ya dhati katika kuchangia elimu ya juu na kuwaomba waendelee na moyo huo.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza maswali madogo mawili kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Chuo Kikuu cha Sokoine ni chuo pekee cha Kilimo nchini Tanzania kinachotoa digrii ya kwanza, *Masters* pamoja na *Ph. D.* kwa masuala ya Kilimo. Na kwa kuwa miaka yote fedha ambazo zinazotolewa za maendeleo kwa chuo hiki ni ndogo kiasi cha kwamba chuo kimeshindwa kujipanua na hivyo kuwa na uhaba mkubwa wa Wahadhiri, Maabara, miundombinu ya kila kitu pamoja na maktaba.

Sambamba na suala la kilimo kwanza ambalo limeletwa na Serikali. Serikali ina mpango gani wa haraka wa kupanua chuo hiki kwa kutoa fedha za kutosha ili tuweze kwenda na *speed* ya kilimo kwanza?

Suala la pili, kwa kuwa Serikali imesema ina mpango wa kuunganisha wanafunzi na Wahadhiri kupata elimu kwa njia ya mtandao. Na kwa kuwa elimu ambayo inayotolewa kwa njia ya mtandao ni elimu nadharia na elimu inayomjenga mtoto wa Tanzania ili tupate elimu bora na sio bora elimu ni elimu ya nadharia na vitendo.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba wanafunzi wale wanaopata elimu kwa njia ya mtandao wanapatiwa pia elimu kwa njia ya vitendo? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA): Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa kuonesha kwamba, anafuatilia kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, naomba niweke bayana kwenye Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali hii sikivu, kwa kutambua kwamba, Kilimo ndiyo Uti wa Mgongo na ndiyo Kilimo Kwanza, tunategemea mambo mengi. Katika Bajeti itakayosomwa na Waziri mwenye dhamana, ataelezea ni kiasi gani Vyuo Vikuu na hasa Chuo Kikuu cha Sokoine kimetengewa fedha. Naogopa nikisema sasa tunaweza tuka *pre-empt* hotuba yake. Kwa hiyo, naomba nimuahidi kwamba, tumetoa kipaumbele na kama tunalivyoona, zipo fedha kadhaa zilizotengwa kwa ajili ya tafiti mbalimbali ili kuwekeza zaidi kwenye elimu kwa wahadhiri wa kada mbalimbali.

Kuhusu ufundishaji kwa kutumia mtandao, yaani *tele-conference*, Wanafunzi watapata mafunzo haya ya mtandao pale inapobidi na mafunzo kwa vitendo yataendelea kupewa umuhimu. Naomba nikuthibitishe kwamba, Vyuo Vikuu vingi duniani sasa hivi wanafundisha kwa utaratibu huu. Aidha, katika jibu la msingi, tumeeleza mkakati uliopo kupitia MMEJU, namna ya kuongeza wahadhiri na kuwapa uwezo zaidi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, lakini mtakumbuka tumeanza na mambo mengine ambayo yamechukua muda wa maswali, kwa hiyo, tutafidia ule muda wa dakika kumi kwa kuendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini.

Na. 174

Huduma ya Maji Shinyanga Kutolewa na Mamlaka Mbili

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA aliuliza:-

Kwa kuwa huduma ya maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Shinyanga Mjini inasimamiwa na Mamlaka mbili za KASHWASA na SHUWASA:-

- (a) Je, ni nini uhusiano wa Mamlaka hizo katika kutoa huduma bora ya maji katika Mji wa Shinyanga?
- (b) Je, ni matatizo gani yaliyojitokeza mpaka sasa katika kutoa huduma ya maji chini ya Mamlaka mbili?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye vipengele (a) na (b), naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka mbili za Majisafi na Majitaka Kahama/Shinyanga na Shinyanga, zimeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Maji (*Water Act, 272*) ya Mwaka 1997, ambayo kwa sasa imezingatiwa kwenye Sheria ya Huduma ya Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Namba 12 ya Mwaka 2009 (*Water Supply and Sanitation Act, 2009*). Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Kahama/Shinyanga (KASHWASA), iliundwa mwaka 2007/2008 mara baada ya ujenzi wa Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria kukamilika na kutangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali Na. 45 la tarehe 23 Februari, 2007.

Lengo kuu la kuanzisha Mamlaka ya KASHWASA ni kuendesha shughuli za uzalishaji wa maji kutoka Ziwa Victoria na kuuza maji hayo kwa jumla (*bulk water*). Mamlaka ya KASHWASA inatoa huduma hyo kwa Mamlaka za Majisafi na Majitakaza Shinyanga Mjini (SHUWASA), Kahama Mjini (KUWASA) na vijiji 39 (kwa sasa) kat

ya vijiji 76 viliyopo katika Wilaya za Misungwi, Shinyanga Vijijini na Kahama. Mamlaka ya KASHWASA ilianza rasmi kazi ya uzalishaji maji na kuyasafirisha kwa wateja wake mnamo mwezi Februari, 2009.

Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya SHUWASA, inanunua maji kutoka KASHWASA na kuyasambaza kwa Wananchi walengwa katika Mji wa Shinyanga kwa bei walipanga kulingana na gharama zao za uendeshaji na kupitishwa na EWURA.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uhusiano uliopo kwa Mamlaka hizi mbili ni kwamba, KASHWASA inazalisha na kuza maji kwa jumla na SHUWASA inanunua maji yaliyozalishwa na KASHWASA na kuyasambaza kwa wateja wake na kukusanya mapato.

(b) Mheshimiwa Spika, Mamlaka zote mbili zinafanya kazi chini ya Wizara yangu na makubaliano yamewekwa kati ya Wizara yangu na Mamlaka hizo kwenye Mkataba wa Maridhiano (*Memorandum of Understanding – MoU*). Vile vile Mamlaka hizi zimesaini Mkataba Maalum wa Kuza Maji (*Bulk Water Purchase Agreement*), ambao umeainisha majukumu ya kila Mamlaka. Hadi sasa, hakuna matatizo makubwa yaliyojitekeza ambayo yangesababisha kuathiri utoaji wa huduma. Pamoja na hayo, changamoto hazikosekani hasa pale panapokuwa na biashara ya muuzaji na mnunuzi, kumekuwa na kutoridhika kwa mnunuzi (SHUWASA) kulipia kiwango cha maji anayodaiwa na (KASHWASA) kutohana na upotevu wa maji uliokuwepo wakati wa urekebishaji wa miundombinu. Wizara yangu inafuatalilia kwa karibu sana mgongano huo na hatua zinazostahili zinatekelezwa kupitia Bodi mbili za Mamlaka hizo mbili. Nampongeza Mheshimiwa Dr. Mlingwa, kwa ufuatilaji wake wa karibu sana kuhusu maji Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii ya kujibu swal linalohusu maji mijini, kuwapongeza na kuwashukuru Wananchi wa Mugumu Serengeti, kwa kukabidhiwa na kuupokea Mradi wa Kihistoria wa Bwawa la Manchira na Mradi wa Maji Mjini Mugumu na mapokezi makubwa walijompatia Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alipozindua Mradi huo Ijumaa iliyopita, tarehe 2 Julai, 2010.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina swal moja tu la nyongeza. Niendelee kuipongeza Serikali kwa huduma hii muhimu ya maji kutoka Ziwa Victoria kuja Shinyanga. Kama alivyokiri Mheshimiwa Waziri kuwa, bado kuna changamoto na moja ya changamoto iliyopo ni kukosekana kwa mfumo wa utoaji wa huduma ya maji unaojiendesha wenyewe katika tanki kubwa la maji pale Old Shinyanga; yaani *Automatic System* ya kufungua na kufunga maji kutoka KASHWASA kwenda tanki la SHUWASA lililopo pale Old Shinyanga, kiasi kwamba, wakati mwingine maji yanafunguliwa kwenda kwenye tanki la KASHWASA mpaka tanki hilo linajaa na linaanza kutiririsha maji ovyo na kwa hiyo SHUWASA wanalipia maji yasiyotumika au wakati mwingine mtambo unakuwa umezimwa na kwa hiyo tanki linaishiwa maji, Wananchi wa Shinyanga Mjini wanakosa maji.

Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali anatuhakikishia kuwa mtambo huo unaojindesha wenyewe utawekwa lini ili kuondoa tatizo hili na kuwahakikishia Wananchi wa Shinyanga Mjini upatikanaji wa maji wakati wote na SHUWASA kuweza kulipia maji yanayolipiwa na wateja?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, Mradi wowote ule ambaa ni mpya, lazima kunakuwa na hitilafu za hapa na pale katika urekebishaji hasa unapounganisha Mradi wa zamani na Mradi mpya. Mradi wa Kahama Shinyanga ni mpya na kwa sehemu, usambazaji wa maji Shinyanga Mjini ni mfumo wa kizamani. Asilimia 40 tu ya mfumo huo ni sehemu mpya, ambaa tumelaza mabomba mapya na asilimia 60 iliyobaki tutaendelea kulaza mabomba mapya kwa gharama ya karibu shilingi bilioni 12 na tutafanya hivyo awamu kwa awamu.

Kuhusu tatizo la pale Old Shinyanga, ambapo kunatakiwa kuwe na mfumo ambaa unajirekebisha wenyewe, hili ni suala la kiufundi ambalo halitatupa matatizo na nimeziagiza Mamlaka zote mbili ziangalie tatizo hili ili waweze kurekebisha mapema iwezekanavyo. Siyo jambo ambalo litatushinda.

MHE. DR. SAMSON F. MPANDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa maswali mengi kutoka kwa Wabunge yanahusiana sana na matatizo ya maji nchini kote; je, unaonaje ukaweka Idara ya *Consultation* katika Wizara yako ili kutatua matatizo madogo madogo ambayo yangeweza kutatuliwa pale Wizarani badala ya kuja kukabana hapa Bungeni?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda ni mdau mkubwa wa Sekta ya Maji na anatoka huko, kwa hiyo, anaifahamu sana Wizara yangu na siku zote ushauri wake tunautilia maanani. Kwa hiyo, hilo la kuhusu masuala ya uelekezi kutoa ushauri hasa kwa Halmashauri tutalizingatia.

Kubwa zaidi siyo kukabana humu Bungeni na ninashukuru sana hamkunikaba koo wakati wa Bajeti yangu, lakini ninataka kusema tu kwa habari njema na hii narudia alichokisema Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alipokuwa anazindua Mradi wa Manchira, amebaini kwamba, Bajeti ya Wizara ya Maji haitoshi na kwamba, naomba tumpe kura zote; atakapopata tena Urais ataongeza maradufu Bajeti ya Wizara ya Maji. Haya ni maneno yake mwenyewe. Ahsante sana. (*Makofifi*)

Na. 175

Ombi la Kuwapatia Maji Wananchi wa Mbozi

MHE. GODFREY W. ZAMBI aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikubali ombi la Wananchi wa Mbozi hasa wa Kata za Mlangali, Iyula, Ruanda na Muyovizi kuwapatia maji kupitia Mradi wa Maji Lukululu Group:-

Je, Mradi huo umefikia wapi na unategemewa kukamilika lini?

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mradi wa Maji wa Lukululu Group umeibuliwa na Wananchi kwa ajili ya kuhudumia vijiji 12. Kati ya hivyo; vijiji 6 ni vya Kata ya Mlangali ambavyo ni Ukululu, Mlangali, Mbewe, Shaji, Ndolezi na Shomora na vijiji 6 vya Kata ya Muyovizi ambavyo ni Idunda, Mahenje, Ichesa, Ivugula, Muyovizi na Mbulu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Lukululu Group umeanza mwezi Januari, 2010 kwa kufanya upimaji wa maeneo ya ujenzi wa miundombinu kwenye vijiji vyote ambavyo vitahudumiwa na Mradi huo. Kazi ya upimaji imekamilika mwezi wa Machi, 2010. Hivi sasa utekelezaji wa Mradi upo kwenye hatua ya usanifu na kutayarisha makisio ya gharama ya ujenzi, kazi ambayo inafanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kwa kushirikiana na Ofisi ya Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya. Kazi inategemewa kukamilika mwezi Agosti, 2010.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga shilingi milioni 150 katika mpango wa mwaka wa 2010/2011 kwa ajili ya Mradi huo. Serikali itaendelea kutoa fedha kulingana na upatikanaji wa fedha Serikalini kwa ajili ya Mradi huo ambao ujenzi wake unakadirisha kuchukua miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa juhudi zake kubwa za kuisukuma Wizara kuhusu utekelezaji huu. Vilevile napenda kumjulisha kwamba, tunatarajia Mradi wa Mloo utakuwa umetekelizwa na kukamilika mwisho wa mwezi wa Julai.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Je, pamoja na kunishukuru mimi sasa atakubali kupokea shukrani za Wanambozi na hususan za Wanamloo kwa *speed* yake ya kutekeleza Mradi wa Maji wa Mloo na kumaliza tatizo sugu pale Mloo? Je, atakuwa tayari kuongeza kasi ya usukumaji wa Miradi ya Maji katika Wilaya ya Mbozi ili Wananchi waweze kupata maji safi na salama?

(ii) Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba vijiji 12 vya Kata za Mlangali na Muyovizi vimetengewa shilingi milioni 150 kwa mwaka huu wa fedha. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba shilingi milioni 150 kwa Mradi wa Vijiji 12 ni pesa kidogo sana; na je, atakuwa tayari kutenga fedha zaidi kwa mwaka wa fedha ujao?

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge umeuliza matatu hapo, lakini Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Mlowo katika Wilaya ya Mbozi, naomba kusema kwamba, hii ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alipokuwa anapita Mlowo kwenda Kamsamba hivi karibuni na sisi tunatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, shukrani alizozitoa nazipokea kwa niaba ya Serikali, lakini hasa nitamfikishia anayepaswa kupewa shukrani hizo, naye ni Mheshimiwa Rais.

La pili, kuhusu Mradi wa Lukululu; miradi yote kabla hatujaifanyia usanifu, huwa hatujui gharama zake halisi, kwa hiyo tunatenga fedha ili kuuweka ule mradi katika vitabu vya Serikali. Gharama halisi za Mradi wa Lukululu zitajulikana baada ya zabuni kutangazwa hivi karibuni. Kwa hiyo, angalau shilingi milioni 150 zipo na iwapo kwa awamu ya kwanza tutazihitaji zitatosha sawa, kama hazitoshi basi kuna njia mbalimbali za kuutekeleza huu Mradi kwa maana ya kwamba, tunaweza kuwa na *re-allocation* au kwa mwaka huu zisipotosha kwa sababu labda ya chanzo tu, lakini kwa mwaka unaofuata tutakuwa tumefahamu gharama halisi ya Mradi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, kama anavyokumbuka, Mradi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe ulianza kwa kutengewa shilingi milioni 200 lakini sasa ni zaidi ya shilingi bilioni 30. Ahsante.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yanayotia matumaini na hasa kujua rasmi kwamba, Mheshimiwa Rais Kikwete atakaporejea katika awamu nyingine Serikali yake, ataongeza Bajeti ya Maji maradufu. Hiyo ni habari nzuri sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasoma matangazo, niseme tu kuna baadhi ya watu katika jamii wanasema kwamba, tunapotambulisha wageni tunapoteza wakati na dhana hii inatokana na mawazo ya zamani ya kibwanyenye kwamba, kuna watu wadogo na kuna watu wazito. Bunge hili la viwango, linazingatia kwamba, sisi tumetokana na watu. Tunazo taratibu zetu zilizo tofauti kwa sababu sisi hapa tunapigiwa kura na haohao wanaosemekana ni wadogo. Kwa hiyo, kuwaenzi Watanzania wa kawaida wanapokuja Bungeni ni jambo ambalo tumelianzisha katika Bunge hili la Tisa; jambo linalopendwa na Wananchi wetu na linaondoa ule unafiki wa kusema Wananchi wana maana kwetu wakati wa kura tu. Tutaendelea kuwatambua hivi hivi kwa sababu wao ndiyo wanatuweka hapa. (*Makofi*)

Halafu niseme tu, kilicho kikubwa katika michango ya Bunge siyo kutumia muda mrefu kama wengine wanavyosema wanapoteza muda; cha maana ni ubora wa maamuzi yanayochukuliwa na Bunge kama yana manufaa kwa Wananchi. Mimi ninaamini maamuzi mengi sana tuliyofanya katika Bunge la Tisa, yamekuwa na manufaa makubwa

kwa Wananchi. Kwa hiyo, hata pale tunapopata mjadala mfupi, kumbukeni kuwa, kazi kubwa imefanyika kwenye Kamati na ndiyo maana mambo mengi yanayoamuliwa hivi sasa ni moja kwa moja yenyé manufaa kwa watu wetu.

Waheshimiwa Wabunge, wageni. Wageni wa Mheshimiwa Margaret Sita, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni Watendaji Wakuu wa Wizara, ambao ni pamoja na Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi na Wakuu wa Vitengo na Maafisa Mbalimbali wa Wizara. Wote hao wanaongozwa na Bi. Mariam Mwaffisi, Katibu Mkuu. Ahsante sana Katibu Mkuu, kwa kazi yako nzuri ya kuwasaidia Waziri na Naibu Waziri, ninapata taarifa zako mara kwa mara, kwa hiyo, nashukuru sana. (*Makofiki cheko*)

Sasa naomba wale waliofuatana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mendeleo ya Jamii wasimame. Wale pale, ahsante sana.

Wageni maalum wa Wizara hiyo ni Wawakilishi wa Washirika wa Maendeleo ambao pia ni Balozi na Asasi zisizo za Kiserikali kama ifuatavyo: Bi. Salome Anyoti, Mwakilishi wa UNIFEM; Bi. Lucy Merere, Mwakilishi wa Ubalozi wa Ireland; Ndugu Joan Zum, Mwakilishi wa Ubalozi wa Uhlanzi; Bi. Christina Hopenova Harnofer, Mwakilishi wa UNICEF, *welcome to the House. We are happy to see you representing one of the development partners; thank you very much.* Kuna Ndugu Francis Mtitu, Mwakilishi wa PLAN INTERNATIONAL; Ndugu Engelbert Mwangali, Mwakilishi Msaidizi wa UNICEF; Ndugu Ummy Mwalimu, Mwakilishi wa Ubalozi wa Denmark; na Bi. Vicky Mushi, Mwakilishi wa Ubalozi wa Canada.

Wapo Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii wanen; naomba wasimame; asanteni sana. Wapo Watumishi 24 kutoka Manispaa ya Mkoo wa Dodoma, wengine walikosa nafasi labda wako kwenye *Basement*; Oh! wale pale kushoto, karibuni sana, wanaongozwa na ndugu Minja, ambaye ni Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii wa Moka; ninaomba asimame peke yake; asante sana.

Waheshimiwa Wabunge, wapo Watumishi watano kutoka Halmshauri ya Wilaya ya Bahi Dodoma ni Wilaya Ambato iko jirani, isije ikawa wale wa Bahi wamekwenda Mtera. Pia kuna Watumishi watano kutoka Wilaya ya Chamwino. Wako Viongozi 10 wa Baraza la Watoto Taifa, ambao wameongozwa na Katibu wa Baraza hilo, Ndugu Faustino Arbogast; watoto wale pale asanteni sana, tunawatachia mema katika masomo yenu.

Wageni wa Mheshimiwa Haroub Masoud, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ni mkewe Biubwa Said au naye mtera tena Oh! Ahsante sana, mzee anaendelea vizuri hapa, kwa hiyo, endelea tu kumtunza vyema. Pia yupo mwanaye Mheshimiwa Haroub anaitwa Haroub Haroub; halafu kuna Lulu Yussuf, hakutajwa uhusiano; ni mtoto mdogo eh! Kuna Ndugu Abdallah Hamis, Mratibu wa Maskani Wilaya ya Kati Zanzibar; Asante sana ooh! Lulu ndiyo yule amepakatwa.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Suzan Lyimo na Mheshimiwa Elietta Switi, ambao ni Dr. Fenela Mkangaza, Mkurugenzi wa *Gender Center* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Yupo pia Dr. Harve Moris Semakafu, Mratibu Mkazi wa Demo Finland Tanzania, wako pamoja pale karibuni sana, tunafurahi kwa kazi mnayoifanya. Pamoja na wote hao, wapo wanafunzi 160 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Mgulani Manispaa ya Temeke, wale pale asanteni sana na karibuni. Tunawapongeza walimu kwa kuwaleta watoto hapa na watoto wote tunawataktia msome vizuri, muwe raia wema wa Tanzania baadae.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wa Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, ambao ni walimu 30 kutoka Halmasahuri ya Manispaa ya Morogoro. Ahsanteni sana walimu, tunapongeza sana kazi zenu katika mazingira magumu wakati mwingine lakini nina hakika Serikali itazidi kuwaangalia nanyi muendelee na shughuli za kuielimisha Tanzania mpya.

Wapo wageni wangu mimi na Mheshimiwa Magaret Sitta, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ambao ni watoto 22 na walimu 6 kutoka Shule ya Msingi inaitwa Center for Education Plus; sijui wako wapi hawa? Ooh! Wako pale; shule hii tunailea kwa miaka minne sasa. *Education Plus* maana yake lazima uwe na zaidi ya Elimu, ndiyo falsafa yake, unaweza ukaelimika sana lakini ukakosa uzalendo, ukakosa maadili, ukawa ni kiongozi wa majambazi, unashiriki wizi na vinginevyo. Kwa hiyo, unatumia elimu na ndiyo maana shule hii inaitwa *Education Plus*, kwa sababu inafundisha toka misingi ya awali, inafundisha umuhimu wa maadili ili wasomi wa baadae waweze kuwa pia na maadili mema. Sasa wanaongozwa na wazito wafuatao; Mama Florence Mapigano, huyu ni mke wa Jaji Mapigano, unaona shule ya namna hii inasaidiwa na mke wa Jaji Mstaafu; Mwalimu Mkuu ni Elialilia Nyali; walimu wengine ni Ndugu Tumaini Msikwa; Ndugu Kalunde Msabila; Ndugu Peter Nsimba; na Ndugu Brison Adam; karibuni sana. Tunashukuru sana mmekuja, tutaonana hivi punde na ninawataktia ziara njema hapa Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya kazi; Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, anaomba niwatangazie kwamba, Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kutakuwa na kikao cha Kamati, saa saba mchana, leo tarehe 5 Julai, Ukumbi Na. 231, Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala.

Nimepata Waraka rasmi hapa, kwa sababu Mheshimiwa Profesa Kapuya huwa hapendi sana kukaa hapo; Waziri Mkuu, ameniandikia anasema kuwa, anatarajia kusafiri kwenda Dar es Salaam Jumamosi kwa shughuli za kikazi na kurejea Dodoma tarehe 7 Julai, wakati nitakapokuwa sipo, Mheshimiwa Profesa Kapuya, Waziri wa Kazi, atakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni hadi hapo nitakaporejea. Loh! Kwa kweli ndugu yangu huyu ameukata, siku tatu, hii ni jaha jamani. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nina udhuru kidogo, kwa hiyo, nitamwomba Naibu Spika aje aendeleze shughuli zilizoko Mezani.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na baada ya kuzingatia Taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu, kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Namshukuru sana, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kunituea kwanza kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundini na kisha Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, nafasi ambazo zimeniwezesha kushiriki katika mafanikio ya Elimu na pia katika kuendeleza usawa wa kijinsia, maendeleo ya wanawake, ustawi na maendeleo ya watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza kwa Dhabi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 katika miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Nne. Namshukuru sana, kwa kuenzi usawa wa kijinsia, ambao ni muhimu katika maendeleo, hasa kwa kuwateua wanawake kushiriki katika ngazi mbalimbali za maamuzi za kisiasa na kiutendaji.

Vilevile, nampongeza sana kwa uamuzi wake wa kutunga Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na hata kuwapa fursa ya kuongea nao Ikulu tarehe 14 Juni, 2010. Namtakia kila la heri, ashinde kwa kishindo katika uchaguzi ujao ili aweze kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na hatimaye maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa juhudini zake kubwa za kuimarisha Muungano na kuhamasisha utekelezaji wa Sera mbalimbali za nchi yetu. Mafanikio katika utekelezaji wa Sera hizo, yameiwezesha nchi kupiga hatua kubwa ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutupa maelekezo ambayo yametusaidia sana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu kwa ufanisi. Aidha, nampongeza kwa hotuba yake ya bajeti, ambayo imekuwa dira ya mjadala wetu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza kwa umahiri wako katika kusimamia na kuratibu shughuli za Bunge kwa ufanisi. Aidha, nampongeza pia Mheshimiwa Spika, wewe binafsi Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti, kwa kukusaidia kuliongoza Bunge vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa Dhabi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba yake iliyofafanua Mwelekeo wa Uchumi wa Nchi yetu na Bajeti ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ikiongozwa na Mwenyekiti wake mahiri, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kwa kuchambua na kujadili Bajeti ya Wizara yangu.

Ushauri na maelekezo ya Kamati hiyo, yameiwezesha Wizara kuandaa bajeti yake katika muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Janet Zebedayo Mbene (CCM) na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu (CUF), kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Wabunge. Aidha, ninapongeza Mheshimiwa Frederick Mwita Werema, kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Uteuzi wao unaonesha ni jinsi gani Mheshimiwa Rais anavyothamini michango yao katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote katika Bunge lako Tufuku, kwa kutekeleza vizuri majukumu yao katika kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Nne. Nawatakia kila la kheri warejee tena katika Bunge lijalo ili wakamilishe masuala yote ya maendeleo waliyokwisha kuyaanzisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko, natoa salamu za rambirambi kwa Familia ya Marehemu Sigfrid Selement Ng'itu, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ruangwa. Mchangano wake katika Bunge lako Tukufu, utakumbukwa daima. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kipindi cha Desemba 2005 hadi Juni 2010:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza nafasi na fursa kwa wanawake: Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na nafasi za maamuzi. Mheshimiwa Rais, amefanya uteuzi wa wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa na kiutendaji.

Natumia fursa hii, kwa niaba ya Wizara, kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa jitihada hizo za kuongeza wanawake katika ngazi za juu za uongozi.

Hii inaonesha kwamba, Mheshimiwa Rais anajali na kuthamini maendeleo ya wanawake. Aidha, Wizara yangu imeandaa rasimu ya Mkakati wa Kuwezesha Tanzania Kuongeza Ushiriki wa Wanawake katika Ngazi Mbalimbali za Uongozi wa Kisiasa, Kiutendaji na Nafasi za Maamuzi. Rasimu hiyo inaboreshwu kwa kuzingatia maoni ya wadau mbalimbali kabla ya kuwasilishwa ngazi za juu kwa maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekuwa ikitibitwa na kufuatilia utendaji wa Madawati ya Jinsia ya Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala mbalimbali wa Serikali, Mikoa na Halmashauri. Hali halisi inaonesha kuwa, Madawati hayo yamekuwa yakitekeleza majukumu yake kwa kutoa elimu ya jinsia kwa Wakuu wa Idara na Vitengo na Wafanyakazi wengine wa Taasisi husika ili kuongeza uelewa wao katika uingizaji wa masuala ya jinsia katika bajeti, mipango, sera na mikakati ya sekta zao.

Madawati hayo yameshirikishwa pia katika mapitio ya sera, mikakati na programu za sekta husika na kufanikiwa kuingiza masuala ya jinsia katika nyaraka hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Mikopo ya wanawake: Wizara yangu kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*WDF*), imeendelea kutoa mikopo kwa wanawake kupitia Halmashauri mbalimbali.

Kati ya mwaka 2005/2006 hadi 2009/2010, jumla ya Halmashauri 118 zimepatiwa kiasi cha shilingi 928,800,000. Aidha, Maafisa Maendeleo ya Jamii 265 kutoka ngazi ya Kata, Halmashauri na Moka, walipatiwa mafunzo kuhusu kuhamasisha wanawake kujiunga na SACCOS na vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali kwa kuzingatia Sheria ya Ushirika ya Mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake Tanzania (*TWB*) ilianza kutoa huduma za kibenki tarehe 28 Julai, 2009 na kuzinduliwa rasmi tarehe 4 Septemba, 2009 na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hadi kufikia tarehe 26 Juni, 2010, jumla ya akaunti zilizofunguliwa ziliwa 14,684 ambapo akaunti 10,088 sawa na asilimia 68.7 ni za wanawake, akaunti 4,324 sawa na asilimia 29.4 ni za wanaume na akaunti 272 sawa na asilimia 1.9 ni za makampuni. Aidha, hisa 2,993,168 zenye thamani ya shilingi 2,993,168,000.00 ziliwa zimenunuliwa.

Vile vile, benki imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wateja wake kabla ya kuwapatia mikopo. Jumla ya wajasiriamali 3,560 wakiwemo wanawake 3,524 na wanaume 36 wamepatiwa mikopo baada ya kupatiwa mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Mtoto, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria ilikamilisha uandaaji wa Sheria ya Mtoto 2009. Sheria hiyo ilipitishwa na Bunge lako Tukufu tarehe 4 Novemba, 2009 na kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba 2009. Sheria hiyo ilianza kutumika rasmi tarehe 1 Aprili 2010 na lengo ni kuhakikisha kuwa haki za mtoto za kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kushirikishwa na kutobaguliwa zinapatikana kwa watoto wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru Baraza la Watoto na wadau kwa kuipongeza Serikali na Bunge tarehe 17 April, 2010 Mjini Dodoma kwa kutunga na kupidisha Sheria ya mtoto. Halikadhalika, Wizara yangu iliratibu na kuimarisha Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mpaka sasa kuna mabaraza ya watoto ya wilaya 87. Mafanikio mengine ni pamoja na kudurusu Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 1996 ili kuelekeza namna ya kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika upatikanaji wa haki za mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2005/2006 – 2009/2010, Wizara ilihudhuria mikutano minne ya Kimataifa inayohusu Maendeleo na Ustawi wa Mtoto. Mikutano hiyo ilifanyika Accra – Ghana mwaka 2005, Geneva – Uswisi Novemba 2008, Addis Ababa – Ethiopia Novemba 2009 na Dakar – Senegal Novemba 2009. Katika mikutano hiyo Tanzania iliwasilisha na kutetea taarifa za utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Haki na Ustawi wa Mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utumikishwaji wa watoto. Wizara imeendelea kuhamasisha, kuhimiza na kuelimisha familia na jamii kwa ujumla kuhusu haki za mtoto hususan kuzuia utumikishwaji wa watoto katika kazi za hatari zinazoathiri afya zao. Wizara kupitia vyombo vya habari, mabango na maadhisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika 16 Juni, Siku ya Familia Duniani 15 Mei pamoja na Siku ya Kupambana na Ajira Mbaya kwa Watoto Duniani 12 Juni imekuwa ikisisitiza kuacha uvunjaji wa Haki za Watoto ikiwemo utumikishwaji. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 36 na kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii 120 katika mikoa 18 ya Tanzania Bara kuhusu haki za mtoto za uhai, ulinzi, kuendelezwa, kushirikishwa na kutobaguliwa. Washiriki wa mafunzo hayo wanaelimisha jamii kuhusu haki za mtoto katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupunguza vifo vya watoto wachanga. Wizara yangu imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa inayohusu haki na ustawi wa mtoto. Hii ni pamoja na kuwezesha kufanyika kwa mkutano wa nchi za Kusini na Mashariki mwa Afrika kuhusu malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto uliofanyika Arusha mwezi Februari 2008. Aidha, Wizara imeandaa

rasimu ya Sera ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ambayo hivi sasa imewasilishwa kwenye ngazi za juu za maamuzi. Rasimu hiyo inasisitiza wazazi/walezi, jamii na wadau kuwapatia watoto wadogo huduma muhimu kama vile lishe bora, chanjo na tiba ambazo pamoja na mambo mengine zitasaidia kuzuia vifo vya watoto wachanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutokomeza mila zenyenye kuleta madhara, Wizara ilianzisha kampeni ya Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake iliyozinduliwa mwaka 2008 na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile iliwezesha Kamati ya Kitaifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto kuundwa ili kuratibu utekelezaji wa kampeni ya kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake, watoto, vikongwe na albino.

Mafanikio mengine ni pamoja na Wizara kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa sheria 190, wakiwemo Polisi 80, Askari Magereza 80 na Mahakimu wa Wilaya 30 yanayohusu kuzuia na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake. Aidha, Wizara yangu iliandaa mkutano wa Kamati ya Sekretariati ya Kutokomeza Ukeketaji Kanda ya Afrika Mashariki Tawi la Tanzania. Vilevile, Wizara imeandaa Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Familia ambayo inatoa mwelekeo wa kukabiliana na mila zenyenye kuleta madhara katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu na mafunzo. Wizara ina Vyuo 53 vya Maendeleo ya Wananchi ambavyo vimeenea mikoa yote Tanzania Bara. Vyuo hivyo huwapatia wananchi stadi mbalimbali za maisha zinazowawezesha kujajiri na kuajiriwa hivyo kuchangia katika vita dhidi ya umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano, Wizara yangu kuitia vyuo vya Maendeleo ya Wananchi imetoa mafunzo ya stadi na maarifa mbalimbali kwa wananchi 145,037 wakiwemo wanawake 67,667 na wanaume 77,370 ili kuinua viwango vya uzalishaji kwenye kazi zao (Jedwali Na. 3). Aidha, ukarabati na ujenzi wa majengo na miundombinu umeendelea kufanyika katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 33 (Jedwali Na. 4). Ukarabati umeboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia hivyo kuvutia wananchi wengi kuijunga na vyuo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya Elimu ya Juu. Wizara ina vyuo tisa ambavyo hutoa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi za cheti, Stashahada na Shahada. Wahitimu katika vyuo hivyo huajiriwa na Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kupewa majukumu ya kuhamasisha jamii katika kubaini matatizo yao na kubuni mbinu na mikakati itakayowawezesha kuyatatua ili kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukidhi mahitaji ya wataalam wa maendeleo ya jamii ngazi za kata na kijiji, vyuo nane vya maendeleo ya jamii viliendelea kutoa mafunzo ya ngazi ya cheti na stashahada. Jumla ya wanafunzi 2,196 ikiwa ni wanawake 1,519 na wanaume 677 walidahiliwa katika mafunzo ya Cheti cha Msingi cha Maendeleo ya Jamii. Aidha jumla ya wanafunzi 765 ikiwa ni wanawake 513 na wanaume 252

walidahiliwa katika mafunzo ya stashahada ya Maendeleo ya Jamii (Jedwali Na 5). Wataalam hao huajiriwa katika ngazi za kata na kijiji hivyo wana umuhimu wa pekee katika kuleta chachu ya maendeleo katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kimekuwa kikitoa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya stashahada ya juu. Kuanzia mwaka 2009/2010 udahili wa stashahada ya juu ulisitishwa na badala yake ukaanzishwa udahili wa ngazi ya shahada. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita chuo kimefanikiwa kudahili jumla ya wanafunzi 1,436 ikiwa ni wanawake 818 na wanaume 618 kwa mafunzo ya Stashada ya Juu na Shahada ya kwanza ya Maendeleo ya Jamii (Jedwali Na. 6). Wahitimu katika chuo hiki ni muhimu katika kuhamasisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mazingira ya kusomea na kujifunzia vyuoni, Wizara yangu imejenga majengo mawili ya miadhara (*Lecture Theatres*) katika Chuo Cha Maendeleo ya Jamii cha Tengeru na inaendelea kujenga maktaba ya kisasa katika chuo hicho. Aidha, kazi ya kupitia upya mitaala ya ufundi kwa ngazi ya Stashahada na cheti kwa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Ufundi vya Missungwi na Mabughai ilifanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeyapatia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) 3,923 hati za kutambulika kisheria (Jedwali Na.7). Miongoni mwa Mashirika haya, 3,198 yamepatiwa vyeti vya usajili na 725 vyeti vya Ukubalifu. Aidha, Usajili wa Mashirika haya unayawezesha kuendesha shughuli zao kihalali katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa. Vilevile, Wizara yangu itaendelea kuyawezesha Mashirika mengi zaidi kujisajili na kupata uhalali wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa taarifa sahihi za sekta ya *NGOs* nchini ni nyenzo muhimu ya kuimarishe uwazi, uwajibikaji na ubadilishanaji wa habari miongoni mwa wadau wa sekta hii. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006 hadi 2009/2010, Wizara imeanzisha Tovuti (<http://www.tnnc.go.tz.>) na Benki ya takwimu na taarifa za uratibu wa *NGOs*. Tovuti hiyo ilizinduliwa rasmi mwezi Julai, 2009 na Mheshimiwa Margaret S. Sitta Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Aidha, Wizara imeendelea kuingiza na kuhifadhi taarifa za *NGOs* kwenye Benki na Tovuti hiyo ili kusogeza baadhi ya huduma za usajili na uratibu wa Mashirika haya karibu na wananchi hususan sekta binafsi, wafadhili, *NGOs* zenyewe na Idara za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuimarishe mfumo wa mawasiliano. Wizara yangu imeimarisha kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kukipatia vitendea kazi katika kusimamia shughuli za Wizara. Aidha, miundombinu ya mawasiliano katika jengo jipya imeimarishwa. Vilevile, kitengo kimekamilisha utengenezaji wa tovuti ya idara ya *NGOs* na Benki ya takwimu ambayo taarifa na maelezo muhimu kwa ajili ya usajili na uratibu wa *NGOs* vinapatikana. Halikadhalika, Wizara yangu imeimarisha Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ya Umma kwa kukipatia vitendea kazi kama vile Kompyuta, Printa, Kamera na Vinasa Sauti. Watumishi

wawili wamepatiwa mafunzo ya mawasiliano ya uandaaji wa vipindi vyta redio na televisheni. Watumishi hao wamefanikiwa kuandaa vipindi mbalimbali vyta televisheni na redio vinavyohusu Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imetoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi ili kuwaongezea uelewa na kuwapa stadi na maarifa ya kutekeleza majukumu yao. Wizara imepeleka jumla ya watumishi 756 kwenye mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi kama inavyofafanuliwa katika (Jedwali Na. 8).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2005/2006 – 2009/2010, Wizara yangu imeendelea kutoa elimu ya hifadhi ya mazingira kwa wananchi kupitia katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Aidha, vyuo hivi vimepanda jumla ya miti 44,502 katika maeneo yanayozunguka Vyuo ili iwe ni mfano na hamasa katika jamii zinazozunguka vyuo hivyo. Vilevile, kupitia vyuo hivyo jamii zinazovizunguka zimehamasishwa kuhusu matumizi bora na endelevu ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupunguza maambukizi mapya ya UKIMWI. Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo kwa wananchi wanaojiunga na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kuongeza uelewa wao katika masuala ya UKIMWI. Jumla ya wananchi 145,037 wakiwemo wanawake 67,667 na wanaume 77,370 wamepata mafunzo hayo. Aidha, elimu ya masuala ya UKIMWI mahali pa kazi imetolewa kwa watumishi 200 wa makao makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali halisi ya sekta ya maendeleo ya jamii na changamoto zilizopo. Dhana ya maendeleo ya jamii inamaanisha hatua ya maendeleo ya watu iliyofikiwa kama itakavyojidhihirisha kupitia vigezo mbalimbali na pia jinsi watu walivyoshiriki katika kufikia maendeleo hayo. Inasisitiza umuhimu wa kujilettea maendeleo kwa njia ya kujitegemea. Kwa mantiki hiyo sekta ya maendeleo ya jamii ni mtambuka na hivyo utekelezaji wa majukumu ya sekta unahusisha sekta nyingine nyingi. Hivi sasa utekelezaji wa programu za kuondoa umaskini katika sekta mbalimbali unazingatia ushiriki na michango ya hali na mali kutoka kwa watu. Wananchi wamekuwa wakijitolea kushiriki katika upanuzi wa huduma za kijamii na kiuchumi ikiwemo ujenzi wa shule za msingi na sekondari, ujenzi wa zahanati na vituo vyta afya, na ujenzi wa barabara vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli huo, kazi kubwa ya Wizara na Sekta ya Maendeleo ya Jamii ni kuwezesha ushiriki wa watu katika upangaji na utekelezaji wa shughuli zinazohusu maendeleo yao katika sekta mbalimbali kupitia utoaji wa sera, kuweka mikakati na kuandaa wataalam wa maendeleo ya jamii. Kwa mantiki hiyo Wizara imeandaa Sera ya Maendeleo ya Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Jinsia, Maendeleo ya Mtoto, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na rasimu ya Sera ya Familia. Aidha, Wizara inasimamia Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 na Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2002. Hali kadhalika, Wizara inasimamia Vyuo 62: tisa

(9) vikiwa vya kufundisha wataalam wa maendeleo ya jamii na 53 vya kutoa mafunzo ya maarifa na stadi kwa wananchi, kulingana na mahitaji yao ya kuwawezesha kujajiri au kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuitia Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia, Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi kuthamini na kuenzi usawa wa jinsia kama sehemu ya utekelezaji wa haki za binadamu. Hali kadhalika, Wizara inawezesha uendeshaji wa kampeni mbalimbali dhidi ya mila na imani zilizopitwa na wakati na kandamizi kwa wanawake na baadhi ya makundi kama vile watu wenye ulemavu wa ngozi, vikongwe na watoto. Kwa kutambua mchango unaotolewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara inaendelea kurahisisha usajili na uratibu wa Mashirika hayo na kutoa ushauri pale unapohitajika. Aidha, Wizara imeanzisha tovuti ambayo inawawezesha wananchi kutoa maoni yao kuhusiana na utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya umuhimu wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii katika kufanikisha vita dhidi ya umaskini, kukuza uchumi, kudumisha utawala bora na haki sawa kwa binadamu wote; wanawake, wanaume, watoto na watu wenye ulemavu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambayo ni muhimili wa sekta hiyo imeendelea kuwa na ufinyu wa bajeti na nyenzo za kufanyia kazi. Aidha, kuna upungufu mkubwa wa wataalam wa maendeleo ya jamii ambao ndio kichocheo cha maendeleo katika ngazi ya kata. Hivi sasa ni asilimia 40 tu ya Kata zote nchini zenyne wataalam hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa mpango wa mwaka 2009/2010 na malengo ya mwaka 2010/2011; katika mwaka 2009/2010 Wizara kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali iliendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa mafanikio makubwa. Aidha, katika mwaka 2010/2011 maeneo matano yafuatayo yamepewa kipaumbele:-

(i) Kuimarisha vyuo vya maendeleo ya wananchi na vyuo vya maendeleo ya jamii kwa kuvifanyia ukarabati wa miundombinu (madarasa, mabwalo ya chakula, mabweni, ofisi na nyumba za watumishi) na kuhakikisha vyuo vinapatiwa chakula, vyombo vya usafiri na vifaa vya kufundishia.

(ii) Kutekeleza Mikataba ya Kikanda na Kimataifa; Itifaki za usawa wa kijinsia; Maendeleo ya Wanawake, Haki na Ustawi wa watoto.

(iii) Kujenga uwezo wa Wizara katika ufuutiliaji na tathmini za shughuli za Wizara.

(iv) Kuhamasisha jamii juu ya masuala ya jinsia ikiwemo uzingatiwaji wa masuala ya jinsia katika mipango, mikakati na bajeti; kupinga ukatili wa kijinsia, ukatili dhidi ya watoto na kuwapunguzia wanawake mzigo wa kazi.

(v) Kuendelea kuimarisha Benki ya Wanawake Tanzania.

(vi) Maeneo haya kwa pamoja yametengewa asilimia 74.5 ya bajeti yote ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2009/2010 na malengo ya mwaka 2010/2011 ni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo ya jamii. Katika mwaka 2009/2010 Wizara yangu kupitia vyuo vya Maendeleo ya Wananchi iliwapatia wananchi 31,039 mafunzo ya ujuzi na stadi mbalimbali za maisha wakiwemo wanaume 16,044 na wanawake 14,995. Jumla ya shilingi 586,390,000 zilitumika kutoa mafunzo hayo. Katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu inatarajia kuendelea kudahili na kutoa mafunzo kwa wananchi 31,000 ndani na nje ya vyuo. Jumla ya shilingi 605,760,000 zinatarajija kutumika katika utoaji wa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kukamilisha kazi ya ukarabati katika vyuo 21 vya Maendeleo ya Wananchi (Jedwali Na.9). Vyuo hivi vilianza kufanyiwa ukarabati katika kipindi cha 2008/2009, lakini ukarabati wake haukukamilika kutohakana na fedha zake kutopatikana. Jumla ya shilingi 1,200,585,808/= zimetumika katika ukarabati huo. Ukarabati mkubwa na mdogo na ununuizi wa samani utaendelea kufanyika katika mwaka 2010/2011 katika Vyuo 22 vya Maendeleo ya Wananchi. Aidha vyuo 3 vitanunuliwa magari kwa ajili ya kurahisisha usafiri katika programu ya mafunzo nje ya vyuo na matumizi mengineyo. Jumla ya shs.3,409,200,000/= zimetengwa kwa ajili ya shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2009/2010, Wizara yangu ilifanya tafiti mbili (2) katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 53 na vyuo vitatu (3) vya Maendeleo ya Jamii ili kubaini taathira ya mafunzo ya Elimu ya Wananchi kwa Walengwa na kuangalia uwezekano wa Vyuo hivyo kutoa mafunzo ya elimu ya wananchi sanjari na mafunzo ya ufundi stadi. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kwamba vyuo hivi vinaweza kutoa mafunzo ya aina zote mbili kwa sababu hadi sasa mafunzo ya ufundi stadi yanatolewa. Aidha, utafiti umeonesha kuwa asilimia 80 ya wanachuo hufaulu pindi wanapofanya mitihani ya ufundi stadi. Tafiti hizo ziligharimu shilingi 268,000,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wa maendeleo ya jamii ni muhimu katika kuhamasisha na kuelimisha wananchi ili kushiriki katika mchakato wa kujiletea maendeleo. Katika jitihada za kuongeza wataalamu hao, Wizara katika mwaka 2009/2010 ilidahili na kutoa mafunzo kwa wanachuo 1,337 katika vyuo 9 vya Maendeleo ya Jamii vya Tengeru, Rungemba, Buhare, Monduli, Missungwi, Ruaha, Uyole, Mlale, na Mabughai. Idadi ya wanachuo katika ngazi ya cheti walikuwa 775, Stashahada 425, na Shahada 137. Jumla ya shilingi 527,204,000 zilitumika kugharamia mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili viweze kutoa wataalamu wengi zaidi. Aidha, Wizara yangu inatarajia kudahili na kutoa mafunzo kwa Wanachuo 1,910 katika ngazi ya Cheti, Stashahada, na Shahada. Vilevile vyuo 2 vitanunuliwa magari ili kuvipunguzia tatizo la usafiri. Jumla ya shilingi 485,301,391 zimetengwa kwa ajili ya shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekamilisha usajili wa vyuo 2 vya Maendeleo ya Jamii vya Tengeru na Rungemba na inaendelea na taratibu za usajili wa Vyuo 7 vya Maendeleo ya Jamii (*Registration and Accreditation*) katika Baraza la Elimu ya Juu (*NACTE*) kama inavyooneshwa katika (Jedwali Na. 10).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upanuzi wa mafunzo vyuoni, Chuo cha maendeleo ya Jamii Tengeru kimeanza kutoa mafunzo ya muda mfupi yanayochukua muda wa wiki moja mpaka wiki sita yanayotolewa ndani na nje ya chuo. Mafunzo haya yanahusu Misingi ya Maendeleo ya Jamii, mipango shirikishi, ubunifu na uandishi wa miradi, mbinu za uongozi na utawala, mbinu za kuendesha biashara, uchambuzi na upangaji wa masoko. Aidha, chuo hiki kimeanza kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo husika. Vile vile, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Rungemba, Ruaha na Uyole vimeanza kutoa mafunzo ya jioni ya stashahada ya Maendeleo ya Jamii na Cheti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza tija na kuwapunguzia mzigو wa kazi wananchi hususan wanawake, katika kipindi cha 2009/2010 Wizara yangu imetumia kiasi cha shilingi 153,000,000/= kwa ajili ya kununua matrekti 18 ya kusukuma kwa mikono na yatakuwa yamesambazwa ifikapo mwezi Agosti, 2010 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili walengwa wapate fursa ya kuyatumia katika uzalishaji wa mazao ya kilimo. Vyuo viliviyotakiwa kupata matrekti hayo ni Muhukuru, Msaginya, Chala, Kihinga, Kibondo, Kasulu, Nandembo, Chisalu, Tarime, Sofi, Ilula, Mbanga, Kilosa, Urambo, Missungwi, Mabughai, Ruaha na Monduli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha utendaji kazi katika sekta ya maendeleo ya jamii, katika kipindi cha 2009/2010 Wizara yangu iliendesa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii. Mkutano ulijumuisha washiriki 320 kutoka katika Halmashauri zote nchini, Sekretarieti za Mikoa, Sekta nyine na Zanzibar. Wajumbe walijadili na kupidisha maazimio mbalimbali yaliyolenga kuboresha utendaji na kuleta ufanisi zaidi katika mazingira yetu ya kazi. Jumla ya shilingi 223,250,500 zilitumika katika uendeshaji wa mkutano huo. Wizara yangu katika mwaka 2010/2011 itaendelea kuendesa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii ambao umekuwa muhimu katika kujadili na kupima mafanikio na changamoto za sekta hii. Zaidi ya washiriki 320 wanategemewa kuhudhuria na jumla ya shilingi 216,250,000 zimetengwa kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maendeleo ya Jinsia. Katika kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara yangu inaendelea kuratibu na kusimamia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake (*WDF*) kwa kushirikiana na Halmashauri. Katika kipindi cha 2009/2010 Wizara imeendelea kupeleka fedha kwenye Halmashauri kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ili kuwakopesha wanawake wajasiriamali kwenye maeneo yao. Jumla ya Shs. 220,000,000/= zimepelekwa kwenye Halmashauri 30 zilizokamilisha marejesho ya mikopo. Wizara kwa kipindi cha 2010/2011 itaendelea kuratibu na kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kupitia Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mfuko wa Fursa Sawa kwa wote (*EOTF*) iliwezesha mafunzo ya biashara na ujasiriamali kwa wanawake 350 kwa kuchangia Shilingi 13,150,000/=. Wanawake hao walitokea mikoa mbalimbali Tanzania Bara, ambao baada ya mafunzo hayo walishiriki maonesho ya 34 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam. Kwa mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendeleza mafunzo, kusimamia na kuratibu shughuli za wanawake Wajasiriamali watakaoshiriki maonesho ya biashara Kimataifa ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Benki ya Wanawake Tanzania ilianzishwa na inaendelea kutoa huduma za kibenki kwa wananchi ikiwa pamoja na mikopo. Hadi kufikia tarehe 26 Juni, 2010 jumla ya vikundi 89 (Jedwali Na. 11) vilipatiwa mafunzo na kupata mikopo yenyе thamani ya shilingi 1,100,000,000/=. Aidha, Benki imeweza kutoa jumla ya mikopo yenyе thamani ya shilingi 3,892,665,860/= kwa wateja mbalimbali ikiwa ni pamoja na vikundi vya wajasiriamali. Katika kipindi cha 2010/2011, Wizara itahamasisha jamii na taasisi mbalimbali kununua hisa za Benki ya Wanawake ili kuiimarisha. Aidha, katika kuendelea kuimarisha Benki hii katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 2.0.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwajengea mazingira mazuri ya biashara wanawake wajasiriamali Wizara katika kipindi cha 2010/2011, itahamasisha uanzishwaji wa vituo vitano vya biashara vya wanawake katika mikoa mitano. Lengo la kuanzisha vituo hivyo ni kuongeza fursa kwa wanawake wajasiriamali kupata masoko ya bidhaa wanazozalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kuimarisha uratibu, uchambuzi unaozingatia masuala ya jinsia katika mipango, programu na bajeti ya sekta mbalimbali. Jumla ya shilingi 62,315,000.00 zilitumika kutoa mafunzo kwa washiriki 127 kutoka makundi yafuatayo: Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na Makatibu wa Kamati nyingine za Bunge 47, Wakuu wa Vituo vya Polisi wa Kanda ya Ziwa inayojumuisha mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara 40 na viongozi wa ngazi mbalimbali za vijiji kutoka Kanda ya Ziwa inayojumuisha mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara 40. Wizara yangu katika kipindi cha 2010/2011 itaendelea kutoa mafunzo ya uchambuzi na uingizaji wa masuala ya jinsia katika bajeti kwa watendaji wa dawati la jinsia na wataalamu wengine katika Wizara na Idara za Serikali. Vile vile, mafunzo ya uchambuzi na uingizwaji wa masuala ya jinsia katika bajeti yataendelea kutolewa kwa Kikundi cha Jinsia cha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majukumu mengine Wizara yangu inajukumu la kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi ikiwa ni pamoja na kugombea nafasi mbalimbali za kisiasa. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kuhamasisha wanawake kuhusu umuhimu wa kujitokeza kugombea na kupiga kura katika chaguzi mbalimbali ili kufikia uwakilishi wa uwiano wa asilimia 50

kwa 50 katika nafasi za kiutendaji na kisiasa. Jumla ya washiriki 851 wakiwemo wanaume 58 wamenufaika na elimu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika Lisilo la Kiserikali la *Friedrich Ebert Stiftung (FES)* liliendesa semina kwa wanawake 52 kuhusu uongozi, stadi za uongozi na mbinu za kuthibiti na kusuluuhisha migogoro kwenye jamii. Kati ya wanawake hao, 24 walipata nafasi za uongozi ngazi ya kitongoji na Wenyekiti wa Kijiji. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara itaendelea kuwashamasisha wanawake na jamii kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika mwezi Oktoba, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudhi za kutokomeza ukatili wa kijinsia, Wizara katika kipindi cha mwaka 2009/2010 iliandaa sinema inayooonesha matendo ya ukatili dhidi ya Wanawake, Watoto na Albino. Sinema hiyo ilioneshwa katika vijiji mbalimbali vya Mikoa ya Kanda ya Ziwa ili kuwashamasisha wananchi kupinga ukatili wa kijinsia. Katika kipindi cha 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, watoto na Albino kupitia Kampeni ya Kataa Ukatili dhidi ya Wanawake, Watoto na Albino.

Mheshimiwa Naibu Spika, maadhisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa mwaka huu yalifanyika katika ngazi ya Kitaifa kuanzia tarehe 3-8 Machi, 2010, Mkoani Tabora. Maadhisho hayo yalizinduliwa na Mheshimiwa Ali Juma Shamhuna, Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, Viongozi mbalimbali kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar walishiriki wakiwemo Mheshimiwa Machano Othmani kutoka Ofisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Asha A. Bakari; Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto na Mheshimiwa Samia Washoto; Mwenyekiti wa UWT wa Mjini Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgeni Rasmi katika kilele cha maadhisho ya Siku ya Wanawake Duniani terehe 8 Machi, 2010 alikuwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maadhisho hayo yalihudhuriwa pia na Wageni waalikwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Samwel Sitta, Spika Wa Bunge la Tanzania, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (*UNFPA*), Bibi Julitha Onabanjo, ambaye alisoma salamu za Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mwakilishi Mkazi wa Umoja Wa Ulaya (EU), Bwana Tim Clarke, baadhi ya Makatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu. Jumla ya Wageni waalikwa zaidi ya 100 walihudhuria maadhisho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kaulimbiu ya maadhisho hayo ilikuwa ni “Miaka 15 baada ya Beijing: Wanawake wanaweza, wapewe nafasi.”

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maadhimisho hayo kulifanyika pia makongamano ya kujadili mafanikio, changamoto zilizojitokeza na mikakati ya kukabiliiana na changamoto hizo, kwa wakazi wa Mkoa wa Tabora na Waandishi wa Habari; Sherehe hizi zilifana sana kutokana na ushirikiano mzuri tulioupata kutoka kwa uongozi na wananchi wa Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika mwaka 2010/2011, itaendelea kuhamasisha jamii kupitia vyombo vya habari ili kujenga uelewa kuhusu dhana ya ushiriki sawa baina ya wanawake na wanaume katika ngazi za maamuzi, uongozi na utendaji. Wizara itatoa mafunzo kwa wanawake watakao chaguliwa katika ngazi za Ubunge na Udiwani ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo ya mtoto. Katika mwaka wa 2009/2010, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria iliahidi kuandaa Sheria ya Mtoto 2009. Nafurahi kiliarifu Bunge lako tukufu kwamba Sheria hiyo imekamilika na ilipitishwa na Bunge lako tukufu. Aidha, kupitishwa kwa sheria hii kuliungwa mkono na watoto kwa kufanya maandamano yaliyofanyika mjini Dodoma tarehe 14 Aprili, 2010 na kupokelewa na Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda. Katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na wadau itatafsiri sheria ya Mtoto, kuandaa kanuni, kuchapisha na kusambaza sheria hiyo kwa wananchi ili waielewe na kuizingatia katika utoaji wa haki za mtoto. Katika mwaka 2010/2011, Wizara imetenga jumla ya shilingi 37,000,000/= kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika mwaka wa fedha 2009/2010 imeandaa rasimu ya Sera ya Jumui ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto Tanzania ambayo hivi sasa inawasilishwa kwenye ngazi za juu za maamuzi. Rasimu ya Sera hiyo inasisitiza wazazi/walezi, jamii na wadau kuwapatia watoto wadogo huduma muhimu kama vile lishe bora, chanjo, tiba na uchangamshi wa awali ambazo zitasaidia kupatikana kwa maendeleo na ustawi wa mtoto. Katika mwaka 2010/2011, Wizara inatarajia kutumia jumla ya shilingi 260,000,000/= kwa ajili ya kuchapisha, kutoa elimu kwa wadau, kusambazwa na kuitengenezea mkakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha fedha cha mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kuhamasisha jamii kuhusu tatizo la watoto wanaoishi mitaani ili iweze kuwahudumia kwa kuwapatia elimu, chakula, mavazi na ulinzi, na kila inapowezekana waweze kurejeshwa katika familia. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya Mpango Mkakati wa Jamii wa Kudhibiti Tatizo la watoto hao. Mpango huo umelenga kudhibiti tatizo la watoto hao kwa kuhusisha jamii, taasisi zisizo za kiserikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, vyombo vya habari na wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika, Wizara yangu inasambaza Kitini cha Jamii kuhusu Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Dodoma na Singida. Katika mwaka wa 2010/2011, Wizara itaendelea kutoa mafunzo na kusambaza kitini hicho kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika mikoa mingine. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Jamii wa Kudhibiti Watoto Wanaoishi Mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kuratibu vikao vya Sekretarieti ya Kutokomeza Ukeketaji Tanzania. Kupitia vikao hivyo, kimeundwa kikosi kazi cha maandalizi ya kutathmini utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukeketaji na Mila nyingine zenyenye kuleta madhara nchini. Katika mwaka wa 2010/2011, Wizara itaendelea kuratibu vikao vya Sekretarieti pamoja na kutekeleza na kutathmini Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukeketaji na mila nyingine zenyenye kuleta madhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ina jukumu la kuratibu uandaaji wa taarifa ya nchi kuhusu utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda ya haki na ustawi wa mtoto. Mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliratibu ushiriki wa serikali katika kutetea Taarifa ya Awali ya Utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto katika kikao cha 14 cha Kamati ya Afrika ya Wataalam kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto kilichofanyika Addis Ababa, Ethiopia mwezi Novemba, 2009. Aidha, Wizara yangu ilishiriki katika mkutano wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto uliofanyika Dakar Senegal. Mkutano huo ulizungumzia jinsi ya kusambaza na kuboresha utoaji wa huduma za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto barani Afrika. Mkutano huo uliazimia kwamba utoaji wa huduma hizo uzingatie uwezo wa kiuchumi na rasilimali zilizopo katika nchi za Afrika. Katika kipindi cha 2010/2011, Wizara itaendelea na uratibu wa utekelezaji wa mikataba yote ya haki na ustawi wa mtoto na kuitolea taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara iliendelea kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo yalifanyika kimko na Kaulimbiu yake ilikuwa ni “Imarisha Familia: Mtoto Apate Haki Zake”. Vilevile, Maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani yalifanyika kimko na kaulimbiu ilikuwa ni “Elimu: Msingi wa Maisha Bora ya Familia”. Katika mwaka 2010/2011 Wizara itaendelea kuratibu maadhimisho ya siku hizo. Maadhimisho hayo ni utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa na ya Kikanda kuhusu haki na ustawi wa mtoto na maendeleo ya familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha fedha cha mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliahidi kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba rasimu ya Mkakati huo imeandalishi na hivi sasa inapata maoni mbalimbali ya wadau ili ikamilishwe. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara itawezesha rasimu hiyo kupitishwa katika vyombo vya maamuzi na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekuwa ikiongeza fursa ya ushiriki wa wananchi katika maendeleo kupitia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kufuatia uboreshaji wa zoezi la usajili wa Mashirika hayo chini ya Sheria ya NGOs Na. 24 ya mwaka 2002. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Mashirika 649 yalipata hati za kutambulika kisheria ambapo 600 kati ya hayo yalipata Usajili na 49 Cheti cha Ukubalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara yangu imeendelea kuratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya *NGOs* ya mwaka 2001 na Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002. Jithada hizi zililenga kuongeza uwajibikaji na ushiriki wa Mashirika haya katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kuhakikisha mchango wao unafahamika kwa jamii na umma. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la *NGOs* ilizindua Kanuni za Maadili ya *NGOs* mwezi Julai, 2009 mjini Dodoma. Jumla ya nakala 7,000 za Kanuni hizi katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza zilisambazwa kwa wadau wa Sekta ya *NGOs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iliendelea kuingiza na kuboresha taarifa za *NGOs* kwenye tovuti ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambayo ni [hppt// www.tnnc.go.tz](http://www.tnnc.go.tz). Kwa kufanya hivyo tumesogeza baadhi ya huduma za usajili na uratibu karibu na wananchi, hivyo kuwapunguzia gharama. Baadhi ya huduma zinazopatikana kupitia tovuti hii ni maelezo kuhusu taratibu za usajili, fomu za usajili na uwasilishaji wa taarifa za mwaka za *NGOs*. Aidha, wadau wamekuwa wakiitumia tovuti hii katika kupata ufanuzi wa mambo mbalimbali kuhusu Sekta ya *NGOs*. Taarifa hizi pia zimekuwa zikiingizwa na kuhifadhiwa kwenye Benki ya Takwimu na taarifa ya Uratibu wa *NGOs* na hivyo kuwezesha upashanaji wa taarifa mionganoni mwa wadau wa sekta hii hususan sekta binafsi, wafadhili, *NGOs* zenyewe na Idara za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kuboresha na kuhuisha taarifa na takwimu kwenye Benki na Tovuti ya Taifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Taarifa zitakazoingizwa na kuboreshwa ni pamoja na Mashirika yaliyosajiliwa na kupata Cheti cha Ukubalifu chini ya Sheria ya *NGOs* Na. 24, ya mwaka 2002, Fomu mbalimbali zinazohusu usajili na uratibu wa *NGOs*, nakala ya Sera ya Taifa ya *NGOs* na Sheria ya *NGOs*, Kanuni za Maadili ya *NGOs* na Taarifa za vikao vya Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs*. Ni matumaini yangu kuwa wananchi wataendelea kutumia tovuti na benki hii kupata taarifa muhimu kuhusu sekta ya *NGOs* na kutupatia mrejesho wa utendaji wetu na wadau wengine wa Sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeiwezesha Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* kufanya vikao vitatu (3) vya kisheria kwa mwaka 2009/2010 katika mikoa ya Shinyanga, Iringa na Pwani kwa ajili ya kuratibu shughuli za *NGOs* nchini. Kila baada ya vikao hivyo, Bodi ilitembelea *NGOs* za mikoa husika na kukutana na wadau wa Sekta ya *NGOs*. Katika zoezi hili, Bodi ilikutana na wadau 286 na kutembelea Mashirika 36 ili kubaini changamoto zinazoikabili Sekta ya *NGOs* na kubadilishana uzoefu kuhusu matokeo bora ya shughuli za Mashirika haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu wa mikoa ambayo Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs* ilitembelea na kufanya mikutano na wadau unaonesha kujengenka kwa mahusiano ya kuaminiana mionganoni mwa wadau wa Sekta ya *NGOs*. Hivyo, katika mwaka

2010/2011 Wizara yangu itaendelea kuiwezesha Bodi hii kufanya vikao vyake katika mikoa ambayo bado haijafikiwa. Aidha, Bodi imepanga kukutana na wadau wa Sekta ya *NGOs* na kuzitembelea *NGOs* katika mikoa ambayo itafanya vikao vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ushiriki wa wananchi katika Sekta ya *NGOs* ni muhimu katika kuboresha utendaji wa Mashirika haya. Kwa kutambua umuhimu huo, wizara yangu imekuwa ikitoa weledi kwa wananchi kuhusu Sera ya Taifa ya *NGOs* ya mwaka 2001 na Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005. Tumekuwa tukifanya hivyo kuitia Ofisi ya Msajili, Maonesho ya Saba-saba, Nane-nane na Wiki ya Utumishi wa Umma ambapo jumla ya wadau 504 wamepata weledi huo. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, tutaendelea kutoa weledi huo ili kuwafikia wadau wengi zaidi na kuongeza ushiriki wao katika shughuli za *NGOs* nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sera na Mipango. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara ilifuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi katika mikoa ya Arusha, Singida, Iringa, Tabora, Kigoma, Kilimanjaro, Shinyanga na Tanga. Jumla ya Vyuo 20 vilitembelewa kuona shughuli za ukarabati wa majengo na miundombinu. Ukarabati ulikuwa unaendelea taratibu kwa kutegemea upatikanaji wa rasilimali fedha. Aidha, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo katika vyuo. Lengo ni kuhakikisha yanakuwepo matumizi mazuri ya fedha na miradi kukamilika kwa ubora na muda uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha ufanisi wa utendaji kazi, Wizara katika kipindi cha 2009/2010 iliwapatia mafunzo ya muda mfupi watumishi 21 huko Morogoro yaliyohusu ufuatiliaji na tathmini ya sera za maendeleo. Mafunzo hayo yaliwaongezea watumishi uwezo wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa sera za Wizara katika jamii. Mafunzo haya yataendelezwa mwaka 2010/2011, kwa kuhusisha watumishi wengine 25 kutoka Idara na Vitengo vyote vya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Wizara iliahidi kukamilisha uandaaji wa mpango mkakati wa kuimarisha takwimu za sekta ya Maendeleo ya Jamii. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ukamilishaji umefanyika kwa kuandaa rasimu, kuisambaza kwa wadau na kupata maoni yao. Maoni hayo kwa sasa yanazingatiwa na kujumuishwa katika rasimu ili kukamilisha mkakati. Mpango Mkakati huu utawezesha Wizara kukusanya na kuchambua takwimu za sekta ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha 2009/2010, Wizara iliendelea na utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa Kituo cha Habari na Taarifa za Wanawake. Awamu hii inahusisha utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wa Wanawake katika nyanja za mafunzo na upashanaji habari. Utekelezaji wa awamu hii utaendelea katika mwaka wa fedha 2010/2011 kwa kukusanya na kueneza taarifa zinazohusu wanawake, watoto na jamii katika ngazi ya Taifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kuptitia kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kinakamilisha tovuti ya Idara ya Maendeleo ya Jamii ambapo taarifa mbalimbali za Idara na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Maendeleo ya Wananchi zitapatikana ili kuwawezesha wadau wa sekta ya maendeleo ya jamii kupata taarifa mbalimbali. Aidha, taarifa za matokeo ya mitihani ya wanachuo zitapatikana. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaboresha tovuti ya Wizara ili iweze kuwa na Benki ya takwimu ya shughuli zote za Wizara kwa ajili ya matumizi ya wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Utawala na Utumishi. Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2009/2010 iliendelea kusimamia utendaji kazi kwa misingi ya haki, usawa, uadilifu, utawala bora na uwazi na kuweka mkazo katika kudhibiti vitendo vya rushwa, uzembe kazini pamoja na janga la UKIMWI mahala pa kazi. Masuala haya ni ya msingi katika kuiwezesha Wizara kuwa na watumishi waadilifu na wanaowajibika, wenye ari, moyo na msimamo thabiti kuhusu utumishi wa umma na walio tayari kutoa huduma bora kwa umma wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2009/2010 iliendelea kupiga vita rushwa kwa kutoa elimu kuhusu Sheria Na. 11 ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini ya mwaka 2004 kwa watumishi wote wa Wizara. Aidha, watumishi 111 wa Wizara walipatiwa mafunzo ya utawala bora, kanuni na taratibu za kazi, udhibiti wa rushwa na uzingatiaji wa maadili mahali pa kazi. Wizara itaendelea kusimamia maadili ya Utumishi wa Umma katika mwaka wa fedha 2010/2011 na kiasi cha shilingi 32,080,000/= kinatarajiwa kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeendelea kuwapatia mafunzo watumishi kwa kuzingatia Mpango wa Kuendeleza Rasilimali Watu kwa lengo la kuwaongezea ari na ufanisi wa kazi. Katika mwaka 2009/2010, kiasi cha shilingi 125,191,530 kilitumika kutoa mafunzo ya muda mfupi, kati na ya muda mrefu kwa watumishi 51 katika nyanja mbalimali. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara yangu imetenga shilingi 17,800,000/= kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wake kwa lengo la kuwaongezea ari ya utendaji kazi, ufanisi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi 34 wamepandishwa vyeo kwa kipindi cha 2009/2010. Aidha, watumishi 217 wamethibitishwa kazini na wengine 222 wameingizwa katika Masharti ya Kudumu na Pensheni. Kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 Wizara imetenga shilingi 37,890,000/= kwa ajili yakuwapandisha vyeo watumishi wa kada mbalimbali kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ili kuwapa ari ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2009/2010, Wizara yangu imeanza kutekeleza utaratibu wa kupima matokeo ya utendaji kazi kwa uwazi ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji wa watumishi kwa kijiwekea malengo yanayopimika. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa kila mtumishi anapangiwa kazi za kutosha kulingana na majukumu ya Wizara na kufanya tathmini ya utendaji wake. Aidha, Wizara yangu ilitoa mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Kupima Utendaji Kazi (*Open Performance Review Appraisal System - OPRAS*) mwezi Aprili, 2010 kwa watumishi 155 wa Wizara ikiwa ni sehemu ya

utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Kuboresha Sekta ya Umma. Jumla ya shilingi 40,000,000/= zilitumika kwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ilitumia Shilingi 1,311,000,000/= katika kuendelea na awamu ya nne ya ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ambalo limekamilika kwa asilimia 90. Aidha, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara inatarajia kutumia jumla ya shilingi 1,021,546,700/= kukamilisha jengo hilo sambamba na uwekaji wa mazingira mazuri ya ofisi pamoja na ununuzi wa samani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Nne imekuwa ikisisitiza utoaji huduma kwa wananchi kwa kiwango cha juu kwa wakati. Katika kufanikisha azma hii, Wizara katika mwaka wa fedha 2009/2010 imeendelea kutekeleza mkakati wa kuelimisha watumishi kuhusu utoaji huduma kwa mteja. Jumla ya watumishi 85 wa kada mbalimbali wamepata mafunzo hayo na kiasi cha shilingi 20,000,000/= kilitumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa mwaka wa fedha 2009/2010 iliendesha vikao viwili nya Baraza la Wafanyakazi. Kimoja mwezi Desemba, 2009 na kingine Juni, 2010 kwa lengo la kuwashirikisha wafanyakazi katika masuala muhimu yanayowahusu. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara inatarajia kutumia shilingi 38,410,750/= kuendesha vikao viwili kwa wajumbe 38 wa Baraza la Wafanyakazi. Aidha, Wizara imetenga shilingi 19,100,000/= kuratibu kikao kimoja cha ushirikiano na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, UKIMWI ni janga la Kitaifa, kijamii na kikazi. Kutokana na athari zake kwa nguvu kazi yenye uelewa, elimu, uzoefu na utaalam ambalo taifa limewekeza kwa kipindi kirefu ili kuwapata. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara yangu imetumia kiasi cha shilingi 66,000,000/= kuwawezesha watumishi 111 kupata elimu ya masuala ya UKIMWI mahala pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, mapitio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika Awamu ya Nne na Malengo ya mwaka 2010/2011 yanaonesha ni kiasi gani Wizara yangu ilivyo mtambuka, na hivyo kuhitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali katika kuimarisha na kuleta ufanisi katika utendaji wa Wizara hii. Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuiwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika maendeleo yao binafsi na Taifa letu kwa ujumla. Lengo letu sote, ikiwa pamoja na Wizara yangu, ni kupunguza umaskini kwa kuboresha maisha ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kumshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Lucy Sawere Nkya Mbunge, kwa ushirikiano, ushauri na usaidizi mkubwa anaonipa katika kuongoza Wizara hii. Vilevile, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Bibi Mariam J. Mwaffisi, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa Idara, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Wanawake Tanzania, Wakuu wa Vyuo na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu wa ngazi zote na waliopo kwenye taasisi zetu zote, kwa jitihada zao katika

utekelezaji wa majukumu ya Wizara, ambayo ni pamoja na kuniwezesha mimi kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Juhudi zao na maarifa katika utekelezaji wa majukumu tuliyonayo umeweza kuendeleza sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza hotuba yangu, sina budi kuwashukuru wale wote tunaofanya nao kazi na wengine ambao kwa namna moja au nyingine tunashirikiana. Peke yetu kama Wizara tusingefikia mafanikio niliyoyataja. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu, kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao: Asasi ya Wanawake na Maendeleo (*WAMA*), Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*), Mtandao wa Jinsia Tanzania (*TGNP*), Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (*TAWLA*), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (*TAMWA*), Shirikisho la Vyama vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (*FAWETA*), *Medical Women Association of Tanzania (MEWATA)*, *White Ribon, Friedrich Ebert Stiftung (FES)*, *Hanns Seidel Foundation, Plan International*, Mashirika mbalimbali yasiyo ya Kiserikali pamoja na wale wanaofanya kazi kwa maslahi ya jamii kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzishukuru Serikali za nchi rafiki ambazo kwa kupitia Mashirika yake zinaendelea kutusaidia. Nchi hizo ni pamoja na Marekani (*USAID*), Denmark (*DANIDA*) na Canada (*CIDA*). Aidha, Mashirika ya Kimataifa ambayo ni: *UNICEF, UNDP, UNFPA, UNESCO*, Mfuko wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Maendeleo ya Wanawake (*UNIFEM*), pamoja na mashirika mengine ya ndani na nje nayo pia nayashukuru kwa misaada yake. Aidha, napenda kuwashukuru Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*), *ILO*, Ubalozi wa Ireland na Ubalozi wa Uingereza kwa kuwa tayari kushirikiana nasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, namshukuru sana Mume wangu Mheshimiwa Samwel Sitta Mbunge, ambaye amekuwa msaada mkubwa sana kwangu, nawashukuru pia watoto wangu na familia yetu kwa ujumla kwa kuniwezesha kufanya kazi kwa utulivu, nawashukuru sana Walimu kwa kupitia chama chao *CWT* na wafanyakazi wote kwa kupitia shirikisho la Wafanyakazi *TUCTA* kwa kuniwezesha kuingia Bungeni. Nitakumbuka daima ushirikiano walionipa. Pia wamenipa uzoefu mkubwa, uzoefu nilioupata kwenye uongozi wa kujenga hoja nilipokuwa Rais wa Chama cha Walimu, pia nilipokuwa Mwenyekiti wa Shirikisho la Wafanyakazi *TUCTA*, umenisaidia kupata uzoefu katika kuongoza majadiliano yanayozaa matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu huu wa uongozi wa kujenga hoja na kuongoza majadiliano yanayozaa matunda ni nyenzo nzuri na muhimu ya kuwezesha kuzikabili changamoto zinazowakabili wanawake. Kwa wanawake wa Tabora ninakotoka ninakogombea, nina imani watanikubali ili nitumie uzoefu nilionao katika uchaguzi huu ujao ili kwa pamoja tusaidiane nao katika kupata maendeleo ya kijamii, kisiasa na hasa kiuchumi ili tuweze kupambana na adui umaskini kwa faida yetu sisi wanawake, faida ya moka wetu wa Tabora na Taifa kwa ujumla. Ninawaomba wanawake wa Tabora wanipe ushirikiano huu muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio ya Bajeti ya Wizara mwaka 2010/2011. Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2010/2011, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe matumizi ya Shilingi 19,884,684,000/=, kati ya hizo Shilingi 11,606,361,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo Shilingi 6,591,759,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 5,014,602,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (*other charges*). Aidha, Shilingi 8,278,323,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo Shilingi 6,755,523,000/- ni fedha za hapa nchini na Shilingi 1,522,800,000/- ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)
WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. HAROUB SAID MASOUD (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII): Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kusoma hotuba ya Kamati yangu naomba niseme machache ambayo Mheshimiwa Chilolo alinieleza asubuhi. Anasema anamshangaa Spika anaumwa namna ile hawezi kuondoka? Nikamwambia leo hatumwi mtoto hapa kwa sababu ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kabla sijaanza niseme maneno machache ya kuwaaga Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Uongozi wa Bunge na Wafanyakazi wote wa Bunge. Sitagombea nafasi hii safari hii. Nimeamua mwenyewe kwa ridhaa yangu nipumzike, na nimewapa nasaha wenzangu kwamba wale waliopo katika Kamati wajitahidi wagombee nafasi zao warudi na waombe Kamati ile ile. Lakini vile vile niliwaambia wawe na ushirikiano kama tulivyokuwa nayo kabla katika Wizara zetu zote tatu, *Inshallah* Mwenyezi Mungu atawasaidia na atawarejesha wote kwa kishindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 na Kanuni 114(11), nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kuniruhusu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati naomba nitumie fursa hii kutoa salamu za pole kwa Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kufiwa na Mume wake. Aidha, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa vile vile kwa kufiwa na Mume wake, wote kwa pamoja tunawapa pole na kuwaombe kwa Mwenyezi Mungu awape nguvu na ujasiri katika wakati huu mgumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilifanya kazi ya kuchambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto Tarehe 31 Mei, 2010 na terehe 1 Juni 2010 Mjini Dar es Salaam. Katika kikao cha Kamati ilipewa taarifa ya utekelezaji wa malengo yaliyomo katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 na pia Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2010/2011. Maelezo hayo yalitolewa na Mheshimiwa Magreth Sitta, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Aidha, alitoa ufanuzi kuhusu dira, dhima, majukumu ya Wizara na utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati ilielezwa kwa kina kuhusu utekelezaji wa mpango wa Maendeleo, Mapato na Matumizi kwa mwaka 2009/2010. Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha pamoja na kazi zilizopangwa kufanywa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Kamati yangu ilitoa maoni na maagizo katika maeneo mbalimbali na hasa yanayohusu:-

- (i) Kuongeza bajeti ya Wizara Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto;
- (ii) Mkakati wa kusambaza teknolojia sahihi na rahisi kupitia mafunzo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;
- (iii) Kufufua na kuimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs);
- (iv) Mikakati ya kurekebisha sheria zinazohusu haki za Wanawake na Watoto;
- (v) Teknolojia rahisi katika kuhamasisha wanaume kufanya kazi na kusaidia wanawake;
- (vi) Fedha za Mfuko wa Maendeleo *WDF* kupelekwa katika *SACCOS* zinazotambulika;
- (vii) Uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Wanawake;
- (viii) Mkakati wa kufikia asilimia hamsini kwa hamsini;

- (ix) Maendeleo ya mtoto nchini, mikakati ya kuboresha utendaji kazi wa taasisi zisizo za Kiserikali (*NGOs*) hapa nchini;
- (x) Mikakati ya kuboresha sekta ya maenendeleo ya jamii nchini;

- (xi) Mikakati ya kupata fedha kwa ajili ya mafunzo kwa Maafisa Maendeleo wa Wilaya na Kata; na

- (xii) Mikakati ya ujenzi wa ofisi za Wizara na nyumba za viongozi wa Wizara Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kiliarifu Bunge lako kuwa Wizara kwa kiasi kikubwa imefanya kazi ushauri wa Kamati katika maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudzi zaidi zinahitajika itaendelea kushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2009/2010. Katika Mwaka wa Fedha 2009/2010 Wizara iliidhinishiwa na Bunge matumizi ya shilingi 21.6 bilioni. Kamati ilielezwa kwa undani kuhusu matumizi katika kutekeleza bajeti ya Mwaka 2009/2010. Baadhi ya shughuli zilizotekelawa na mafanikio yake ni kama ilivyoorodheshwa hapa chini.

(i) Wizara kupitia Benki ya Wanawake, jumla ya akaunti 9,990 zilifunguliwa kufikia Aprili 30, 2010. Kati ya hizo akaunti 8,008 zilifunguliwa na wanawake na 1,751 zilifunguliwa na wanaume;

(ii) Wizara imeendelea kupeleka fedha kwenye Halmashauri kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*WDF*) na kwa mwaka 2009/2010 Serikali imekopesha shilingi 172,000,000/=;

(iii) Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*) ilichangia shilingi milioni kumi (10,000,000/=) ili kuwezesha mafunzo ya biashara na ujasiriamali kwa wanawake 450 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara;

(iv) Rasimu ya Waraka wa Mkakati wa Kuwezesha Tanzania Kuongeza Ushiriki wa Wanawake katika ngazi mbalimbali za uongozi wa kisiasa, kiutendaji na nafasi za maamuzi umekamilika na kuwasilishwa katika ngazi ya mwisho ya maamuzi;

(v) Rasimu ya Mwongozo wa kuboresha utendaji wa Dawati la Jinsia imeandaliwa;

(vi) Mafunzo yanayohusu kuzuia ukatili wa kijinsia yametolewa kwa Polisi 40 na viongozi wa kijamii ili kuongeza uelewa wao katika kukabiliana na vitendo vyta ukatili wa kijinsia;

(vii) Wizara kwa kushirikiana na *UNESCO* na *UNIFEM* walifanya mkutano wa wataalam na wanasheria kutoka nchi Wanachama wa Ukanda wa Maziwa Makuu ambao ulijadili kuhusu uanzishwaji wa Vituo vya Takwimu za Kijinsia. Jumla ya washiriki 40 kutoka nchi za Burundi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Uganda, Tanzania na Congo Brazaville walihudhuria;

(viii) Vyuo vya Maendeleo ya wananchi viliwezesha kudahili na kutoa mafunzo ya maarifa na stadi za maisha ndani na nje ya vyuo kwa washiriki 31,039 ili kuinua viwango vya uzalishaji mali na kujitegemea;

(ix) Katika suala la ufuatiliaji wa Haki na ustawi wa Mtoto, Wizara imeanza mchakato wa kuandaa Sera ya malezi, Makuzi na Maendeleo ya mtoto na utekelezaji wake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo Wizara, Idara na Taasisi za Serikali;

(x) Katika uratibu wa Mashirika yasiyo ya kiserikali, Wizara imeendelea na usajili wa *NGOs* na kutoa Cheti cha Ukubalifu. Kufikia Mei, 2010, idadi ya *NGOs* zilizosajiliwa na kupata cheti cha usajili ni 3,755 ambapo Mashirika 618 yalisajiliwa na kupata cheti cha ukubalifu katika kipindi cha mwaka 2009/2010 ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.5; na

(xi) Wizara imeendelea na zoezi la kuingiza taarifa za sekta ya *NGOs* katika Tovuti ya *NGOs*. Tovuti hii itasaidia kutoa fursa kwa wadau kupata taarifa za *NGOs* wakati wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya, Kamati ilielezwa kuhusu changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza bajeti ya Wizara kwa mwaka 2009/2010. Changamoto hizo ni:-

(i) Uhaba wa vifaa/nyenzo za kufanya kazi hii iliathiri sana utendaji kazi na utoaji wa huduma;

(ii) Ucheleweshwaji wa utoaji wa fedha hasa za maendeleo kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi;

(iii) Utoaji wa fedha kidogo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa ambao unasababisha utumiaji wa fedha vyuoni kukosa uhakika na kuzorotesha utoaji huduma vyuoni; na

(iv) Uhaba wa Wafanyakazi na Bajeti ndogo inayotolewa kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2009/2010. Ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2010/2011, imeomba kiasi cha shilingi 19,884,684,000 ikiwa ni upungufu wa Bajeti ya Wizara kutoka shilingi bilioni 21.6 ya mwaka wa fedha 2009/2010. Upungufu huu kwa kiasi kikubwa utapunguza utekelezaji wa vipaumbele vya wizara ambavyo vimeonekana kuwa ni muhimu. Vipaumbele hivyo ni pamoja na:-

(i) Kujenga uwezo wa Wizara katika ufuatiliaji na tathmini za shughuli za Wizara;

(ii) Kutekeleza Mikataba ya Kikanda na Kimataifa; itifaki za usawa wa kijinsia Maendeleo ya wanawake; Haki na ustawi wa motto; na

(iii) Kuendelea kuimarisha Benki ya wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata taarifa na maelezo ya malengo na kazi zilizopangwa kufanywa kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Kamati ilijadili kwa undani masuala mbalimbali na kuipitisha bajeti ya Wizara hii. Kamati yangu inaunga mkono maombi ya Wizara, hata hivyo, Kamati inatoa maoni na ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nisome kuhusu maoni na ushauri wa Kamati. Kuongeza Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kwa namna ya pekee tunaipongeza Wizara kwa kuzingatia wito wa Kilimo Kwanza kwa mifano halisi kwa kuwa sasa iko kwenye mchakato wa kusambaza teknolojia sahihi na rahisi kupitia mafunzo yatakayotolewa katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Mafunzo hayo yanatarajiwa kuendeshwa katika Kanda saba (7) za Kaskazini, Magharibi, Mashariki, Kati, Kanda ya ziwa, Nyanda za Juu Kusini na Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kupitia hazina kutoa fedha za miradi kwa muda muafaka ili kuirahisishia Wizara kutekeleza miradi muhimu kama hii kwani mpango huu utatoa msukumo maalum katika shughuli za kilimo hususan katika Mikoa sita inayozalisha chakula kwa wingi nchini yaani Iringa, Mbeya, Ruvuma, Kigoma, Rukwa na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Kwa namna ya pekee Kamati inaipongeza serikali kupitia wizara kwa kuongeza fursa ya ushiriki wa wananchi katika maendeleo kupitia mashirika yasiyo ya Kiserikali kufuatia uboreshaji wa zoezi la usajili wa Mashirika hayo chini ya Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*WDF*) kuwafikia wanawake wa vijijini. Kwa kuwa kwa muda mrefu fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake zilikuwa zinapelekwa katika Halmashauri mbalimbali ili waweze kuzikopesha kwa vikundi vya wanawake na kwa kuwa utaratibu huo umekuwa na manufaa kidogo sana kwa kuwa wanawake wa vijijini hawanufaiki. Kamati inashauri pawepo na juhudzi za makusudi za kuhimiza ushirikiano kati ya maafisa maendeleo ya jamii na Wabunge wa maeneo husika. Hatua hii itahamasisha utekelezaji kwa kuwa Wabunge wako karibu zaidi na wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uimarishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania. Kwa kuwa mchakato wa uanzishwaji wa benki ya Wanawake Tanzania umekamilika na Kwa kuwa kufungua matawi Mikoani ni mpango wa muda mrefu na kwa kuwa, mahitaji ni makubwa kwa wananchi kupata huduma hizi za kibenki, Kamati inaishauri Serikali kufungua vituo mikoani kwa ajili ya kukopesha wajasiriamali wadogowadogo wakati ufunguzi wa matawi ya benki ukisubiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikakati ya kutayarisha bajeti kwa kuzingatia mtazamo wa Jinsia. Kwa kuwa jinsia sio suala la Wanawake bali ni mahusiano ya kijamii

kati ya wanaume na wanawake, mahusiano ambayo yamejengwa na jamii hasa katika mgawanyo wa mali, habari na mahusiano katika shughuli mbalimbali na kwa kuwa maandalizi ya bajeti huwa yanaanza mapema, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(a) Bunge lishirikishwe mapema katika mchakato wa bajeti yaani kujadili vyanzo vya mapato, namna ya kufikia vipaumbele na vigezo vya kuweka kiwango cha juu cha bajeti (*ceiling*) kwa kila Wizara na Idara zinazojitegemea.

(b) Kwa kuwa ni muhimu sana kwa wabunge na Makatibu Wakuu kukaa pamoja katika kuelimishana kuhusu miongozo ya bajeti (*budget guidelines*) na namna ya kuboresha bajeti kwa kufuata misingi ya jinsia, Kamati inapendekeza kwamba kila mwaka iandaliwe semina ya mafunzo kati ya Kamati Makatibu Wakuu kwa lengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inampongeza Rais wa Serikali ya Awamu ya Nne kwanza kwa kutambua mchango wa wanawake katika nyanja zote; kilimo, siasa, uchumi na hata uongozi kwa dhamira njema. Mheshimiwa Rais amefanya uteuzi katika nyadhifa mbalimbali kwa kuteua wanawake ili wajengewe mazingira ya kuonesha uwezo wao. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali ikamilishe mchakato wa kuhakikisha wanawake wanaingia kwa wingi katika vyombo vya maamuzi katika uchaguzi huu wa 2010 hasa katika Mabaraza ya Halmashauri na Bunge. Dhamira njema ijengwe na hasa kupitia Serikali na Vyama vya Siasa kuhakikisha kwamba wanawake wengi wanachaguliwa na kuteuliwa katika majimbo na idadi ya viti maalum inaongezeka ‘Wanawake wasiogope, wanaume wasihofu kwa pamoja tushirikiane’.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Vyuo maendeleo ya Jamii bado havijajitosheleza kiitaluma na kwa kuwa Chuo cha Ufundı cha VETA kinatoa elimu nzuri na za ujasiriamali kwa vyuo vingine, Kamati inashauri VETA itoe msaada kwa Vyuo hivi vya Maendeleo ya Jamii au ikiwezekana viunganishwe ili viweze kutoa Mafunzo kwa wahitimu na hatimaye waweze kujajiri wenywewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu naomba kukushukuru wewe binafsi, kwanza kwa namna unavyoendesha Vikao vya Bunge kwa umahiri na busara na kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Pia kumshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge ambao ndio misingi wa mafanikio ya Bunge katika shughuli zake za kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Naibu Waziri; Katibu Mkuu, Ndugu Mariam Mwafisi ambaye hivi karibuni ninasikia anastaafu, Mwenyezi Mungu atamweka mahali pazuri kuliko hapo.

Pia nawashukuru Watumishi wote wa Wizara na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru sana na kuwatachia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na Wajumbe wenzangu kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti; Mheshimiwa Haroub S. Masoud, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mjumbe; Mheshimiwa Fatma O. Ally, Mjumbe; Mheshimiwa Ameir A. Ameir, Mjumbe; Mheshimiwa Zuleikha Y. Haji, Mjumbe; Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mjumbe; Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mjumbe; Mheshimiwa Salim A. Khalfan, Mjumbe; Mheshimiwa Mwajuma H. Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mjumbe; Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, Mjumbe; Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mjumbe; Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mjumbe; Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mjumbe; Mheshimiwa Kiumbwa M. Mbaraka, Mjumbe; Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mjumbe; Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Gertrude P. Rwakatare, Mjumbe; Mheshimiwa Mohamed A. Said, Mjumbe; Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mjumbe na Mheshimiwa Elietha N. Switi, Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashillilah kwa kazi nzito anayofanya akisaidiwa na Makatibu wa Kamati Ndugu Elieka Saanya na Ndugu Rachel Nyega katika kuihudumia Kamati hii ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa hii kwa wakati unaotakiwa. Nashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsanteni. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Haroub Said Masoud, wewe siku zote ni mtetezi wa masuala ya wanawake katika nchi hii. Kwa hiyo, sisi tunakujuwa kwa miaka yote na kama alivyosema Mheshimiwa kwamba, katika kinyang'anyiro hiki jamani mkikuta wagombea wako 10 na mwanamke uko mmoja, usiogope wanaume na kila mtu asihofu ila mwende pamoja tu. (*Makofi*)

Sasa nitamwita Msemaji Mkuu kutoka Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii, Mheshimiwa Anna M. Komu, Waziri Kivuli.

MHE. ANNA MAULIDAH KOMU- MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa napenda kutumia fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu Na. 99(7) Toleo la Mwaka 2007. Kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, amani na upendo kwa kutujaalia kukutana kwetu

leo hii tukiwa bukheri wa afya. Pia niwashukuru wanachama wote na viongozi wa chama changu, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). kwa ushirikianao wa dhati walionao katika kujenga demokrasia makini nchini na kujizatiti katika kuleta changamoto ya demokrasia ya vyama vingi. Nami naendelea kuwaahidi uzi ni uleule, kama nilivyoahidi nitaendelea kufanya kila lililo ndani ya uwezo wangu kutimiza majukumu niliyopewa na chama changu pamoja na Watanzania wote kwa ujumla. Hakuna kulala mpaka kieleweke.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, kwa kuendelea kuniamini na kunipa fursa hii ya kuiwakilisha Wizara hii nyeti, muhimu na tegemeo la Watanzania wote kwa mara nyingine tena. Sanjari na hilo pia napenda kuwashukuru Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano wanaonipa ndani na nje ya bunge. Bila kumsahau Naibu Waziri kivuli wa Wizara hii, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika kwa msaada wake wa mawazo na hekima katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea na hotuba yangu naomba nichukue fursa hii kuwaombea wale wote tulioanza nao Bunge hili siku ya kwanza na baadaye Mwenyezi Mungu mwangi wa Rehema akaamua kuwapenda zaidi na wakaondoka katika ulimwengu huu na pia bila kuwasahau ndugu, jamaa na wapenzi wetu waliotangulia mbele ya haki, Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendelo ya jamii ina tafsiri pana sana. Hii inajumuisha maendeleo kwa wananchi wote wa jinsia zote. Mara nyingi, tumekuwa tukipima maendeleo hayo kwa kutumia pato la mwananchi kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongelea maendeleo ya jamii maana yake ni mkusanyiko wa familia au kaya kuwa na uwezo wa kumudu maisha bora ya binadamu, katika nyanja mbalimbali. Kwani tunaamini maendeleo ya jamii yanaanzia katika ngazi ya Kaya. Kama kaya inashindwa kumudu milo mitatu kwa siku hatuwezi kusema kuwa jamii hiyo ina maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imekuwa ikitoa tahadhari siku zote ni kwa vipi Serikali inaweza kuleta maendeleo kwa jamii ya Watanzania, lakini kwa makusudi tu imekataa kuzingatia ushauri wetu. Hili la Serikali kuleta maendeleo ya jamii limeshindikana japokuwa Serikali iliunda Wizara maalum kwa ajili ya kuleta maendeleo katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pato la Taifa ni tshs. 28 trillioni na idadi ya watu ni 40.7 milioni kwa bei za mwaka 2001,takwimu zinaonyesha pia kuwa pato halisi la Taifa ni asilimia 6.0 mwaka 2009 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.4 mwaka 2008. Lakini pato la wastani kwa siku kila Mtanzania sasa hivi ni shs. 693,185 mwaka 2009 ikilinganishwa na shs 628,259 mwaka 2008. Sawa ni ongezeko la asilimia 10.3 ambalo wengine wanasherehekea. Hii ni fedheha, ni aibu kwa Serikali iliyoko madarakani. Kwani mbona hatupimi ukuaji wa ugumu wa maisha? Je, shs 600, mtanzania huyu

anakula nini? Anaweza kusomesha mtoto wake au kununua pembejeo? Kambi ya Upinzani inachukua nafasi hii kuungana na wananchi wote ambaو wanaendelea kutaabika kutokana na adha za maisha magumu yanayo wakabili kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ufanuzi ni jinsi gani Serikali haina nia ya dhati katika kuwandolea wananchi wake umaskini, kuweka kumbukumbu sahihi katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, aliongelea Mfuko wa Rais wa Kuwawezesha Wananchi (*Presidential Trust Fund*) kuwa badala ya kuwawezesha wananchi unachangia kuwaongezea umaskini wananchi wenyewe kipato kidogo kwani kiwango cha riba kinachotozwa ni asilimia 30 kwa mwaka ikiwa ni asilimia 2.5 kwa mwezi, hii ni zaidi ya kiwango kinachotozwa na mabenki ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hoja ni kuwa Mfuko huu umekuwa wa kibiashara zaidi kuliko madhumuni yake ya kumsaidia mwananchi, kwani fedha za Mfuko huu kwa kiasi kikubwa zinatoka Serikalini na jina la Mfuko ni Mfuko wa Rais na Mfuko wa Rais kufanyabiashara kama unavyofanya ni sawa na mtumishi kumuibia mwajiri wake. Rais ameajiriwa na wananchi waliompa ridhaa yao kwa njia ya kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Viongozi kwa makusudi kabisa wanapotosha Umma wa Watanzania ni lile ambalo Kambi ya Upinzani imekuwa ikitoa ushauri kuwa Wake wa Marais ni watu wanaofanya kazi nzuri na kubwa katika kuona jamii ya Watanzania wanapata maendeleo, lakini kile chombo wanachokitumia katika kutimiza kazi hizo ni chombo binafsi. Hoja hapa ni kwamba *EOTF* iliyokuwa inasimamiwa na Mama Mkapa, *WAMA* inayosimamiwa na Mama Kikwete zinatakiwa asasi hizo ziwe na Miliki ya Ikulu kama taasisi maalum kwa Mke wa Rais atakayekuwepo na sio zao binafsi kama ilivyo sasa. Jambo hili linawatia kasoro wake wa Marais kama vile wamekuja kujenga taasisi zao binafsi kwa kutumia mgongo wa Rais. Hili linatia aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ni muda umepita tangu wanawake waanze kudai kuwa na Baraza lao litakalowaunganisha wanawake wote wa Tanzania bila kujali itikadi zao za kisiasa. Hili lilianza kujitokeza baada ya kuingia kwa mfumo wa siasa za vyama vingi pale UWT ilipopoteza uhalali wa kuwa Umoja wa Wanawake wote wa Tanzania kwani ulikuwa ni Tawi la CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inafarijika na kuupongeza kwa dhati mkakati ulioanzishwa na umoja wa Wanawake waliomo Bungeni (*TWPG*) kuanzisha chombo kitakachowaunganisha wanawake wote bila ya kujali itikadi zao (ULINGO), ambacho kipo chini ya Mheshimiwa Anna Abdallah. Tunaamini huu ni mwanzo mzuri katika uundwaji wa Baraza la Wanawake wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake ndio wanaelewa matatizo yao hivyo kungojea Serikali ifanye taratibu za kuanzisha Baraza ni kupoteza muda kwani, watendaji

tunaowategemea Serikalini ni wanaume, ambao hawaelewi ni nini wanachohitaji wanawake katika hali ya sasa ya ushindani. Hongera sana Mheshimiwa Mama Anna Abdalla, Mbunge na Makamu wako Mheshimiwa Suzan Lyimo Mbunge, pamoja na wajumbe wote wa *TWPG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na asasi nyingi sana zinazotoa mikopo kwa akina akinamama kupitia Wizara hii, lakini hali halisi inaonyesha kuwa mikopo hiyo haiwafikii walengwa ambao ni akina mama wakule vijijini. Kambi inaona hapa kuna tatizo kubwa, inaweza kuwa ni dawati linaloshughulikia suala hilo halifanyi kazi zake kwa utaratibu unaotakiwa, au riba inayotozwa ni kubwa mno na pengine masharti yanayotolewa ni magumu kiasi kwamba walengwa wanashindwa kuyatimiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za akinamama walionufaika ukiangalia ni kuwa karibu wote wanatoka maeneo ya mijini na hivyo takwimu hizo zinatolewa kijumla jumla tu. Kambi ya Upinzani inasema kuwa mtindo huu wa utolewaji takwimu za jumla unaifanya Serikali ishindwe kutatua tatizo la msingi la hali halisi ilivyo kwa akinamama waishio vijijini. Ili kutibu tatizo hili ingeonyeshwa takwimu kulingana na wanawake wangapi Wilaya, Kata, Kijiji fulani wamepata mikopo. Tunasema hivyo kwa kuwa idadi ya vijiji inajulikana kwa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo lingine ambalo limeendelea kufanya wanawake waonekane kuwa wametengwa na Serikali yao, ni suala zima la mirathi. Kwa sasa hakuna idara rasmi katika Wizara ya Maendeleo ya Jinsia na Watoto kwa ajili ya kuwasaidia wanawake wajane wanaodhalilishwa kwenye kadhia nzima ya mirathi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliona hili kwani ni kero kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake tunaendelea kuiomba jamii kutuona kwamba tunaweza sana, tupewe nafasi ili tuendelee na ustawishaji wa jamii zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kuwa mgawanyo wa kazi huletea ufanisi yaani *specialization leads to efficiency* na Wahenga walisema mikono mingi huharibu mapishi. Kambi ya Upinzani inauliza, kwa nini tunakuwa na Wizara zaidi ya moja katika kushughulikia suala moja (hili linaitwa jambo mtambuka). Hii kwa maana nyingine ni kigezo cha kukwepa majukumu ya msingi ya Wizara husika, kwani unaambiwa kazi zake zingine ziko Wizara nyingine na kasma ya shughuli iko kwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhihirisha hili naomba nitoe mfano mdogo ambao ni moja ya vitu vinavyosababisha mkanganyiko huo wa majukumu. Suala la watoto, Idara zinazojikita katika kushughulikia masuala ya watoto ziko katika Wizara tatu tofauti. Nazo ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya tatifi zilizofanywa mwaka juzi na baadhi ya Halmashauri nchini, zinaonyesha jumla ya watoto 437,544 wapo katika mazingira hatarishi. Huu ni wakati wa jamii kuangalia namna ya kuwaondoa watoto wa mitaani ili kuondokana na tatizo la kuzagaa kwa watoto hawa. Ni vizuri kukawa na mpango

madhubuti wa kuwasaidia waliopo mitaani na kuzuia wengine kutoingia katika hatari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la watoto wa mitaani wanasababishwa na mambo mengi yanayozikabili familia, yafuatayo ni baadhi ya mambo hayo:-

(1) Kutengana kwa wazazi (mifarakano katika ndoa) kumekuwa ni tatizo linalosababisha kuongezeka kwa watoto wa mitaani, mila na tamaduni za makabila zetu zinatofautia kuna makabila ndoa ikishavunjika basi na watoto ndio wanaokuwa waathirika wakubwa wa mtafaruku huo;

(2) Mimba za utotoni ambazo kwa kiasi kikubwa inachangiwa na jinsi familia zinavyotoa malezi kwa watoto wao na hivyo kupelekea tabia binafsi ya mhusika;

(3) Watoto kuzaliwa nje ya ndoa ni tatizo lingine linalosababisha watoto wa mitaani kuongezeka;

(4) Vifo vya wazazi ni chanzo kingine cha kuongezeka kwa watoto wa mitaani, vifo hivi vinatokana na magonjwa na ajali mbalimbali vinavyozidi kushamiri katika nchi yetu;

(5) Ukatili, unyanyasaji na umaskini uliokithiri katika baadhi ya familia. Kutokana na sababu hizo, watoto hawa wamekuwa wakikibiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo kutopata elimu, malazi, mavazi, matibabu, ulinzi na malezi bora. Matatizo haya kwa asilimia kubwa husababisha watoto hawa kukimbilia mitaani; na

(6) Jambo lingine ni familia kutokujibika kwa watoto wao na hivyo kupelekea watoto kutokuwa na msimamizi na mshauri kwenye ngazi hiyo muhimu katika makuzi ya vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, matatizo hayo yote niliyoyaeleza hapo juu mengi yake si ya kuilaumu Serikali bali ni sisi wote kama wazazi tuwajibike kwa familia zetu na kwa njia hiyo tutatengeza jamii ya vijana watakaokuwa wawajibikaji (*responsible society*). Hivyo basi Kambi ya Upinzani inaishauri jamii ya Watanzania wote bila kubagua itikadi za kisiasa, kidini na kimila kuwajibika kwa familia zao kwanza (*responsible society*) na kuhakikisha tunawalea watoto wetu kwenye mila na tamaduni zetu bila ya kutoa sababu za umaskini na kuwaacha watoto wetu kuzagaa mijini na kuwatuma kufanya shughuli zisizo na msimamo mwema wa maisha ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko mitaani hupata athari kubwa kwa jamii kutokana na ukweli kwamba huku ndiko baadhi ya watoto wanapoanza kutumia mihadarati, kujihusisha na vitendo vya ukahaba, unyang'anyi na ujambazi. Hakuna asiyejua watoto wa mitaani shida wanayoipata, wengi hifuata mkumbo wa watoto wenzao katika kutafuta maisha kwa njia ya kuombamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari zingine zinazotokana na kutokujibika kwa jamii ni kuzalisha viongozi wasio na maadili pale wanapopewa dhamana ya kusimamia na kulinda rasilimali za jamii. Jambo ili linasababisha madhara ambayo tunayaona sasa ya kuwa na wala rushwa, mafisadi papa na wale wote wanaotumia nafasi zao za kiutendaji kwa manufaa binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sababu ambazo tumejitahidi kuzieleza hapo, mwisho anayeathirika ni mtoto. Katika hilo Serikali imeshindwa kuoanisha Ustawi wa Jamii na Ustawi wa Mtoto, ambaye tunasema kuwa ni Taifa la kesho. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya muundo wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwani Wizara hizi kuwa katika Wizara mbili tofauti ndivyo inavyokuwa vigumu kutoa huduma stahili kwa mtoto. Kama nilivyowahi kusema katika hotuba yangu ya mwaka 2008 kuwa nanukuu: “Sote tunafahamu kuwa mgawanyo wa kazi huleta ufanisi yaani “*specialization leads to efficiency*” na wahenga walisema mikono mingi huharibu mapishi. Tunakuwa na Wizara zaidi ya moja katika kushughulikia suala moja (hili linaitwa jambo mtambuka). Hii kwa maana nyingine ni kigezo cha kukwepa majukumu ya msingi ya Wizara husika, kwani unaambiwa kazi zake zingine ziko Wizara nyingine na kasma ya shughuli iko kwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashukuru kwa kuwa na sheria mahususi ya mtoto imekwishapitishwa lakini bado kanuni zake hazijapitishwa ili sheria hii ifanye kazi, kwani sheria hii haiwezi kuanza kufanya kazi bila ya kuwa na kanuni za jinsi itakavyoteklezwa. Hivyo, Kambi ya Upinzani inaona watoto wanaendelea kunyanyasika na kuendelea kubakwa na mateso mengine, tunaomba sana Serikali ione umuhimu wa kutengeneza kanuni husika. Tunauliza kuna sababu gani ya kuharakisha sheria na kuchelewesha kutunga kanuni zake? Kwa mfano, Sheria ya UKIMWI na walemavu, tujitahidi kutoa kanuni mara baada ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofifi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa kuwasilisha taarifa yako vizuri, sasa nina wasemaji wengi nitaanza na wale ambaao hawajachangia hata mara moja ila nataka kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge wanaume walioomba kuchangia wote lazima watapata nafasi. Lakini tunaanza na wale ambaao hawajachangia hata kidogo, yuko Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na yupo Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa namna ya pekee napenda kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama katika Bunge hili Tukufu kuchangia katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika kipindi hiki cha mwaka 2010/2011. Napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa hotuba yake nzuri sana inayotegemea kuleta maendeleo kwa Watanzania. Napenda

pia nimpungeze Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji wote pamoja na afisa wote katika Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kushirikiana kwa njia moja au nyingine hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika napenda nichangie machache katika Wizara hii ikiwa ni ufinyu wa bajeti ambaa unaikabili Wizara hii. Mara nyingi tulikuwa tunasimama hapa kuchangia au kusisitiza kwamba Serikali iongeze bajeti katika Wizara hii kwa sababu ina majukumu makubwa katika jamii zetu Tanzania, katika maeneo mbalimbali. Tunakumbuka kwamba majukumu ya Wizara hii ni makubwa, ndani ya jamii zetu kuanzia Vijijini na Mijini. Tutakumbuka kwamba kuna mila mbalimbali katika jamii zetu, mila na desturi mbalimbali, Mwenyekiti wa Kamati ameeleza bayana katika taarifa yetu ya Kamati na bado mila hizi baadhi ya jamii hawajataku kuondokana nazo ambazo ni za kizamani na zinamdhilisha mwanamke. Kwa hiyo, Wizara hii ina jukumu kubwa la kuielimisha jamii na wakati huo huo hasa kule Vijijini. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali katika kipindi cha mwaka 2011/2012, kuweza kufikiria kwa kina uongezwaji wa bajeti katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ni nyingi katika Wizara hii ambazo tayari zimeshaelezwa na Mwenyekiti wa Kamati hata yule mchangiaji katika Kambi ya Upinzani amechangia mengi na Wizara yenewe katika uwasilishaji wake zinazoikabili Wizara hii. Kwa kweli inastahili kuongezewa bajeti ili kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi. Mara nyingi watendaji wa Wizara wanakuwa wanakwama katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kutokana na ufinyu wa bajeti. Tunaiomba sana Serikali iweze kufikiria kwa kina uongezwaji wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakumbuka kwamba Wizara hii inasimamia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ambavyo vinatoa elimu mbalimbali kwa wananchi mbalimbali. Lakini ni kwamba vyuo hivi bado vina upungufu mkubwa wa vifaa mbalimbali ambavyo vinahitajika katika kuendeleza utaalam ndani ya vyuo hivi. Pia vyuo hivi ni vya zamani sana kwa hiyo, vinahitaji ukarabati mkubwa na fedha mara nyingi inayotengwa haitoshi Wizara hata kwa vyuo hivi na hata maeneo mengine basi inakuwa inachelewa sana kutolewa katika utekelezaji wa ufanikishaji katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, tunaiomba Hazina kutoa fedha hizi mapema zaidi ili utekelezaji au ukarabati wa vyuo hivi na uendelezaji wa maabara na mambo mengine ufanyike kwa wakati ili kuweza kuendeleza jamii zetu huko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakumbuka kwamba katika mwaka 2009 tulipitisha sheria ya mtoto ndani ya Bunge hili Tukufu na sheria hii imeshaanza kutumika, lakini hadi sasa sheria hii bado wananchi hawajafahamu hasa wale walioko Vijijini. Naiomba Serikali kuongeza bajeti zaidi ili kuwawezesha wafanyakazi au wataalam wa Wizara hii kwenda kule Vijijini kuelimisha jamii kwa sababu bado jamii iliyotuzunguka hajjaweza kutekeleza sheria hii. Naiomba sana Serikali, tutakumbuka kwamba watoto kama ilivyosemwa katika taarifa ni maendeleo ya Taifa la kesho. Kwa hiyo, watoto wanadhalilika, wananyanyaswa hawapatiwi elimu na hasa watoto wanawake wanaachwa nyuma, wanaopewa vipaumbele ni watoto wa kiume kuliko watoto wa kike. Hata katika Mawizara tukiangalia kwa undani zaidi tunaona kwamba vijana wa kiume ni wengi zaidi katika Mawizara kuliko vijana wa kike. Kwa hiyo, huu uzoefu umejengeka zamani na

unaendelea katika baadhi ya jamii kuwafundisha zaidi watoto wa kiume kuliko watoto wa kike. Kwa hiyo, hata utekelezaji wa sheria haujaweza kutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakumbuka kwamba kupitia Bunge hili tuliagiza kwamba Wizara iweze kutafsiri sheria hiyo kwa lugha ya Kiswahili ili iweze kufahamika zaidi nchini na Wizara imeshaandaa Sera ya maendeleo ya mtoto kwa lugha ya Kiswahili lakini bado uenezwaji wa Sera hii haujaenezwa vizuri. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kuangalia kwa kina na vile vile Hazina iweze kutekeleza majukumu yake kwa kuzipatia Wizara fedha kwa wakati zaidi ili iweze kufanikisha majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza Serikali kwa kuanzisha Benki ya Wanawake nchini na pia naipongeza Serikali kwa kuweza kutenga fedha bilioni 2 katika kipindi hiki kwa madhumuni ya kuendeleza mikopo kwa wajasiriamali wanawake au wananchi kwa ujumla katika Benki hii. Nawaomba sana wananchi kuendelea kujitokeza kwa wingi kujiunga na Benki hii ili kuweza kufaidika na rasilimali zinazotolewa na Benki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa mashirikiano yao makubwa katika kipindi chote cha miaka mitano na nawaomba ridhaa yao tena katika kipindi kingine cha miaka mitano ijayo na nawashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika kipindi hiki cha 2005/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. AL-SHYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa Mheshimiwa Waziri. Kwa kweli ni hotuba nzuri sana ambayo imegusa kila nyanja katika Wizara hii.

Pili, napenda kumpongeza Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa uongozi wake mahiri katika awamu hii ya nne aliyoongoza. Uongozi wake ulikuwa mzuri sana kiasi ambacho mmeona mwenyewe ameweza kujitokeza kuchukua fomu peke yake, hakutokea mpizani. Hii inaonyesha wazi jinsi uongozi wake ulivyokuwa mzuri na tumepata sifa dunia nzima kwa uongozi wake. Inabidi tumpongeze sana Mheshimiwa Rais.

Pia, napenda kumpongeza tena Mheshimiwa Rais kwa kuwajali sana wanawake, ameweka kipaumbele sana katika teuzi nyingi ambazo ameteua, amewalenga sana wanawake. Kwa kweli inabidi tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuwapa kipaumbele wanawake, ameteua katika nyadhifa mbalimbali katika uongozi maeneo mbalimbali

kama tulivyoona katika kitabu cha mchango cha Mheshimiwa Waziri ameonyesha jinsi nyadhifa mbalimbali ambazo Mheshimiwa Rais ameziwekea kipaumbele kuwateua wanawake. Kwa hiyo, hatuna budi kumpongeza na sisi wanawake wenyewe pia tujifagilie, Mheshimiwa Rais ametujali sana. (*Makofi*)

Pili, napenda kuchangia kuhusu Benki ya Wanawake. Naipongeza sana Wizara kwa benki hii. Nampongeza Mheshimiwa Rais ndiye aliyezindua benki hii. Lakini benki hii ipo mjini tu, ipo Dar es Salaam. Sasa tukipita vijijini, akina mama wanauliza kwamba benki hii sisi tutapata vipi? Tutaweza vipi kupata mikopo? Tutafaidika vipi na benki hii? Wanatamani na wao pia wangefaidika. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti alivyosoma taarifa ya Kamati ameeleza kwamba angalau ingeenezwa pia katika Mikoa mbalimbali ili wanawake nao wa vijijini, wanawake wa hali ya chini na wao wapate faida kupata kufungua akaunti na pia kuweza kupata mikopo katika benki hizo.

Jambo la tatu ambalo napenda kuchangia ni kuhusu ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto. Naipongeza sana Wizara kwa kutoa mafunzo. Katika ukurasa wa nane tumeona katika kitabu cha hotuba, wametoa mafunzo kwa Polisi, Magereza, watu wa Mahakama ili kuweza kupambana na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto. Kwa kweli hii hali ya ukatili sasa hivi imezidi kuwa ngumu kidogo. Hali ya binadamu kumwua binadamu mwengine imekuwa yaani kama kitu rahisi sana. Mtu anamtoa roho binadamu mwengine kama mchezo tu, ambapo sisi Watanzania hatukuwa na hali hiyo. Hatuna hali hiyo sisi ya kuwa na roho ngumu ya kumtoa mtu roho. Inashangaza sana, hawa watu mimi nafikiri hawa sio Watanzania. Nimesikia kwenye TV leo asubuhi kuna baba amemchinja mke wake, amemchoma visu tumboni mke wake, amemtoa roho na yeye mwenyewe akajiua. Sasa moyo huu unatoka wapi? Kwa kweli ni jambo la kujiuliza. Ukatili umekuwa ni wa hali ya juu sana, watu wanatoana roho, watoto wanauawa, watoto wanabakwa halafu wanauawa. Ni vitu ambavyo vinauma sana, inabidi tuvifanyie kazi.

Tunaishukuru Serikali imeweka kipaumbeke kwenye suala hili. Wananchi kwa ujumla, viongozi wa dini, tunawashukuru sana, wanaendelea kupiga kelele kwenye Misikiti kwenye Makanisa wanaongelea sana suala hili ambalo sasa hivi watu miyo yao imebadilika. Lakini kutokana na hali hii, tukishirikiana wote kwa pamoja tukiongeza na ulinzi shirikishi, hali hii nina imani kwamba itakwisha kabisa na wananchi watakuwa na moyo wa imani kidogo kutokuuana wenyewe na au kuua watoto wadogo na akina mama na hali kadhalika watoto wa kiume.

Lingine ambalo ningependa kuchangia ni kwamba napenda kuwapongeza wanawake wote wa Tanzania. Napenda kuwapongeza kwa sababu wanawake wamekuwa mstari wa mbele, wanawake wamekuwa wanajitoa, wanawake wamekuwa wakifanya ujasiriamali, sasa hivi ukienda kwenye Saba Saba utakuta wanawake katika kila banda ndiyo wako mstari wa mbele zaidi katika maonyesho yanayoendelea kule Saba Saba. Nimeona kwenye TV wanavyohojiwa wanawake wajasiriamali, kwa kweli vifaa wanavyovitengeneza ukiviona huwezi kuamini, utasema hivi vifaa hawajatengeneza akina mama. Lakini kwa kweli nawapongeza. Akina mama wanafanya kazi nzuri. Kwa

niaba ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote wa humu ndani, tunawapongeza sana akina mama, wamekuwa mstari wa mbele mno, hatuna budi kuwapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kunteua kuwa Mbunge. Namshukuru sana ameniteua na nimefanya kazi yangu, namshukuru. Safari hii nitaingia tena kugombea. Nina imani akina mama wataniona na watanitambua na watanipa hiyo nafasi tena. Kwa hayo machache, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, unatangaza nia! (*Kicheko*)

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ni kweli hamjaniona siku nyingi, lakini ni mapito ya dunia tofauti tofauti, pamoja na siasa. Kazi iliyofanyika Kilindi ni kubwa mno, kufanya tathmini imechukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nishukuru, lakini kwa kuwa muda ni mfupi, nitaongea kwa haraka na kwa kifupi. Nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuwasilisha hotuba yao ya bajeti. Bajeti ni nzuri kwa kiwango chake, lakini vile vile kwa kazi nzuri wanayoifanya nikiwa Afisa Maendeleo ya Jamii ambao wote mnalitambua. Nimekuwa nikifanya kazi karibu sana na Wizara hii. Nina hakika na nina kila sababu ya kuwapongeza. Niwape pole ambaao wamefiwa katika kipindi hiki ambacho sikuwepo na hata hao waliofiwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naongea kwa kifupi kwa sababu ya muda wenyewe na mimi niungane kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuzingatia jinsia. Ni kweli kabisa katika sekta zote na nyanja zote tumeona akijitahidi kwa kasi kubwa sana kuhakikisha kwamba jinsia inazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limeendelea hata chini, huku Mikoani na Mawilayani na hususan napenda nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa wa Tanga - Saidi Kalemba na Mkuu wangu wa Wilaya - Charles Gishuli Mbegesi. Kwa kweli watu hawa kama suala halijazingatia jinsia halizungumziki wala halipitishwi. Kwa hiyo, naomba niwapongeza sana na hii imetokana na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana uanzishwaji wa benki kama wenzangu ambavyo wameongelea. Sitaki kujirudia, lakini niseme wananchi wa Kilindi nao wanaomba sana na wananchi wa Tanga kwa ujumla wanasubiri sana benki hiyo. Nimpongeze sana Mama Chacha na Watendaji wake wote kwa kazi kubwa wanayoifanya. Ukipita kwenye ile benki utaona kwamba mwitikio ni mkubwa sana. Vile vile, niweze kusema kwamba kulingana na ile Sheria ya Mtoto ambayo tulipitisha hapa ikaanza kazi tarehe 01 Aprili. Bado naona kasi kubwa ya wimbi la watoto wa mitaani hasa mjini Dar es Salaam. Lakini vile vile vijijini nako tumeshuhudia sasa hivi kasi kubwa sana ya watoto ambaao wana mazingira ya aina hiyo na kwa sababu kule tunaishi kijamii. Huwezi kusema ni wa mtaani sana, lakini mazingira wanayoishi kwa kweli ni hatarishi sana hasa ukizingatia wale wenye mimba za utotoni na tumeshuhudia siku za

karibuni, hata wazazi na baba walezi matukio yametokea wamewapa mimba watoto wao wenyewe.

Kwa hiyo, mambo haya yote nadhani kulingana na hii Sheria tuliyopitisha kuna haja kabisa ya kuweka mkazo. Lakini vile vile niishukuru sana Serikali kwa kutoa ruzuku, *OC* katika miaka hii miwili kwa Ofisi zetu za Wilaya za Maendeleo ya Jamii. Tatizo moja ni kwamba fedha hizi zikifika zinaingia kwenye *General Fund* katika Wilaya zetu. Sasa *General Fund* kwa mfano Halmashauri ina mapato kidogo, unakuta fedha hizi upatikanaji wake kwa kweli unakuwa ni mdogo sana. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria labda katika siku za usoni tuangalie uwezekano sasa wa kuweza kuwafungulia akaunti ili waweze ku-manage wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri pia ni tatizo kubwa sana kule Kilindi kwa mfano gari hawana, wanategemea kuchangia magari ya Idara nyingine Jambo ambalo linawakwamisha sana katika shughuli zao. Nadhani katika kipindi kijacho kwa kushirikiana tutaweza kuhakikisha wanapata gari. Kuhusu upimaji wa UKIMWI kasi ni nzuri, uamsho umekuwa ni mkubwa. Pia tumeshaiomba Wizara ya Afya na naomba tena kupitia Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii ambayo inajali watu tupatiwe *CD4 machine*, inabidi twende zaidi ya kilomita 132 ili kuweza kupima damu. Kwa hiyo, naomba tena nirejee kwenu ili tuweze kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza sana wananchi wa Kilindi kwa kazi nzuri sana ambayo wamekuwa wakiifanya. Naomba niwataarifu wote katika Bunge hili na Watanzania wote wanaonisikiliza. Kilindi tumetekeleza Ilani yetu ya uchaguzi kwa asilimia 95. Naomba basi makofi Waheshimiwa kwa niaba ya wananchi. (*Makofi*)

Asilimia tano inaendelea kutekelezwa kwa sababu ndiyo kwanza hela zimetoka na mambo mnayosikia hakuna kilichofanyika Kilindi, naomba niwahakikishie hizo ni kasi tu za kutaka madaraka. Lakini wananchi wa Kilindi wanajua kazi iliyofanyika. Pongezi kwa Madiwani wote, nampongeza Mkurugenzi wetu Kudra Mwinyimvua pamoja na Watendaji wote. Pamoja na mazingira magumu na miundombinu ambayo bado ni hafifu, lakini inaongezeka kasi kila siku, wanafanya kazi nzuri sana. Naishukuru Serikali kwa miaka mitano hii kwa kweli imeonyesha nia ya dhati ya kutuendeleza wananchi. Kwa Kilindi wameonyesha kwa vitendo. Tumeona barabara zimeongezeka, barabara kuu sasa hivi zinapitika, nyingine zimepandishwa viwango. Barabara za vijiji zinapitika na umeme umefika kwa miezi nane katika Makao Makuu na unaendelea kusambazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Kijiji yamepatikana maji na kwingine kunaendelea kufanyika. Kuhusu kilimo, pembejeo tumejata, vikundi vyta ujarisiamali, zanahati zimeongezeka. Sasa hivi tuna Hospitali ambayo watu Kiteto wataanza kuja na Mvomero, wanakuja pale kutibiwa na tunafanya upasuaji, *Ambulance* zipo, Shule za Sekondari zimeongezeka, Kidato cha Tano na Sita ndiyo tunaendelea sasa hivi na Chuo cha Walimu na Chuo cha Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazingatia kwamba pamoja na miundombinu yetu iliyokuwa hafifu katika Mkoa wa Tanga kwa umahiri wa viongozi wake akiwemo Mbunge wao na ushawishi ambao anao, tumeweza kuongoza katika kufaulu wanafunzi wa Darasa la Saba. Wale wenye umeme, wenye kila kitu tumeweza kuwashinda. Jamani hapa tunastahili pongezi, wananchi wa Kilindi pamoja na Viongozi wao akiwemo Mbunge wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi imeshughulikiwa, Hatimiliki zinatolewa sasa hivi kwa kasi, zile za jadi ili watu woweze kupata haki yao. Kwa hiyo, kwa kweli kwa upande wa Kilindi tunasema sisi tumefanya tathmini na kwa kweli tumeboreka sana. Lakini vile vile Serikali imefanya tathmini, hivi karibuni. Nimshukuru sana Mheshimiwa Celina Kombani na Wizara yake pia, wamefanya tathmini ambazo zimekuwa zikifanyika, tumeendelea kuboreka na safari hii tumepata katika Sekta zote kwa tathmini tuliyopewa juzi asilimia 100, ukiacha sekta moja ambayo tunaelewa kwamba ni kutokana pengine na ushirikishwaji mdogo. Kwa hiyo, nadhani tuna kila haja ya kuwapongeza watu wa Kilindi pamoja na Viongozi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kilindi, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote na Manaibu Waziri kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakitupa. Zile lugha kali kali ambazo mwakilishi wao alikuwa anatumwa kuja kuzisema zilikuwa ili kuhakikisha tu kwamba mambo yanakwenda. Kwa niaba yao, tunaomba pale ambapo tulikwenda mbali sana, basi tunaomba tusamehewe, haikuwa katika nia mbaya, lakini tulikuwa tunataka kupata maendeleo ambayo nimeainisha hapo juu. Nina hakika kwa ushirikiano wa hawa Mawaziri na Ofisi zao tumeweza kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Spika, wewe Naibu Spika, Wenyeviti, Wabunge wenzangu kwa ushirikiano wote ambao tumekuwa nao. Kuna vipindi sikutambua mpinzani wala CCM kwa ushirikiano ambao tuko nao pamoja katika kuangalia tunapata maendeleo ya Watanzania. Yale maisha bora lengo letu ilikuwa tuyapate kwa njia yoyote, kila mtu kwa *style* yake kulingana na itikadi yake. Lakini kimsingi nawashukuru wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimalizie kwa kusema wananchi, huu ni mwaka wa uchaguzi. Naomba tupuuze watu wanaotaka kutugawa kwa udini, ukabila na pesa. Fikiria mwananchi unapewa laki moja leo hutapewa mpaka baada ya miaka mitano, gawanya kwa miaka mitano ni shilingi ngapi, gawanya kwa miezi ile ni ngapi. Kwa kweli naomba muangalie mchague Viongozi bora wenye kutaka maendeleo na wasio na haja ya madaraka. Kuitwa Mheshimiwa kwangu siyo muhimu kama hasa kwangu niliyesimama hapa, ili muweze kufanikiwa. Kwa upande wa Kilindi nina hakika hakuna swali kuhusu kugombea kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kusema, naungana na Mheshimiwa Waziri, bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii ambapo ikipatikana fursa basi woweze kuongezewa kwa sababu majukumu yao ni makubwa na

tunayatambua na hayo maendeleo ya jamii ndiyo ambayo yanaleta kishawishi kwa yote niliyoyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nawashukuruni, asalam aleikum. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Leo umeongea kweli! Maana siku nyingine inakuwaga ugomvi. Leo ustaarabu mtupu!

MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ili kuongea machache kuhusiana na Wizara hii muhimu katika maisha yetu ya kila siku na naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mama Sitta, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mama Lucy Nkya, Katibu Mkuu, Mama Mariam Mwfisi kwa kutuletea hotuba ambayo ni fupi, lakini imefahamika vizuri sana. Nawapongeza sana kwa kazi zao. Lakini vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani - Mama Komu kwa kuwasilisha vizuri na kuandaa kwa niaba yetu hotuba ambayo imeeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa maelezo kidogo kwamba nchi haiwezi kujidhatiti na kutamba kwamba inaendeleza demokrasia na utawala ulio bora ikiwa zaidi ya wananchi wake hawashirikishwi katika maamuzi muhimu yanayohusiana na maisha yao ya kila siku. Kwa hiyo, ni lazima, ili tupige hatua mbele ya kuweza kutamba kwamba Tanzania tunaendelea katika kukuza demokrasia na utawala bora ni kuona kwamba asilimia zaidi ya 50 ya wananchi wake ambao ni wanawake nao wanashirikishwa vilivyo. Sio kwa kupendelewa, lakini ikiwa ni haki yao katika maamuzi muhimu ambayo yanahu maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili naipongeza Serikali hatua ambayo inaendelea nayo ya kutoa nafasi mbalimbali na kuteua Viongozi ambao ndiyo tuko nao kama mfano Wizara hii. Viongozi Wakuu wote ni wenzetu na kwa kweli kazi wanaziweza na hata wale ambao wako kwenye Wizara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tafiti mbalimbali zimefanywa duniani kwamba Taasisi ambazo zinaongozwa na wanawake zinakuwa zina-*perform* vizuri zaidi kimahesabu na kiutendaji kuliko zile zinaongozwa na wanaume. Huo ni ukweli, ipo mifano mingi tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie katika majukumu ya Wizara na niguse ile *bullet* ya nne ambayo inaelezea suala la kuwajengea uwezo wanawake na wanaume ili waweze kushiriki katika ngazi zote za utekelezaji wa miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo na kufaidika sawa katika maendeleo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni muhimu sana na katika hili hatuwezi kulifikia kwa mawazo yangu kama hatujiangalia bajeti kwamba nayo inazingatia jinsia na suala la kuiangalia bajeti hii ambayo imeletwa mbele yetu yenye jumla ya shilingi trilioni 11.1 kwamba imezingatia jinsia au haikuzingatia, sio suala rahisi. Sio suala ambalo mtu

yoyote anaweza akalifanya. Ni suala ambalo linahitaji utaalami. Wenzetu walio wengi katika ma-desk yao ya Taasisi mbalimbali katika Wizara mbalimbali wanaweka Kitengo hasa ambacho kinahakikisha kwamba wakati wa upangaji wa bajeti, bajeti hiyo inazingatia masuala ya jinsia.

Unaweza kuona unaletewa bajeti, mfano pamoja na kwamba tunaambiwa masuala ya jinsia ni *cross cutting issues*, yaani masuala ya mtambuka, lakini bado unaweza ukalitewa hapa bajeti ya Wizara ya Maji ikaonyesha jinsi gani maji yatafika kijijini. Lakini mara nyingi utakuta yanapofika wanaofaidika wa kwanza ni wenye viwanda na ni wenye hela nyingi. Lakini siyo wanawake ambao yatawafikia majumbani kwao na kupunguza ule muda ambao watautumia kwenda kutafuta maji. Bado jamii ya wanawake walio wengi wa vijijini Watanzania wanaishi katika hali ya ugumu wa maisha wa kutafuta nishati na wa kutafuta maji na mambo mengine ambayo ni *basic needs* za kila siku za maisha.

Kwa hiyo, kwa mtazamo wangu, naona bado hatujalifikia l lile lengo la kuona kwamba fedha inayotolewa na Taifa ina uwiano katika usawa kati ya wanayowafikia wanaume na inayowafikia wanawake. Mfano mwengine ni juu ya vitu ambavyo vimesamehewa kodi katika bajeti yetu, safari hii ni vifaa vya kilimo. Zimetajwa pale mashine na vitu mbalimbali. Lakini je, mwanamama aliyeko kijijini yeye atafaidika vipi na hilo? Hilo litawafaidisha wakulima wakubwa ambao wataweza kununua *ma-power tillers* na mambo kama hayo. Mwana mama ambaye bado anategemea kuinamisha mgongo wake na jembe yeye hatafaidika katika kodi hiyo. Kwa hiyo, bado uwiano huu wa kibajeti haujaonekana ukizingatia jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri kwa Wizara kwamba kama Wizara hii, iwe ndiyo kazi yake kuhakikisha kwamba Wizara zote zitakuwa na *desk* ambayo itahakikisha kwamba kabla bajeti haijaletwa humu ndani imevaliwa miwani ya *gender* ili iangaliwe kwamba *gender* imezingatiwa ndani ya bajeti ndiyo iletwe humu ndani na vile vile zichukuliwe jitihada basi za kuwaelimisha Waheshimiwa Wabunge ili nao waweze kuichanganua na kuiona kwamba iko *gender responsive* kama bajeti ili iweze kupitishwa na kama sio hivyo, itakuwa vigumu sana kama Waheshimiwa Wabunge wameelewa kwamba hii bajeti haiko *gender responsive* na ikapitishwa humu ndani, ndipo pale uwiano wa kijinsia hatutaweza kufikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mchache, nihame hapo, nizungumzie suala zima la Maendeleo ya Jamii. Maendeleo ya Jamii inahusisha mambo mengi ndani yake kiasi ambacho unashindwa kujua Wizara hii inalishika lipi na inaliacha lipi. Msemaji wetu wa Kambi ya Upinzani ameweza kuleta ushabihisho kwamba labda Wizara ya Afya iunganishwe na Wizara hii ili masuala ya watoto yawe mazuri. Lakini bado kuna vipengele utaviona, utakuja kusema na Wizara ya Elimu nayo iunganishwe hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalopenda kuzungumzia hapa kwa masikitiko yangu kama mama kwa watoto wetu, bado tuna watoto wengi ambao wana ulemavu wa aina mbalimbali. Watoto hawa wanafikiwaje kuona kwamba haki yao ya kimsingi ile kabisa *very basic need* kwamba wapate elimu watoto hawa wanafikiwa? Mimi huwa

nahuzunishwa sana kuona naangalia sana habari, karibuni niliona mama mmoja akilalamika mtoto wake ana umri wa miaka 10 anasema ana kilo kama 30. Ni mzito kubeba. Alikuwa anambeba akiwa mdogo kumpeleka shule, lakini sasa ame-*give up* kwa sababu hatembei, huyo mtoto ana ulemavu wa miguu. Kwa hiyo, ame-*give up*, mtoto yule yupo nyumbani.

Je, Wizara hii au ni taasisi gani ina *data base* ya kuwatambua watoto walemavu kutoka kule Kijijiini ngazi ya Shina, ili Wizara ya Elimu iweze kuwafikia iwaibue na wasikose hii haki yao ya kielimu? Nilikuwa ninaomba jibu katika hilo na kama bado, basi jitihada inatakiwa kufanywa katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la kusikitisha sana ambalo kila anayesimama hapa wengi tutakuwa tunaliongelea, pamoja na kwamba sheria hii ya mtoto imepitishwa na Kanuni ndio tunatakiwa ziharakishwe zije, lakini bado watoto wa mitaani limekuwa ni tatizo kubwa. Tunasikitishwa sana tunapotembea barabarani, hasa Dar-es-Salaam, utaona watoto wanakosewa, wengine wanagongwa na magari, wengine watoto wakike wanavutwa kwenye magari wanakwenda kunajisiwa kwa sababu wazee wao wanawatumia kama vitega uchumi waende kuomba omba hela ndogo ndogo kwenye magari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine jana pia kwenye habari na katika vipindi vya watoto, mtoto mdogo anasema ye ye baba amemfukuza tu kwenye nyumba, kwa hiyo, yupo mtaani anasafisha vioo vya gari. Mtoto ambaye sasa hivi angekuwa Darasa la Sita au Darasa la Saba, kama akina mama, matumbo yanatuumia!

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Serikali ichukue hatua kali, kwanza kwa wazee wanaowatelekeza watoto hawa, lakini vile vile kwa wale wanaowatumia. Maana wenyewe wanakuwa pembeni, wanawapeleka watoto wadogo sana. Hawa wanawahatarishia maisha yao, lakini pia wanawanyima haki yao, wanawafanya wasiwepo shule ili waweze kupata haki zao za msingi. Lakini la mwisho kabisa, mwisho wa siku wanatujengea jamii ambayo inakuwa ni ngumu kuweza kuleta maendeleo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza na mimi niungane na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuwataka wazazi wenzangu, wanawake na wanaume, lakini zaidi wanawake kwa sababu sisi ndio tunaokaa na watoto muda mrefu ndani ya majumba, turudi kwenye maadili yetu, tulee watoto wetu vizuri. Haitakuwa vyema kuiachia Serikali. Kwa kweli ni jukumu la kila mzazi kuhakikisha kwamba anatekeleza wajibu wake kama mzazi ili tujenge familia ya Watanzania iliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, niwashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Mji Mkongwe, lakini vile vile niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao wao ndio walioniteua kuja hapa kama Mbunge na niwaambie tutaendelea kuwa pamoja katika kazi zetu. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini awali ya yote kwanza naomba kutoa shukrani za pekee kwa

Mheshimiwa Margareth Sitta - Waziri wa Wizara hii, Naibu wake na Katibu Mkuu, ambaye kwa bahati mbaya sana anastaafu na anaicha Wizara hii ikiwa bado ipo kwenye mambo makubwa ya kuweza kusimamiwa ili Wizara iweze kusimama vizuri.

Lakini ninaomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Katibu Mkuu, nikiwa ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, tulifanya naye kazi kwa karibu na alikuwa ni mtu mmoja mwerevu, hodari, msikivu na mara nyingi alikuwa akichukua ushauri wa Kamati. Namtakia ustaafu mwema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kuishukuru sana Wizara kwamba katika kipindi kilichopita, wameleta hapa sheria mbalimbali hasa za kumkomboa mtoto ambazo kwa kweli Watanzania wote tulitoa sana wito kwa Wizara hii kutoa elimu ya kutosha kwa Watanzania ili kuifahamu vyema sheria ya watoto tulioipitisha katika Bunge letu lililopita. Sasa naomba kuingia kwenye masuala ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina majukumu makubwa sana na kwa kweli zipo *NGOs* au mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ambayo yanafanya kazi kwa ufanisi sana. Kwa bahati njema Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii ilibahatika kukutana na Kamati inayoshughulikia Maendeleo ya Jamii ya *South Africa*. Katika maelezo yao, moja, walizungumzia kuhusu masuala ya uendeshaji wa vyama hivi na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ambayo Serikali yao ya Afrika Kusini, wanatoa ruzuku kwa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, jambo ambalo ni la kupigwa mfano.

Namwomba Mheshimiwa Waziri, yupo mwakilishi wa Serikali, Mwakilishi wa Waziri Mkuu, yupo pale, Mawaziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu wapo, na sisi tufike mahali tuone umuhimu wa mashirika haya yasiyokuwa ya kiserikali ambayo yapo mstari wa mbele kuunga juhudzi za Serikali katika kufanikisha masuala ya msingi ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, suala la elimu, kuna mashirika ya kiserikali ambayo yanatoa mchango mkubwa kwenye elimu na mambo mengine muhimu ambayo yapo kwenye kipaumbele cha Serikali. Sasa ninaomba kama Wizara ipeleke mapendekezo Serikalini ili nao waone Serikali yetu inaweza kusaidia vipi mashirika ambayo yanafanya vizuri.

Kuna wasiwasi Watanzania tunayo mashirika mengi ya kwenye *briefcase*, lakini yapo mashirika ambayo kwa kweli yanastahili kupewa pongezi na kuungwa mkono. Naomba kurudia tena kwamba, kwa heshima na taadhima, suala hili naomba kulipeleka Serikalini, waone, waende *South Africa* wakajifunze kwa wenzao wamewezaje? Hatimaye na sisi tuweze kuanza angalau kwa asimilia ndogo, ili tuoneshe mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Idara hii ya Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, pia ina kazi muhimu ya kusimamia mambo ya uendeshaji wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali. Moja ya kazi yake ni kufanya ukaguzi wa mashirika haya yasiyokuwa ya kiserikali. Idara yetu hii ina wafanyakazi wachache sana na mashirika ya Serikali yamesambaa nchi nzima.

Naiomba sana Serikali kuisaidia Wizara hii iweze kufanya kazi kwa ufanisi iiongezee watumishi wawe na watumishi wa kutosha, juhudzi za mashirika yasiyokuwa ya kiserikali mnajua na yapo mashirika ambayo ni ya matapeli. Utapeli huu hatuwezi kuugundua na kuuondoa na kufuta usajili kama hatuna watumishi bora na walio wengi katika Serikali yetu. Naomba kutoa wito kwa Serikali, kuitizama Idara hii kuhusu upande wa wafanyakazi. Lakini pia inalo jukumu la kusimamia na kuona shughuli za taarifa za utunzaji wa mahesabu ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninarudi pale pale. Kazi hii ya kukagua na kuleta taarifa zao za fedha kwa Idara haitakuwa na ufanisi kama pia hatuna wafanyakazi wa kutosha. Kwa hiyo, ninatoa wito kwa Idara kufuatilia kwa karibu sana masuala ya taarifa za utunzaji wa fedha wanazopata *NGOs* hizi na hasa zile ambazo wanapata misaada kutoka nje, ili kuhakikisha kwamba misaada hiyo inawafikia wananchi badala ya kujinufaisha wao wenywewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwezeshaji wa Wizara, naomba kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kiasi fulani. Wizara ilikuwa kwenye hali mbaya sana tulipoingia katika awamu yetu hii 2005/2010, lakini kidogo kidogo wameweza kuongeza juhudzi za kuweza kuiwezesha Wizara, lakini bado kuna tofauti kubwa sana. Ukiilinganisha baina ya Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Wizara nyingine; hivyo kwa sababu hii inawahuishwa Watanzania wote wake kwa waume, maendeleo ya Watanzania wote. Naomba kwa makusudi kabisa Serikali iiangalie Wizara hii kwa jicho la huruma iiongezee, hasa kwenye fungu la maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kwanza kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwanza kwa kuhakikisha Benki ya Wanawake inaanizishwa. Amesimamia vizuri kwa kushirikiana na uongozi wa Wizara, Mheshimiwa Sitta na wasaidizi wake, hatimaye kweli Benki imenza, ahadi yake ameitimiza. (*Makofi*)

Lakini vile vile ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuhakikisha kwamba angalau kila mwaka kuiwezesha Wizara kupata shilingi bilioni mbili kuiwezesha Benki ya wanawake kuongeza mtaji wake wa kuiendesha. Jamani wanawake mnasema mkiwezeshwa mnaweza, sasa Mheshimiwa Rais amewawezesha, tuone kweli kama mnaweza! Mwoneshe umma wa Watanzania kuwa kweli mkiwezeshwa mnaweza. Mtihani wenu mkubwa sasa upo kwenye Benki. Je, tutanufaika na hii benki? Akina baba msitubague, tumo humo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningombaa kutoa wito kwa benki hii ya wanawake, kwa kweli kwa hapa ilipoanza inafanya kazi nzuri. Nimetembelea mara nyingi pale kupata taarifa hizi na zile na pia kuitia Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii ya Bunge, ninazo taarifa za kutosha kuhusu benki hii.

Lakini ninaomba kutoa wito kama Kamati ilivyosema kwamba sasa tokeni pale mlipo anzisheni vituo mbalimbali kwenye Mikoa ili kweli wanawake wawezeshwe. Muwawezeshe akina mama waweze kufungua miradi midogo midogo huko Mikoani.

Tunajua uwezo wa kufungua matawi kwa ajili ya benki hii hakuna, lakini kwa kufungua vituo angalau kuratibu tu shughuli za benki, inawezekana. Ninaomba hilo mlisimamie kwa juhudzi zenu ili akina mama wa Tanzania waone kweli Benki yao inawawezesha na imewafikia huko waliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la ajira ya watoto. Tuna tatizo kubwa hasa kwenye maeneo ya uvuvi, watoto wengi wanatumbukia katika sekta hii kwa kutumikishwa wakiwa na umri mdogo kwenye sekta ya uvuvi. Naomba Wizara jikiteni, nendeni pale feri mkakusanye *data* ili baadaye watoto hawa na maeneo mengine ya fukwe, kwenye minada ya samaki, pwani na kwenye maziwa, hebu zungukeni Tanzania nzima hii, mtasikitika na mtaona hali hii ni mbaya na ya kusikitisha.

Naomba sana kutoa wito kwa Wizara kuliangalia hili ili watoto wetu wa Tanzania waweze kusoma na nina hakika wakisoma na wakiwezesha vizuri, ndio watakaokuwa viongozi wa kesho watakaokuja kusimama kwenye Bunge hili ili kuiongoza nchi yetu na familia zetu zinazokuja hapo usoni kwa Watanzania wajao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na muda wangu kengele ya kwanza imeshalia. Sipendi nigongewe ya pili, naomba kuunga mkono hoja na ninawatakia kila la heri Wizara hii katika uendeshaji wa Ofisi yao. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. HAROUB S. MASOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi kwa sababu sasa hivi ndio nafasi yangu mimi kama Mbunge, pale ilikuwa ni nafasi ya Kamati. Nina machache ya kuzungumza kwa kuboresha baadhi ya mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Mimi nimekaa katika Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwa miaka 15, ninaijua hii Wizara huko inakotoka kuanzia mwaka 1995. Najua namna ya wafanyakazi na walivyokuwa wakifanya kazi wakati huo, lakini Wizara hii imebadilika kweli kweli. Tena tunawapongeza sana. Sasa hivi wafanyakazi wote ni kitu kimoja na pamoja na uongozi wa juu, na ndio maana ukaona mambo yao yanakwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nisije nikasahau, mwisho, mimi ninaunga mkono hoja asilimia mia moja kabisa na ninamtakia heri Mheshimiwa Waziri na Naibu katika mchakato wa kugombea Ubunge wakati utakapofika. Nina imani wananchi hawatakuwa wachoyo hata siku moja kuwanyima kura hawa watu wawili kwani ni watendaji wazuri kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mingi, Kamati ikisaidiana na Wizara imekuwa ikipiga kelele kuhusu bajeti ndogo. Wizara hii ndio kioo cha Serikali, bila Wizara hii hapatakuwa na maendeleo kabisa. Tumeona kazi nzuri ambazo zinafanywa na Mawaziri wanawake, Watendaji Wakuu wanawake, Makatibu Wakuu na Viongozi wote naona ni wa wanawake tu. Kwanza ni waaminifu na waadilifu, haki yao wapewe.

Matokeo madogo madogo yanayotokea ya ubadhirifu, ya rushwa na nini, wanawake wanasema sisi hatumo.

Ninawaomba waendelee na msimamo wao huo huo, ni afadhali kile kidogo nilichokipata kuliko kutaka kucheka kwa nguvu zote, Mungu atawasaidia na kuna siku Serikali itakuoneni, kama ambavyo baadhi yenu mnaonekana hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni nasaha zangu kwa Wabunge hawa wanawake waliopo wa Majimbo na wa Viti Maalum pamoja na wale wengine ambao wana nia.

Ninawaomba sana msiogope kugombea nafasi hizi. Nafasi hizi ni za Ubunge, hazikutamkwa kwamba Mbunge mwanamke au Mbunge mwanaume. Ondoeni hofu, msiweke mashaka, lakini kitu muhimu ni kwamba kuna tabia, maana mimi ni mkweli na muwazi. Kuna baadhi ya wakati akina mama wenyewe mnakorogana.

Hebu kuweni kitu kimoja, mpendane, mtazame, mtaingia kwa kishindo hapa, na inshallah mimi baada ya Uchaguzi Mkuu, ingawa ninapumzika lakini ninataka kuja kuona idadi ya wanawake Bungeni. Nitamwomba Spika aniruhusu niingie ndani, nikae niwaoneni. Sitaona raha kuona mwanamke yeote ambaye yumo humu ndani sasa hivi hajarudi hapa. Mimi mizimu yangu yote na dua zangu zote, ninawaombeeni na inshallah Mwenyezi Mungu ataipokea dua yangu hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyozungumza kabla, mimi nimeingia mwaka 1995 hapa. Nilipoingia kuna baadhi ya taasisi au mitandao ile ya wanaharakati, walikuwa wakionekana ni maadui kweli kweli na akina mama. Matokeo yake mitandao hii ndio iliyosaidia wingi wa Wabunge wanawake ndani ya Bunge hili, Mheshimiwa Anna Abdallah anajua, Mheshimiwa Anna Makinda anajua. Zikiwemo hizi chache ambazo nitazitaja *TGNP, TAWLA, FAWETA, MEWATA, TAMWA na WAMA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi hizi au mitandao hii wewe ni shuhuda, imesaidia kweli kweli katika harakati za kijinsia Bungeni na nje ya Bunge. Mpaka hii leo na miaka yote hii wanashirikiana sana na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, na ninawaomba, na ninatamka kuwaambia kwa sababu hawa nimekaa nao miaka 15, naomba kutamka hasa kwamba sio jambo la kawaida, lakini mimi ninasema ninawaaga rasmi na wao kwa sababu wametuhudumia vizuri, mimi na Kamati yangu muda wote huo, *inshallah*, Mwenyezi Mungu awape uwezo wa kuwasaidia zaidi na kuwapa uwezo zaidi akina mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitambulishwa hapa asubuhi, kuna wageni walikuwepo katika Ukumbi wa Spika pale juu, wanatoka nchi mbalimbali. Ni Watanzania, lakini kwa sababu wanajua leo ni hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, wanakuja kwa sababu na wao ni wanaharakati, wanaumwa na akina mama wenzao. Wametoka walikotoka, wamekuja hapa kushuhudia ninyi wenyewe mnasema nini. Kwa hiyo, tukivurugana, tutawapa picha mbaya wale. Jana nimeonana nao mimi, waliokuja ni wengi, pamoja na wao ninadhani mmewaona Wawakilishi wa Mabalozi waliokuja hapa.

Lakini vile vile kwa sababu wanakereketwa na mambo haya ya akina mama, wameona ni bora waje.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nilipotoka hapo nje, kuna mtu alinihoji, umeshinikizwa? Kustaafu nisigombee, yale ni maamuzi yangu kama Haroub, niliyeshauriana naye ni mke wangu ambaye amenilea, kama alivyosema Mheshimiwa Spika, kwa muda wa miaka 15, nikapata uwezo wa kuendesha vizuri kazi za Ubunge wangu.

Kwa hiyo, kuna mahali kwa kazi yoyote ile, useme hapa ninamuachia mwenzangu. Nami nilitamka hapa siku moja, nitafurahi sana kama atajitokeza mwanamke ndani ya Jimbo langu na bado kauli yangu iko pale pale kwamba, kama kuna wanawake wanataka kugombea huko na uwezo wanao, mimi nitaunga mkono na kampeni nitasaidia kwa hali na mali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu, siku niliyokwenda kuaga Kamati yangu ya Siasa ya Wilaya, niliwaambia mimi ni binadamu, mimi ni kiumbe, inawezekana kuna watu wanasema sijafanya kitu, kuna watu wanasema Bungeni sifanyi kitu, lakini ni jambo ambalo mtanikumbuka maisha milele.

Niliwaambia kuna mradi hapo, bahati nzuri Wizara ya Ardhi wametoa kiwanja, kimeshapimwa na hatimiliki ipo tayari ambayo kwa njia ya pekee, ni lazima nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mkuu wa Mkoa wangu, Ndugu Mustafa Ibrahim pamoa na wafanyakazi wa Idara ya Ardhi, kwa juhudzi zao mpaka wakanipatia eneo ambalo limenitosheleza. Kuna *project* yangu kubwa inaanza mwezi huu ambayo ina-cost shilingi 3.5 bilioni. Niliwaambia Wanasiasa wenzangu, hiyo ndiyo zawadi kwa Chama changu ingawa ni mradi wa shule, hospitali, kituo cha watoto yatima 200 na mambo mengine, lakini kwa sababu nilikuwa natekeleza Ilani ya Uchaguzi, nikasema itakuwa si sahihi nikifanya mambo madogo madogo kama shule, Misikiti na mambo mengine lakini niweke kitu ambacho kitaleta kumbukumbu ya milele. Kumbukumbu ya milele ni kitu ambacho kitasaidia zaidi yatima 200, wakihudumiwa pale milele, ina maana ile ni faraja hata nitakopofariki mimi kwani mimi ni binadamu ninaweza kufariki, nadhani lile jambo zuri litakalofanyika pale ndiyo litanisababishia mimi nipepewe kule peponi kama anavyonipepea mke wangu ambaye amesababisha leo nikatoa hotuba hapa na sasa hivi nachangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri na nitashirikiana na Wajumbe wangu isipokuwa nimewaambia sana akina Mheshimiwa Bujiku Sakila kwamba sitakuwa radhi hata siku moja kumuona Mjumbe yejote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii anarejea Bungeni anaikana Kamati hii, nitamlaani kwa nguvu zote zile, wamsaidie Waziri yejote wa Maendeleo ya Jamii atakayekuwepo wakati huo na *Inshallah*, atakuwa huyu huyu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya machache, naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, hatukujua kama na wewe unastaafu na sisi tunakutakia kustaaafu kwema kabisa kwa moyo wako uliouweka wa kuwaendeleza akina mama kwa kila hali mpaka siku nyingine wakawa wanasema una matatizo lakini wewe mwenyewe msimamo wako ukabakia palepale mpaka kesho, tunakutakia kheri sana. (*Makofi*)

Sasa nimwite Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika halafu Mheshimiwa Florence E. Kyendesya ajiandae na Mheshimiwa Halima J. Mdee ajiandae.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na leo hii kuweza kusimama kuchangia hotuba hii. La pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Prof. Ibrahim Lipumba, kwa kuchaguliwa kuwa mgombea pekee wa Chama cha *CUF*, kwa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano na pili nampongeza Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa Serikali ya Zanzibar kwa tiketi ya *CUF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naanza kuchangia kwenye Wizara lakini kwanza nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika nchi yetu. Kwa kweli, Wizara hii ni Wizara kubwa, mtambuka na ambayo huwa inabeba jinsia zote na kwamba Wizara zote zinaingia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, hii Wizara kila siku tunaipigia kelele kwamba inapewa bajeti ndogo. Kwa hiyo, tunaomba bajeti iangaliwe na iongezwe kwa sababu ina kazi kubwa sana. Wanawake kama tunavyojua ni wengi zaidi. Kwa hiyo, tunaomba bajeti iangaliwe vizuri na iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakuja katika uzalilishaji wa watoto au wanawake. Hivi karibuni hata jana kwenye vyombo vyahabari, tumesikia kuwa Morogoro wamebakwa watoto wasiopungua 83 kwa kipindi cha kuanzia Januari mpaka Aprili, hali hii inasikitisha. Watoto hawa waliobakwa, kwa kweli ni watoto wetu na wanazalilishwa vibaya sana. Tunaomba hawa watakaobainika kutenda tendo hili wachukuliwe hatua mara moja na waadhibiwe. Tunatoa wito huo, kwa Walimu na wazazi na kwamba wazazi lazima na sisi tushirikiane na Walimu na Walezi kwani wote ni watoto wetu. Kwa hiyo, tulishughulikie suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hao watoto pale wanapokamatwa baada ya kubainika kuwa wamebakwa, wapelekwe Vituo vyahabari ili waangaliwe kama wameathirika kutokana na janga la UKIMWI na vilevile wapatiwe tiba za kurefusha maisha yao. Lakini pia wabakaji wajulikane, nani wamewabebesha mimba na mara moja

wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria hata akiwa ni Mwalimu ndiye amefanya hayo, afukuzwe kazi na baadaye apelekwe kwenye vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kusikitisha jana na hata leo asubuhi, tumesikia kuna Askari mmoja wa kike alipewa dhamana ya kuongoza msafara wa Rais na akaupotosha, kwa kweli alifanya kosa na ilikuwa ni wajibu wake kuchukuliwa hatua, kupelekwa kituoni na kuhojiwa. Lakini hata hivyo, la kusikitisha Askari huyo alijiua mwenyewe kwa kujipiga risasi. Sasa nauliza, yejote anayeperekwa Mahabusu, tunaelewa kuwa ananyang'anywa kila kitu alichonacho kama ni silaha, au mkanda wa kufungia nguo yake pia ananyang'anywa na vinahifadhiwa, itakuwaje Askari huyu aachiwe silaha ajiue mwenyewe? Dhamana yake ni nini na Askari aliyejukwepo ni mzembe, kusema kweli hata hatumuelewi. Kwa hiyo, Tunaiomba Serikali ichukue hatua mara moja ya kumkamata Askari huyo na kumhoji ni kwa nini mwanamke huyo akawekwa ndani na ikampeleke kujiu? Kwa hiyo, akamatwe na kupelekwa kwenye kituo na ufanywe uchunguzi zaidi kuhusu suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naja kwenye uuaji. Watoto kwa kweli wanauawa na wananyanyaswa hasa sehemu za Mbeya, watoto kuanzia umri wa miaka mitatu mpaka sita, wala hawana hatia yoyote kwa imani ya kishirikina eti kutafuta utajiri. Kwanza, niwaulize Watanzania, ni nani anayepata utajiri kwa kumuua Albino? Au ni nani anayepata utajiri kwa kumuua mtoto asiyé na hatia? Hili jambo lichunguzwe na atakayebainika basi hata auawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye uzalilishaji wa wanawake, kama walivyosema wenzangu hapa tunazalilishwa, na tunazalilishwa hata na waume zetu, wanaume wanawaua wake zao na baadaye hujiua wao. Lakini hujiua kwa kuogopa kupewa adhabu lakini kosa tayari ameshalitenda la kumuua mwenzake. Kwa hiyo, inafika wakati hata mwanamke mwenyewe ndani ya nyumba anaogopa kujibizana na mumewe kwa sababu anaona akijibizana siku nyingine ni mtihani kwake. Kwa hiyo, naomba wanaume wakae vizuri na wake zao, wasiwanyanyase na kuwaua. Hili si jambo zuri kwa maisha ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nizungumzie kuhusu wanawake wajawazito, wanawake wajawazito kwa kweli wengi wanapoteza maisha hasa vijijiini kutokana na miundombinu ya usafiri, vifaa vya kusafiria, kama mzazi yuko mbali na Zahanati, atajifungulia njiani au achukuliwe na balskeli hata akifika kwenye Zahanati, mzazi anakuwa amejifungulia njiani au amefariki njiani. Kwa hiyo, Tunaiomba Wizara ya Afya ifanye jitihada na ipeleke vitendea kazi hasa usafiri ili wajawazito waweze kufika haraka kwenye vituo vya kujifungulia. Vilevile ni upungufu wa Madaktari, nao pia huleta usumbufu kwa sababu hivi karibuni tulishuhudia kwenye vyombo vya habari kuna mwanamke alijifungulia barabarani, hii inaleta usumbufu. Kwa hiyo, ni lazima Wizara iangalie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo sina mengi ya kuchangia isipokuwa ni hayo na nasema ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na kwa vyovyote vile ameunga mkono hoja hii maana mazungumzo yake mazuri yanaonyesha kabisa kwamba anaunga mkono. (*Makofi*)

Sasa nimwite Mheshimiwa Florence Kyendesya halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Halima J. Mdee, kutokana na muda huu nafikiri na Mheshimiwa Muhammad Sanya tutamfikia.

MHE. FLORENCE E. KYENDESYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu ili nami niweze kuchangia kwa ufupi hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza sana Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margret S. Sitta, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya na Watendaji wake wote kiujumla, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ya Maendeleo ya Jamii, kwa hiyo, nazungumza kama mjumbe ambaye mengi nimejifunza na nimeyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii, kwa kweli inaonewa sana, sijui niseme inaonewa au inadharauliwa kwa sababu mara nyingi watu husema ni Wizara ya Wanawake lakini siyo Wizara ya Wanawake, ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto yaani jinsia zote. Nasema inaonewa kutokana na bajeti finyu ambayo inapewa. Katika bajeti za nyuma yaani mwaka 2007/2008 na 2008/2009 mpaka sasa tunapiga kelele hali hiyohiyo ya kupewa bajeti ndogo inaendelea. Hii Wizara mimi nasema mara nyingi ni Wizara Mama yaani ni Wizara nyeti kwa sababu inachukua Wizara nyingi, mambo mengi kama ya elimu, afya na miundombinu lakini bajeti yake ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, vyuo hivi ndivyo hasa vinavyofundisha wanafunzi amba watakuwa ndiyo Maafisa Maendeleo ya Jamii kwani Maendeleo ya Jamii yanaanza ndani ya familia na kaya hadi Taifa, ndiyo maendeleo ya jamii yenyewe. Lakini hivi Vyuo kwa kweli mara nyingi vinafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijikite kidogo kwenye Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Uyole, Mkoani Mbeya. Mambo mengi wameongelea wenzangu kuhusu Benki ya Wanawake lakini mimi nitaongelea kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Uyole kinafanya kazi katika mazingira magumu sana. Chuo hiki kwanza hakina maji, Chuo kilikuwa na wanafunzi 400, sasa hivi kimefikia wanafunzi 800, Chuo kinategemea maji ya kutoka katika Chuo cha Kilimo cha Uyole, Chuo hicho nacho kitahitaji maji kwa sababu maji yanayopatikana kwenye Chuo cha Kilimo cha Uyole huwa wanafanya majoribio, kwa hiyo, Chuo cha Maendeleo ya Jamii huwa kinakosa maji. Afadhali wakati wa masika huwa wanatumia maji ya mvua, lakini wakati wa kiangazi kuanzia sasa na kuendelea kwa kweli kunakuwa hakuna maji na maji ni uhai, Chuo chenye wanafunzi 800 kinakosa maji? Mimi ninashauri kwa kweli Serikali

ikione hicho Chuo na itenge bajeti ili kichimbiwe kisima kirefu, kijitegemee kwa maji. Huo ulikuwa ni ushauri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni usafiri kwenye Chuo hicho, Chuo chenyé wanafunzi 800 hakina gari, balskeli wala mkokoteni. Gari linalofanya kazi pale ni gari binafsi la Mkuu wa Chuo, ambaye ndio amekuwa dereva na gari lake limekuwa *Ambulance*. Usiku kunapotokea matatizo ya wanafunzi ya ugonjwa wakipiga simu kutafuta *tax* wale madereva wa *tax* wanakataa, wanaogopa kutokana na hali ya uhalifu iliyopo, hivi sasa huwa hawatoi *tax* zao, Mkuu wa Chuo ndiye anaacha usingizi, anabeba wanafunzi na kuwapeleka hospitali maana ni watoto wake na tena kwa hela yake mwenyewe na siyo hela ya Serikali. Wizara ndiyo tusema ina Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, huyu Mkuu wa Chuo kubebeshwa mzigo huo atawenza? Ana mshahara kiasi gani ahudumie familia yake na wanafunzi kwa hela yake mfukoni? Mimi ninashauri kwa kweli Serikali ikione hicho Chuo, itenge angalau bajeti kidogo iwatafutie usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kidogo kuhusu watoto yatima, wenzangu waliotangulia wameongelea. Hawa watoto yatima ni wetu, mara nyingi utakuta *NGOs* zinazohudumia watoto yatima, lakini wana *base* kwamba wanahudumia watoto yatima ambao wazazi wao wamefariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Nawapongeza na kuwashukuru kwa huruma hiyo ya kuwashudumia watoto yatima waliofiwa na wazazi wao waliokufa kwa ugonjwa wa UKIMWI. Lakini mimi nadhani mtoto yatima ni yatima hata wale ambao wazazi wao wamefariki kwa magonjwa mengine siyo UKIMWI nao ni yatima, sasa hawa tunamuachia nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi au jana timesikia huko Dar es Salaam, Baba kamua mke wake kwa kumchoma kisu na yeye amejichoma kisu amekufa, si wameacha watoto ambao ni yatima? Sasa tunaposema watoto yatima waliofiwa na wazazi wao kutokana na ugonjwa wa UKIMWI, hao wengine je? Mimi naona watoto yatima ni yatima, haya mashirika tuyaangalie tuyatupie macho kwa sababu huko naona kuna hela. Mashirika mengi ya kimataifa yanatoa misaada kwa watoto yatima ambao wazazi wao wamefariki kwa ugonjwa wa UKIMWI, kwa hiyo, utakuta kunakuwa na pesa. Sasa wanasema sisi tunahudumia watoto yatima waliofiwa na wazazi wao kutokana na ugonjwa wa UKIMWI, sasa hao wengine waende wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri na kupendekeza kwamba watoto yatima ni yatima *whether* ni kwa ajali au kwa magonjwa mengine, hii ya kusema wenye UKIMWI kwanza *psychologically* hawa watoto tukisema wazazi wao wamekuwa kwa ugonjwa wa UKIMWI, wanavyozidi kukua, wanakua wakijua kwamba baba yangu au mama yangu alikufa kwa ugonjwa wa UKIMWI, kidogo inawasumbua kiakili. Mimi naomba tuseme tu watoto yatima bila kutaja kwamba wazazi wao wamekuwa kwa ugonjwa UKIMWI, sisi wote ni wazazi hasa akina mama linatumua sana kwa sababu hawa watoto wametoka kwenye matumbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa kifupi yalikuwa ni hayo lakini naiombea kheri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, kwa kweli inafanya kazi nzuri, iendelee kufanya kazi lakini tuongeze bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, sasa nimwite Mheshimiwa Halima J. Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia japo kwa uchache Wizara yetu hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sijaanza, nichukue fursa hii kupongeza kwa dhati kabisa baadhi ya wanawake wa Tanzania hasa wewe mwenyewe binafsi Naibu Spika pamoja na Mama yangu, Mheshimiwa Anna Abdallah pamoja na wengine kwa sababu huwezi kumtaja kila mtu, lakini unataja wale ambao unadhani wame-*play role* kubwa sana katika kuhakikisha kwamba wanawake wa Kitanzania wanapata nafasi za uongozi. Kwa hiyo, mimi nawapongeza sana na mkae mkijua kwamba mko ndani ya moyo wangu hata kama tuko kwenye vyama tofauti vyaa siasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Haroub Masoud, ana miaka 15 Bungeni, lakini katika kipindi cha miaka mitano niliyokaa hapa, ninaweza kusema ni Mbunge pekee mwenye jinsia ya kiume ambaye amekuwa mstari wa mbele sana kupigania haki za wanawake. Nampongeza na kumtakia kila la kheri. Ninaamini kile unachokipigania na ambacho wamekipigania Mama zangu hapa, kitaendelea kufanikiwa kwa ufasaha sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kupongeza kwa hatua iliyochukuliwa hasa katika kuongeza nafasi za wanawake katika vyombo vyaa maamuzi, katika ngazi ya Majaji, Wakurugenzi, Wabunge, Madiwani, Serikali za Mitaa na kadhalika, inatia matumaini. Lakini tuna changamoto kubwa sana ya kupeleka matumaini haya katika ngazi za maamuzi kwa wanawake maskini kule chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyochangia hotuba ya Waziri Mkuu, nilizungumza kwa kina jinsi ambavyo katika kipindi cha miaka mitano, hali ya mwanamke wa Tanzania kikipato ama kimapato imekuwa ikishuka kwa kasi sana. Sasa nadhani tuna changamoto kama Serikali kuangalia haya mafanikio japo kwa uchache ambayo tumeyapata katika ngazi za juu za kimaamuzi tunayapeleka kule chini kwa hawa wanawake maskini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, wakati anazungumza hapa, amezungumzia suala zima la *gender budgeting* ama bajeti ambayo inatazama au inaangalia mtazamo wa kijinsia. Mimi nadhani hili suala ni muhimu sana Serikali ikalizingatia hasa ukizingatia kwamba Tanzania kama nchi ilisharidhia na kuonyesha kwamba ina dhamira ya kuhakikisha kwamba bajeti yake inaangalia jinsia zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumzia bajeti kuangalia jinsia zote mbili siyo kwamba tunataka kutenga jinsia moja, tunachosema hapa ni lazima bajeti tunazozipitisha kila mwaka, Mawaziri wakija kutuletea bajeti nyingine, watuonyeshe ni kwa namna gani

bajeti zilizopita zimeweza kunyanya maisha ya mwanamke maskini wa Kitanzania. Hizo taarifa ndizo tunazozitaka na ni kitu kirahisi sana kama tukiamua kupanga na kuangalia ni kwa namna gani tunamsaidia huyu mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumza hili kwa sababu ukiangalia mfano mdogo tu wa huu Mfuko wa JK, kwa taarifa ambayo *BOT* ilitoa kwenye Kamati yetu mwaka 2008 katika zile awamu za mwanzo za mkopo, katika wakopeshwaji karibia 48,000 wanawake ni 13,000 tu. Sasa katika mazingira kama haya, hali ikoje kwa huyu mwanamke kule chini? Huo ni mfano mmoja tu. Sasa nina uhakika mfano kama huu pia upo katika sekta nyingine. Kwa hiyo basi, kama tuna dhamira ya kuboresha kipato cha mwanamke na kuhakikisha kwamba vipato vya Tanzania baina ya jinsia mbili vinakwenda sambamba lazima kwenye taarifa zetu za mwaka, tuonyeshe kwa vitendo kwa kuangalia ni kwa namna gani huyu mwanamke tunamsaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nikija kwenye suala zima la haki za wanawake na watoto lakini na wanaume pia, tumepitisha sheria mbalimbali ambazo kwa namna moja ama nyingine zimeboresha mustakabali wa mwanamke. Lakini kuna sheria nyingine ni kandamizi ambazo Kituo cha Kurekebisha Sheria yaani hii Tume ya Kurekebisha Sheria, imetoa mapendekezo Serikalini toka mwaka 1994, miaka 15 mapendekezo yameletwa yako *store* hayafanyiwi kazi. Sheria mojawapo ni hii ya Tangazo la Sheria za Kimila, namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nilimuomba anipe tafrisi sahihi kwa Kiswahili maana ningeweza kuiweka kwa Kiswahili halafu nikaharibu, ni Tangazo la Sheria za Kimila mwaka 1963, sheria hii inamnyima kabisa Mjane haki ya kumiliki ardhi. Ni kweli Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 inasema kwamba ni haki kwa jinsia zote kumiliki ardhi lakini sheria hii inamnyima mjane haki ya kurithi ardhi kwa sababu kuna tofauti kati ya kumiliki na kurithi, lakini hii inamnyima. Sasa sheria kama hizi ndiyo kandamizi huko vijijini, wanawake maskini wanaathirika sana na sheria hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Sheria nyingine ya Uraia, Sheria ya Uraia, ina ubaguzi ulio dhahiri. Halima leo akiolewa na mwanaume wa nje ya nchi, aandike watoto wake hadi waanze michakato ya kuomba uraia, wakati kwa mwanaume ni *situation* tofauti. Huu ni ubaguzi ulio dhahiri, kwa nini tuisifanyie marekebisho? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Sheria ya Ndoa, hii imezungumzwa na kuzungumzwa, sijui hata kuna mdudu gani humo ndani, kwani inaruhusu watoto wadogo kuolewa. Cha kusikitisha mwaka 2007, Mheshimiwa Mary Nagu, alivyokuwa Waziri wa Sheria, aliji-*commit* kwamba tutaleta mabadiliko ya Sheria ya Ndoa lakini hakuna kilichofanyika na sasa hivi ni mwaka 2010 kama akirudi *inshallah* na asiporudi ndiyo hivyo mambo yamekwenda. Akaja Mheshimiwa Sophia Simba, akipitisha bajeti mwaka 2008 wakati alivyokuwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya jinsia, akaji-*commit* kwamba tutaleta mabadiliko ya hii Sheria ya Ndoa ambayo ina vipengele vinavyomkandamiza mwanamke na vinavyomkwaza mtoto wa kike mdogo lakini hakuna

kilicholetwa sasa hivi ni mwaka 2010. Nataka Mheshimiwa Waziri atusaidie, hivi vitu tunavittatuaje? Mimi siamini kabisa kwa sababu kuna *excuse* kwamba sijui dini na kadhalika lakini mimi siamini kama kuna dini kandamizi, mimi naamini kabisa kwamba hamjafanya kazi ya kutosha kutafuta *audience* na viongozi wa dini kuangalia ni kwa namna gani tunamlinda huyu mtoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo, kwenye kitabu hapa inaonyeshwa kuna Halmashauri ambazo zimepewa mikopo, sasa nikiangalia hapa Manispaa ya Konondoni yaani toka utawala wa JK 2006-2010 hakuna kitu, kuna *dash* hapa. Sasa nataka Mheshimiwa Mama Sitta, anisaidie kwa sababu kuna Majimbo matatu yaani Kawe, Kinondoni na Ubungo na hapa Manispaa yetu hajapewa hela. Sasa mtuambie kama hazipo basi *at least* kwenye bajeti ya mwaka huu mtatufikiria na tufanyaje, inawezekana labda kuna uzembe wa aina fulani katika kutuma maombi. Kwa hiyo, nataka kujuu, kuna michakato gani inafanyika ili kuweza kutusaidia ili na sisi wanawake wetu wapate mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Hiyo Kawe imekoma mwaka huu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Ibrahim Muhammad Sanya, ndiye msemaji wetu wa mwisho asubuhi hii.

MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitakuwa na mengi sana isipokuwa nataka nielezee kitu kidogo tu kuhusu madhila na dhiki walizonazo mama, dada na watoto wetu Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dini na vitabu vyote alivyoteremsha mwenyewe Mwenyezi Mungu, vimempa heshima kubwa sana mwanamke na kama laiti tungkuwa tunafuata hivyo vitabu vya dini ambavyo tunaviamini basi mwanamke angekuwa na heshima kubwa sana duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwanamke siyo wa Tanzania tu lakini dunia nzima mwanamke ndiye anayedhalilika, ni tabia mbovu, chafu na isiyokubalika katika jamii yoyote duniani. Wanawake ndiyo wanaozalisha chakula tukala sisi Watanzania, vijijini unapokwenda mwanamke ndiye mkulima, analima anapalilia, anapanda, anavuna na hata barabarani unapopita yeze ndiye anayeuzza mazao. Chakula hicho hicho anachokilima, akakivuna hicho hicho akakipike tena kuni na maji akatafute yeze kama kilomita mbili au tatu lakini nenda kamuangalie mwanamke wa kijijini maisha anayoishi, yanaskitisha sana. Hata Mheshimiwa Halima Mdee alipozungumza hapa, kuna hizo fedha za Mheshimiwa JK waliopata ni 13,000, fikiria kama fedha hizo zimekwenda kweli vijijini, zitakuwa zimefika katika mikono ya watu wa kati wenye wastani wa kipato, lakini unapokwenda kijiji sijui kama zimefika na yule ndiye aliyetakiwa kuangaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utachukua wiki moja ukasoma magazeti yote kuanzia Jumamosi mpaka Ijumaa basi lazima kutakuwa na kesi moja, mbili au tatu za unyanyasaji wa mwanamke. Mimi wiki mbili za nyuma au moja hivi, kuna mama amefiwa na mumewe katika harakati zao za kumuweka katika ujane alinyolewa nywele, walitoka vijana wakaenda kumcharaza mapanga wakamuua palepale, magazeti yameripoti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mama amekaa na mumewe nyumbani, kaja bwana akagonga mlango na kuomba maji, mama anakwenda kuchukua maji anamletea yule bwana mlangoni, kampiga mchi wa kichwa, kamuua palepale. Mumewe anasikia kelele moja, anatoka anakuta mke wake ameshakufa. Tunakwenda wapi? Kitu gani kinafanya sisi tuwadhalilishe wanawake kiasi hiki? Hawana haki ya kuishi? Wao ndiyo wazee wetu waliotuzaa na kutulea, wanatupikia, wanatulisha, wanalima na kufanya kazi zote ngumu za kutusaidia sisi akina baba lakini bado udhalilishaji ni wa hali ya juu kabisa. Sikwambii tena ya vikongwe na Albino sijui wamekosa nini jamani? Hivi nani katika sisi Wabunge anapendelea mzee wake kafika miaka mia akamuue mzee huyo, Kwa nini tukawaue wa wenzetu? Kwa nini udhalilishaji huu uwe kwa wanawake tu? Wamekosa nini hawa wanawake ambao wamebeba dhima kubwa ya kulilisha Taifa hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema kwamba wanawake wapewe nafasi nyingi sana za uongozi ili wawatetee wanawake wenzao, siyo Bungeni tu na ngazi nyingine za uongozi. Tunaona Mawaziri Wanawake na Naibu Spika wanavyofanya kazi katika Bunge letu na kwingine kote wanafanya hivyo hivyo wala tusiogope tukasema kwamba nchi itaendeshwa na wanawake lakini kama wana uwezo waache waendeshe, lakini wapewe nafasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi *NGOs* zihakikiwe ili zile ambazo zinafanya kazi ziongezewe nguvu na misaada ili zifanye kazi na zile za wajanja zifutwe ili watafutwe watu ambao ni waaminifu kwa ajili ya kuwatumikia wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii bajeti ni ndogo sana, bajeti ya maendeleo shilingi bilioni nane, milioni mia mbili sabini na nane, *is a joke* kwa nchi kama yetu. Bajeti ya maendeleo kwa wanawake iwe kubwa kweli kweli kama bajeti nyingine ili tuwaondolee dhiki hawa watoto na akina mama na ni lazima tuwe na mikakati ya kuwaelimisha. Leo kuna nchi nyingine wanawake wanaanza kufundishwa Judo na Karate kwa sababu ya kukumbana na vijana wahuni wanaotaka kuwafanya uhuni, wamechoka kufanyiwa uhuni wanawake. Kuna kila njia ambazo wanawake sasa wanajihami, sasa na sisi tuweke programme.

Mheshimiwa Naibu Spika, China wakati wa Mao Thetung, kulikuwa na *Mass Education* walikuwa wanatumia nini? Walikuwa wanatumia *screen* kubwa katika vijiji vyao ambavyo wenyewe walikuwa wakiviita *Communes*. Walikuwa wanapeleka *Screen* kule wanawaelimisha wanawake haki zao, sisi leo tunasema tuna televisheni *TBC* na redio lakini vijijini hazifiki kwa sababu hakuna umeme wanaomilika wakawenza kuangalia televisheni, sasa cha kufanya ni nini na tufungueni kiwanda kidogo cha kutengeneza redio ili wananchi wa vijijini wapate redio na kuwe na programme maalum

za usiku kuanzia saa mbili na nusu mpaka saa tatu na nusu waelimishwe haki zao, waache kunyanyaswa na waume zao waliokuwa walevi na waache kunyanyaswa na waume zao ambao hawafanyi kazi. Mtu anakwenda kilabuni analewa, akishalewa anakuja nyumbani anamwambia mama nitengenezee ugali, akichelewa kidogo anampiga, huo ni unyanyasaji, ni kwa nini ampige? Hana haki ya kuishi? Kwa nini usiku asipumzike, hana haki ya kulala? Wewe uende kilabuni urudi umelewa halafu uje kumnyanyasa, unyanyasaji ukomeshwe na lazima tuwe na mkakati kama baadhi ya nchi zilivyofanya, China na Irani hawakubaliani kabisa na unyanyasaji, unapofanya madhila dhihi ya mwanamke unanyongwa barabarani mbele za watu. *Yes! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapotaka kumpiga Ngedere usimuangalie sura yake, kama tunaoneana aibu sheria zetu haziruhusu lakini unyanyasaji utakuwa unaaendelea. Watu wanaoa, wanaacha hovsky, hakuna kitu ambacho Mungu amekihalalisha lakini akawa hakifurahii kama talaka lakini leo sisi tunazitoa tu talaka, upumbavu mtupu, kosa dogo unamuacha mke, unatafuta mwengine, kwa nini? Tuishi na wake zetu, tulee watoto wetu, tuwape elimu nzuri, lishe bora, redio zifike vijiji ili wasikie programme za Serikali zikoje juu ya haki zao. Hatuwezi tukakaa kimya tukawaona ndugu zetu wanawake, akina dada na mama zetu wananyanyaswa, tusome magazeti kila siku na ningefurahi sana kama hii Wizara ingekuwa inafuutilia magazeti kuona hata watoto wadogo ambao wanadai laki moja au mbili kwa ajili ya matibabu, inasikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikundi cha TAMWA kinafanya kazi nzuri, kianze kuibua watoto ambao wana matatizo ili wasaidiwe kama Wizara haina fedha waje hapa Bungeni, tuko tayari kuchangia ili watoto hawa wafanyiwe *operation* na wapone. Hata yatima, dini yetu ya Kiislam imekataza kabisa kuwatenga yatima tunaambiwa tuwasaidie yatima kwa njia zote, tukae nao katika familia, hebu tugawane sisi Wabunge yatima mmoja mmoja, tutakuwa na yatima 350 ambao tunakuwa nao katika nyumba zetu badala ya kuwaweka katika vituo vya kulelea yatima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Huwezi kumkatalia mtu anayezungumzia habari ya yatima na Haroub mwengine anayekuja, tunaomba mwendo huu uendelee hivyo, Haroub akistaafu tumpate Haroub mwengine. Tumefurahi sana kwa maeleo hayo na tunakutakia kheri kwa kweli ndiyo maana nikasema tutaruhusu Wabunge wanaume wote waseme maana yake wao watasema zaidi kuliko sisi. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa mchango wako kwa kweli hauna dosari hata kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, jioni tukirudi tuna wachangiaji wawili ambao ni Mheshimiwa Bujibu Sakila halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Mikidadi, kwa hiyo, orodha yangu itakuwa imekamilika. Kwa hiyo, nitaanza kuwapa Waheshimiwa Mawaziri waanze kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ninalo tangazo muhimu kwamba tarehe 7/7 siku ya Sabasaba katika Ukumbi wa Pius Msekwa tutakuwa na semina iliyandaliliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Muswada wa *Public Private Partnership*. Hii concept ya *Public Private Partnership* ni

mpya kuliko kuileta tu hapa bila kupata nafasi kwenye semina na kuelewa *concept* yake n nini itawawia vigumu sana kutunga sheria bila kuipitia.

Vilevile kuna kitabu kipo kwenye *pegeion holes* zenu kinaitwa *The National Public Private Partnership (PPP) Prime Ministers Office*, kimesambazwa huko. Kwa hiyo, itakuwa vizuri kama Waheshimiwa mtaweza kukipitia na kukiona kitabu hicho na kukisoma lakini bahati mbaya kimeandikwa kwa lugha ya Kingereza lakini nafikiri mkisoma wengi itatusaidia kufanya kazi yetu siku Muswada utakapoletwa.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lingine nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 7.00 Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge kipindi cha asubuhi, tulikuwa tumbakia na wachangiaji wawili. Sasa nitamwita Mheshimiwa Bujiku Sakila, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Mikidadi.

MHE. BUJIKU P. SAKILA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii, kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kwa sababu muda ni mfupi sana, ni vema tu nikaanza kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii, kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa mambo mawili. Kwanza kabisa, viongozi hawa ni wasikivu sana. Mimi nimo katika Kamati ya Maendeleo ya Jamii, nimekuwa nayo kwa kipindi cha miaka mitano, ushauri wetu walikuwa wanausikiliza vizuri sana na ndio maana katika kipindi cha miaka mitano hii tumekwenda vizuri sana. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa usikivu wao huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji wa Wizara hii vilevile wamekuwa karibu sana na Kamati yetu, kama tulivyosema katika taarifa yetu tumekuwa kama familia moja. Kila wakati tulipokuwa tunakutana, tumekuwa tunaongea mambo, tunaelewana vizuri sana. Ninawapongeza sana kwa moyo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii vilevile kuwapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii. Wakati tunaingia katika kipindi cha hiki cha miaka mitano, kwa sisi Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, tulikuwa tunaona kwamba hata watendaji katika Wizara hii ile *morale* ilikuwa chini sana lakini leo hii wana moyo mzuri. Mimi nashukuru kwamba hawa Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Watendaji wameinua ile ari ya Wizara hii. Nawapongeza sana kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi, kwa kweli mimi sina mambo mengi sana. Kwanza, nimesimama kuwapongeza kama nilivyoanza lakini baadaye nitatoa maombi, na nitamalizia kwa shukurani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, kwanza hotuba yao ni nzuri sana. Inatia matumaini hasa kwa kulinganisha kiasi kidogo cha fedha walichopewa. Mara kwa mara tulipokuwa tunakuja hapa mbele ya Bunge lako Tukufu, tumekuwa tukiomba sana Wizara hii iongezewe fedha sababu hasa ilikuwa ni kwa kuangalia majukumu yake. Wizara hii kwa mtazamo wangu mimi, ina kazi kubwa sana ya kutetea wanyonge. Tunayo makundi mawili makubwa katika Wizara hii, tuna wanawake na watoto. Kinachohitaji hapa ni sheria zitungwe, sheria wanatunga, lakini hapa siyo suala la kutunga sheria tu, lakini vile vile kuifanya sheria hiyo ijulikane kwa wananchi ili iweze kutekelezwa vizuri zaidi. Kwa hiyo, naipongeza sana Wizara hii kwa kuleta Miswada ya Sheria katika kipindi hiki, mmefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba bado kuna sheria tunahitaji zije hasa za haki za akina mama, masuala ya ndoa na mirathi. Tunaomba sana Serikali iangalie jinsi ya kuleta sheria hizo mapema kama wenzangu walivyosema, hapo ndipo tutakuwa tumewatendea haki akina mama hasa kwa kutambua kwamba hili ndio kundi ambalo kwa muda mrefu sana limekuwa likinyanyaswa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii, kuipongeza Wizara hii kwani wamefanikiwa kufungua Benki ya Wanawake. Vilevile wameendelea kutoa mikopo, lakini hapa ningependa kutoa ombi moja. Akina mama wengi sana vijijini wanapata mikopo lakini wanachohitaji ni elimu jinsi ya kuitumia mikopo hiyo ili waweze kwa haraka sana kurejesha mikopo hiyo. Tumeona na kufuatilia sana mikopo hiyo ambayo inakwenda makundi mengi ya akina mama, unakuta ni baadhi tu ya vikundi au akina mama wachache amba wanufaika. Baadhi ya akina mama, fedha ikipatikana haiendi katika mipango iliyotarajiwa. Ombi langu kwa Wizara hii, ijipange vizuri ili hawa akina mama kila wanapopata mikopo, kabla hawajaitumia basi waendelee kupata elimu ya mikopo ili fedha inapopatikana waweze kuitumia vizuri na waweze kuirudisha mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kama nilivyosema, napenda kufanya maombi fulani katika jedwali, ukurasa wa 45 wa Kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kuna Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, halafu inaendelea Ngudu, hilo ni tatizo ambalo linajulikana kwa muda mrefu sana kwamba watu hawafahamu Kwimba iko wapi na Ngudu iko wapi. Napenda kusema kwamba, katika kile kitabu labda wangerekebisha tu kwamba Halmashauri ya Wilaya ni Kwimba, Makao Makuu ya Wilaya ndio Ngudu, nimeona hapa wamechanganya kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninaomba nifahamishwe vilevile, katika hotuba wamesema mkopo kwa mwaka 2009/2010 Kwimba imepata shilingi milioni nne (4). Kwanza, nimejaribu kufuatilia ni kwa nini imepata shilingi milioni nne tu, nimeshindwa kuelewa. Lakini vilevile Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, wanasema kwamba hata

hizo shilingi milioni nne hawajazipata. Ningependa tu nijulishwe fedha hiyo imetumwa lini, kwa sababu wanasema kwa mwaka huu Kwimba bado ilikuwa haijapata fedha japokuwa hapa imeandikwa shilingi milioni nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia hamsini kwa hamsini (50% - 50%), naipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia na wanaenda vizuri sana. Mimi ninaamini kwamba, tunaenda vizuri. Ombi langu hapa tujitahidi kwenda pamoja vizuri, nafikiri tunaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma katika kitabu cha bajeti, bado kidogo kuna mawazo kwamba hii Wizara ni ya Wanawake na Watoto tu. Bado haijakaa vizuri, ukiangalia yale maneno, kwa sababu hii hotuba imesomwa mbele ya wananchi na wameisikia. Kwa hiyo, unaposema unasoma kitu kilekile wenzetu wanaweka upande ule. Mimi ninaomba sana, safari nyingine wajaribu kuipitia na walinganishe kwamba, hii hapa ni ya jinsia ili iweze ku-*balance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza sana baadhi ya akina mama ambao wamenisaidia sana katika hali yangu. Kwanza, kabisa Mama Annah Abdallah, amenisaidia sana mwaka 2005, nilikuwa nimekata tamaa. Yeye akiwa Waziri wa Afya, ndiye aliyenitia moyo mpaka nikarudi katika Bunge hili. Lakini vilevile aliyekuwa Katibu Mkuu wake, Mama Mwafissi aliweka ratiba ya kuwa ananitembelea mara kwa mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuzungumzia mada hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nikupongeze wewe kwa kuwa ulikuwa mwanamke wa kwanza kuwa Waziri wa Maendeleo ya Wanawake, Jinsia na Watoto wakati huo na ulifanya kazi nzuri sana kiasi kwamba wengine wote waliofuatia waliiga nyayo zako. Hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amezungumzia mambo mengi, zaidi ya Kumi na Moja (11) yanayohusu Wizara hii lakini mimi nizungumzie masuala mawili tu; la kwanza, kuhusu *NGOs* na la pili, kuongeza nafasi na fursa za uongozi kwa wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze na masuala ya *NGOs*. Madhumuni ya *NGOs* kulingana na Sera ya *NGO*, Na. 24 ya mwaka 2002. Nia na madhumuni ya *NGO*, ni kusaidia Serikali pale ambapo inashindwa kutoa msaada lakini utakuta baadhi ya *NGO* badala ya kusaidia Serikali, zinapinga Serikali, zinafanya maandalaman kupinga maamuzi ya Serikali, Serikali imepanga mipango yao wao wanapinga. Katika suala hili, mimi

sikubaliani nao. Natoa angalizo *NGOs* zote zinazopinga maamuzi na mipango ya Serikali kwa ajili ya maendeleo ya jamii ziangaliwe upya ili zifanyiwe kazi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, *NGOs* zilizotajwa ambazo ni *NGOs* za Ikulu, baadhi ya wachangiaji wamezungumzia hapa kwamba *NGOs* hizi zina matatizo, zinatumia Ofisi za Ikulu, zinatumia fedha za Ikulu na kadhalika. Sasa mimi ninataka niseme hili tu kwamba, hizi *NGOs* zote za Wake wa Marais, tumeona Rais Mwinyi, Rais Mkapa, Rais Kikwete, kwa kweli ni *NGOs* ambazo zinasaidia jamii na wenyewe tunaona kwa macho, kila Wilaya, Mkoa na kazi wanazofanya, sijaona *NGOs* hizi zinakwenda kinyume chake. Sanasana fedha wanazopata ni kwa wao wenyewe kufanya *fund raising*, kutafuta misaada maeneo mbalimbali huko na huko, sijaona hapa katika bajeti inapangwa kwamba hizi ni fedha za *NGOs* za Wake za Marais, sijaona. Kwa hiyo, ninataka niwaambie ndugu jamii kwamba, hizi *NGOs* za Wake wa Marais ni *NGOs* zinazosaidia jamii kwa kweli na siyo zile *NGOs* za mifukoni kama wengine wanavyodhani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikupe mfano mmoja tu, tuchukue mfano wa *NGO* ya Mama Mkapa. Sasa hivi mimi mwenyewe ni shuhuda, ninatoka Dar es Salaam, nimeshuhudia jinsi *NGO* ile ilivyoendeleza akina mama wajasiriamali. Wamejaa kwenye Banda la Sabasaba na ni yeye ambaye amefanya kazi hiyo ya kuwasaidia akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, twende kwa Mama Kikwete. *NGO* ya Mama Kikwete sasa hivi inaendeleza mambo mbalimbali, imeweza kusaidia Shule za Sekondari, imeweza kujenga Mabweni ya Wasichana, imeweza kusaidia vitanda vyta hospitali kwa ajili ya kuzalia akina mama na nyie wenyewe ni mashahidi. Mimi mwenyewe Lindi tayari tumepata vitanda, tumejengewa bweni, tayari sekondari mbalimbali zimesaidiwa na si Lindi tu bali Mikoa mbalimbali nchini Tanzania, yeye mwenyewe amekwenda Mkoa kwa Mkoa, Makete, wapi, nyie wenyewe mtakuwa mashahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninasema kwamba *NGOs* za Wake za Marais, ni *NGOs* za kweli kweli na wanapata pesa za kwao wenyewe kwa kuomba kutoka maeneo mbalimbali na si za kutengewa katika bajeti hapa. Sasa asitoke mtu, akasema kwamba *NGOs* hizi hazifai, zinatumia pesa za Rais, si kweli. Mimi nasema ninawapongeza kwa kazi yao nzuri na waendeleze kazi nzuri wanayoifanya na sisi tuko nyuma yao kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena. Kwa hilo, Mama Salma Kikwete usirudi nyuma, endeleza kazi yako ya kusaidia jamii. Kama ninyi mnataka hiyo nafasi ya kuwa *First Lady* ili na ninyi muwe na *NGO* na nini, basi tafuteni na ninyi muweze kuwa na *NGOs* na siyo kumhujumu mtu, kwamba anafanya vile na hivi, hivi na hivi, si kweli. Mama Kikwete anafanya kazi nzuri sana Tanzania, nampongeza sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiachia suala la *NGOs* za Wake za Marais, ya Mama Kikwete, Mama Mkapa na Mama Mwinyi jinsi wanavyofanya kazi yao vizuri, nije sasa katika suala la kuongeza nafasi na fursa za uongozi kwa wanawake. Kwanza,

ninaipongeza Serikali kwa jitihada zao kubwa za kuongeza nafasi za uongozi katika maeneo kadhaa. Kwa kweli Marais wote wamefuata nyayo za Mwalimu Nyerere za kuendeleza Wanawake katika uongozi. Marais wote watatu waliofuata, Rais Mwinyi, Rais Mkapa na Rais Kikwete kwa sababu Rais Nyerere alipotawala tu, suala la kwanza lilikuwa kuwasaidia wanawake na hii ipo katika Ilani ya Uchaguzi na Sheria zake zote na alifanya hivyo akiamini kwamba wanawake ndiyo maendeleo, wanawake ni nguzo ya maendeleo na wanawake ni wenza katika maendeleo. Kwa hiyo, Marais wote waliofuata walifanya hivyo na mimi kwa kweli ninawapongeza kwa suala hilo na sasa ninasema Marais wote waliofuatia wametambua haki za kimsingi za mwanamke, kisiasa, kiuchumi na kijamii na ndiyo maana sasa tupo hapa. Hata mimi ambaye sikustahili nipo hapa leo, ingekuwa Rais hakutambua masuala ya wanawake, mimi nisingekuwa Mbunge hapa leo. Kwa kweli ni lazima tushukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili wanasema ni lazima kupongeza pale inapobidi kupongeza. Juzi nilisema ukilaumu kila kitu, kila siku wewe utaambiwa una kasoro. Sasa nasema kwa hilo ni suala zuri. Napenda kusema kwamba, Wizara sasa tujipange. Sasa hivi ni wakati muafaka wa kuangalia agenda zile kuu tatu muhimu ambazo zipo kwa wanawake kwamba, zimefanya nini, zimetekeleza nini, tupo wapi na tufanyeje?

Mheshimiwa Naibu Spika, agenda ya kwanza, utekelezaji wa Mkutano wa Beijing wa kutaka Haki, Usawa na Maendeleo ya Mwanamke, tumefanya nini, tuko wapi na tunaendeleaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, ajenda ya pili ni utekelezaji wa Mkataba wa Wanawake wa mwaka 1979, mkataba ule ulisainiwa na nchi 27 za Afrika, mojawapo ikiwa ni Tanzania. Hiyo ilikuwa haki za wanawake za kimsingi, tumefikia wapi, tuliangalie hilo na ajenda ya tatu ni Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda umekwisha naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia, ahsante sana. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. FATMA OTHMAN ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Jamii, ni Wizara inayoungana na Wizara zote zilizopo hapa Tanzania. Ninaipongeza Wizara hii kwa kusimamia kwa dhati utungwaji wa Sheria ya Mtoto kwani mtoto wa Kitanzania walikuwa wanateswa na kuadhibiwa bila kuwa na mahali pa kwenda kutoa malalamiko yao, kwa hilo, tunashukuru sisi wazazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaipongeza Wizara hii kwa jitihada zake kwa kuishinikiza Serikali kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake. Benki hii ni ya ukombozi kwa wanawake pamoja na wanaume kwani inawahudumia wanawake wa kiwango cha chini. Lakini Mheshimiwa Waziri pia wanawake wa Vijijini wana mahitaji makubwa sana ya kupata mafunzo kuhusu benki hii pamoja na mafunzo ya SACCOs.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukatili kwa watoto bado ungalipo kwani mara nyingi tunaonyeshwa kwenye TV watoto wanaopata kipigo kutoka kwa wazazi au walezi wao na kipigo hicho kinakuwa si cha kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunaomba Wizara mtoe elimu kupitia vyombo vya habari ili wananchi wazidi kuelewa kuhusu Vyuo vya Maendeleo, tumevitembelea lakini bado vyuo hivyo haviridhishi. Naomba Wizara katika kipindi cha bajeti ichague vyuo japo vitano wavifanyie ukarabati na kuongeza miundombinu mizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *NGOs*, ninapenda zifuatiliwe kwa kina zaidi kwa kuwa kuna *NGOs* nyingine hazifanyi kazi zao kama inavyotakiwa na kufanya kazi sio zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa Benki ya Wanawake, ni jambo jema sana na wanawake wengi wana mategemeo makubwa ya kufikiwa na huduma za Benki hii. Je, kuna mipango gani huduma hii kuwafikia wanawake vijiji ambako ndiko waliko wanawake wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ajira ya watoto bado lipo na linaathiri maendeleo ya mtoto ikiwemo ukosefu wa kupatiwa haki zao muhimu kama elimu, kulindwa, kuendelezwa na kushirikishwa nk. Je, Wizara ina mipango gani ya kuwasaidia watoto wa aina hii kupitia kwenye familia zao, kwani wakati mwingine watoto/familia wanaingia katika hali hiyo kutokana na umaskini uliokithiri na kukosa maelekezo hivyo kukata tamaa ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, unyanyasaji wa kijinsia, kwa kiasi kikubwa unachangia kurejesha nyuma maendeleo ya jamii hasa wanawake. Hivyo, tunaiomba Wizara iendelee kuelimisha jamii hasa vijiji kwani bado wanawake wananyanyasika katika kupata haki zao na watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Viongozi wote wa Wizara kwa uchapaji kazi mahiri na makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutamka kwamba naunga mkono hoja. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na Timu yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi zangu, naomba kutoa ushauri/ombi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mkopo ya Wanawake, nampongeza Waziri kwa kuwezesha mikopo kuwafikia wanawake vijiji ni katika jedwali Na. 2, Vikundi ya Wanawake Halmashauri mpya ya Ranya mwaka 2009/2010, walipata mkopo wa Tshs.8.0 milioni. Kwa kuwa Wilaya ya Ranya ilianza kupatiwa mkopo kama Wilaya mwaka 2009/2010, ni matumaini yangu katika mwaka 2010/2011 Vikundi/SACCOS za Wilaya ya Ranya watapata mikopo. Naomba Mheshimiwa Waziri atamke hapa Bungeni. Hii ni kwa sababu Wilaya mpya ya Ranya ni kama mtoto na inastahili malezi na misaada ili iweze kukua. Vikundi ya wanawake wajasiriamali ni 36, SACCOS ni kumi na mbili (12) hivyo basi mikopo iliyotolewa mwaka 2009/2010 haikuwafikia wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Taasisi na *NGOs* pamoja na Mashirika ya Kimataifa wanafanya kazi zao mijini na sio vijiji ni wachache tu ambao wako vijini, ni wakati muafaka kwa Wizara kuandaa utaratibu na mpango wa Kitaifa kwa kuwashauri viongozi wa Mashirika ya Kimataifa, *NGOs* na Taasisi mbalimbali kutoa huduma zao vijiji kwa kuwafikia akina mama hasa Wilaya ya Ranya. Naomba *SACCOs* zifuatazo ziwezeshwa kuititia *NGOs* na Mashirika ya Kimataifa, *SACCOs* hizo ni pamoja na A-Z, Kata ya Ranya, kijiji cha Utigi, Upendo, Kata ya Bukwe, Nyamtanga, Kata ya Nyamsingo, Nyathorogo, Kata ya Nyathorogo, Nyamange, Kata ya Nyamange, Kyangombe, Kata ya Kyangombe, Rabuor, Kata ya Rabuor, Kitembe, Kata ya Kitembe, Buhura, Kata ya Buhura, Nyanduge, Kata ya Nyanduge, Kisumwa, Kata ya Kisumwa, Roche, Kata ya Roche.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaombea Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa Mungu waweze kurudi tena Bungeni ili waweze kumaliza kazi walioanza.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Margaret S. Sitta (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary Nkya (Mb), Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, ni vichache, ningombaa Wizara iangalie upya jinsi ya kuanzisha katika Mikoa ya Tabora ambako kuna majengo mengi ambayo yangeweza kutumika kama Chuo kwa kuanzia kama vile majengo ya VETA, ambapo ni majengo ya kisasa. Kwani ukubwa wa eneo hilo kwa sasa imeonekana idadi ya watumiaji wa Chuo hicho ni wachache na kuna mabweni ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya *WDF*, niipongeze Serikali kwa kutoa fedha hiyo kuititia Halmashauri au Manispaa. Niombe ufuatiliaji wa takwimu uwe wa mara kwa mara na Wabunge wapewe taarifa ya marejesho na mikopo kwa waliopewa, ili waweze kutangaza Wizara inasaidia vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia ya Maendeleo kwa wanawake na vijana ambayo Halmashauri/Manispaa inatoa, ni vema pia Wizara ikasaidia kwa kutoa msisitizo wa utoaji wa fedha hizo kwani kwa Halmashauri zingine ni nzito. Ni vema sasa kwa kuwa sehemu kubwa ni wanawake wanaostahili kupewa fedha hizo, hivyo basi, TAMISEMI itoe waraka maalum kwa wahusika wanaozembea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi za Wakuu wa Idara katika Halmashauri zetu, hazina hadhi ya kutosha. Hivyo basi wapewe vitendea kazi vyatya kisasa ili waweke kumbukumbu zao sahihi na kwa wakati. Naomba wakopeshwe angalau pikipiki hasa wale ambao wako kwenye Kata hasa ukiangalia ukubwa wa maeneo hayo. Aidha, wapewe posho ya mazingira magumu ili waweze kutoa elimu ya maendeleo hasa kuhusu uendelezaji wa biashara zao na urejeshaji wa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri elimu itolewe kwa wananchi kuhusu haki za wanawake na watoto katika jamii hasa sheria hizi zilizopitishwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake (*TWB*). Wananchi hawa wapewe elimu ya kutosha, kwa nini *bank* hiyo ipo na umuhimu wa wao kuijunga na *bank* hiyo kwani *bank* hiyo bado wananchi wengi hawaijui vizuri. Hivyo basi, tuombe *bank* hii angalau kwa kuanzia *sub* yake iwepo Dodoma ili ihudumie Mikoa ya Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. HEMED MOHAMMED HEMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuamka nikiwa mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hotuba ya Mheshimiwa Waziri husika, imeanza kuleta matumaini katika kumkuza Mtanzania, maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kuwa na nia njema ya kumkomboa mtoto katika nyanja za ajira na kumpa elimu ili aepukane na unyanyasaji. Mtoto wa mwenzako ni wako, Wizara hii imewapa moyo wazazi wenye nia njema kwa watoto wetu. Mungu akupeni uwezo katika nia yenu njema ya kuwasaidia watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara pamoja na kazi kubwa miliyonayo, ni wakati muafaka sasa kupitia maeneo kama vile maeneo ya uvuvi, masokoni kwa vile ni maeneo ya ajira kwa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maendeleo, neno hili ni pana sana. Kwa mtazamo wa hali ya wananchi ni wazi bado wako nyuma kimaendeleo pamoja na nia njema ya Wizara. Hii ni kusema bajeti ya Wizara ni ndogo sana. Niiombe Serikali iiongezee fedha Wizara hii ili ifanikishe azma yake ya kumng'oa Mtanzania katika dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa malezi yake juu ya yatima. Kwa mtazamo wa dunia, wanadamu duniani tumekuja na tutaondoka na anayeondoka anaacha mtoto. Serikali imeweka Wizara maalum kumlea mtoto huyo, hongera Mheshimiwa Sitta na Naibu wako kwa umahiri wenu wa kuwalea watoto wetu walioachwa na wazee wao. Mungu yuko nanyi malipo atakulipeni Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nasema ahsante.

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kubwa kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri iliyofanywa na Wizara hii, kwa mfano kuwahimiza na kuwahamasisha wanawake ili wagombee uongozi katika nchi yetu; ufunguzi wa Benki ya Wanawake na kuitisha Sheria ya Mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuishukuru Wizara kwa kuruhusu Afisa Maendeleo wa Wilaya ya Rufiji kupewa fursa ya kuhudhuria Semina iliyopangwa na Wizara kwa ajili ya Watumishi wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inashughuli nyingi za kuliendeleza Taifa letu. Naomba Serikali iongezee bajeti ya Wizara hii. Hii ni Wizara inayomgusa kila Mtanzania, inastahili kupewa fedha za kutosha ili itimize kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kuwa Rufiji tunacho Chuo cha *FDC* Ikwiriri. Tuna matatizo makubwa matatu, kwanza, Chuo kinahitaji kipanuliwe na vile vile kuweko na mpango wa kukikarabati. Pili, Chuo hiki hakina gari, tunaomba usafiri na tatu, hivi karibuni niliwahi kupata malalamiko ya kuwa wengi wa wanafunzi wanaochaguliwa Chuo kile sio Wanarufiji, yaani wana Rufiji wako wachache sana. Naomba Wizara iwaelimishe Walimu na Maafisa wa *FDC* Ikwiriri wahakikishe kuwa *FDC* ya Ikwiriri ipo Rufiji, kwa hiyo lazima Wanarufiji wapate elimu. Naiomba Serikali ichukue hatua za haraka kurekebisha hali hii ili wanarufiji nao wapate elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba Mbingu na Ardhi, kwa kunijalia mimi na Bunge lako Tukufu kujadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru kina mama wa Mkoa wa Kusini Unguja, kwa kuniamini na kunipa ridhaa ya kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu na mimi naahidi sitowaangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri na kusimamia vyema majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina majukumu makubwa lakini bado kipaumbele ni kidogo kuhusu bajeti kwani fedha zinazopewa Wizara hii ni kidogo na pia hicho kidogo kinachelewa kutolewa. Kwa hivyo, naiomba Serikali kuipa kipaumbele Wizara hii kwa kuipatia fedha nyingi pia zitolewe kwa wakati ili kusukuma mbele maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukatili dhidi ya wanawake. Ukatili dhidi ya wanawake, ni mkusanyiko wa mambo mengi ambayo hayafai kufanyiwa wanawake na

watoto lakini mimi nitazungumzia mimba za utotoni. Suala la mimba za utotoni, naona bado hatua madhubuti ya kukomesha suala hili hazijachukuliwa kwa sababu vitendo bado vinaongezeka na hatua iliyofikia ni ya kutisha na madhara makubwa yanapatikana kwa sababu watoto wadogo wanaobeba mimba hufa wakati wa uzazi na hivyo kusababisha vifo vingi vya mama na watoto na kuwakatisha elimu wanawake wakati wanaowabebesha mimba wanaranda mitaani. Naiomba Serikali ichukue hatua kwa kutunga sheria kali za wanaowabebesha mimba watoto ikiwemo kifungo cha miaka mitano (5). Wazee wa zamani walisema huruma hailei na ukitaka kuondosha tatizo basi uongeze tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi kubwa walionayo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzalilishaji wa wanawake bado unaendelea. Ni jambo la kusikitisha sana, kwa sababu matukio mengi yanatokea hapa nchini ya wanawake kuuliwa na waume zao. Hili ni jambo la kusikitisha sana hata hivyo baadaye huijuwa wenyewe kwa hofu ya kuadhibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanafunzi wa kike kubakwa, hili ni jambo la kusikitisha. Matukio haya yamezidi katika mji wa Morogoro ambapo watoto 83 walibakwa katika mwezi wa January – April, hali hii inatisha. Kwanza, wazazi na walezi na Walimu tuijilize tumechukua hatua gani kuhusu matukio haya? Ni lazima wachukuliwe hatua wabakaji pale watakapokamatwa na hatua za kisheria zichukuliwe ili kukomesha unyanyasaji huo hata ikiwa Mwalimu anahusika achukuliwe hatua kali na kwanza afukuzwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Askari wa kike aliyepewa dhamana ya kuongoza msafara wa Rais na akaupoteza, ni kweli alifanya makosa na kuchukuliwa hatua ya kupelekwa kituoni kwa kuhojiwa na kuwekwa mahabusu. La kusikitisha Askari huyo alijiwa mwenyewe kwa kujipiga risasi. La kusikitisha sana na kushangaza kwa sababu mtuhumiwa anapopelekwa mahabusu anapekuliwa na kila kitu chake kinachukuliwa hata ikiwa ni mkanda ananyang'anywa, Askari aliyekuwepo kituoni ama hakuwa mwangalifu au alikuwa mzembe kwa huyo Askari hivyo achukuliwe hatua na ufanywe uchunguzi wa kina juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, ninaupongeza uongozi wa Wizara pamoja na watendaji wake wote, kwa kuandaa taarifa

nzuri yenyе kуаа таkwimу. Taarifa yoyote lazima iwe na takwimу kama taarifa hii, hongera sana mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ina maelezo zaidi ya 10 lakini nichangie machache tu, *NGO*, Benki ya Wanawake na kuонgeza nafasi na fursa kwa uongozi. *NGO* ambazo zinaongozwa na Wake wa Rais ni muhimu sana kwani zina fursa ya kupata misaada kutoka Balozi mbalimbali na hivyo kusaidia akina mama. Kwa kweli nichukue nafasi hii kuzipongeza *NGO* ya Mama Mkapa, Rais Mstaafu (Mrs.), ya Fursa Sawa kwa Wote na *NGO* ya WAMA ya Mama Kikwete, Rais wa sasa. Kwa kweli, wanafanya kazi nzuri sana na endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usajili wa *NGO*, nyingi hufanya kazi mijini sana kuliko vijijini. Sasa tuangalie ziende zikafanye kazi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NGO* zingine ni matatizo, baadhi ya *NGO* huwa Wapinzani wa Serikali, Sheria Na.24/2002 ya *NGO*, moja ya nia yake ni kusaidia jamii na Serikali lakini *NGO* zingine wanakuwa Wapinzani wa Serikali, je, tuwafikiriaje? Ninaweka angalizo juu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake, pongezi kwa waanzilishi wa benki hii waliochangia ili kupata pesa, ahsante sana. Tunaomba sana, kuwa na mikakati ya kuendeleza benki hizi Mikoani ili kuwafikia akina mama walio wengi, ziende vijijini badala ya kukaa mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuонgeza nafasi na fursa kwa uongozi, tunaishukuru sana Serikali kwa jitihada kubwa za kuонgeza nafasi za uongozi katika maeneo kadhaa. Kwa kweli tunawapongeza Marais wote waliofuata baada ya Mwalimu Nyerere kwa kufuata nyao za Mwalimu Nyerere kwa kuwasaidia wanawake katika kuwaendeleza katika uongozi. Hongera sana, Rais Mwinyi, Rais Mkapa, Rais Kikwete, wote wanaendeleza wanawake wakiamini kuwa, wanawake wanaweza, wanawake ndio nguzo ya maendeleo, wanawake ni wenzao, mwanamke ni nguvu kazi na huzaa nguvu kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaagiza viongozi wote tushirikiane kuwaendeleza wanawake.

MHE. ANIA S. CHAUREMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa maandishi hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina majukumu makubwa, bajeti yake iwe inaongezwa zaidi ili kufikia malengo yake ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukatili kwa wanawake umezidi, wanawake wanakatwa na mapanga na kupata ulemavu na hata kupoteza maisha, kubakwa na kadhalika. Pamoja na hali hiyo, kwa upande wa watoto, ubakaji na kunajisi watoto bado tatizo kubwa. Hii

Mikoa ambayo inaongoza kwa jambo hili mfano Morogoro na mengine itolewe elimu ya uelewa wa jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watoto wa mitaani, kundi hili linachangiwa zaidi na wazazi wa watoto hawa hasa katika Jiji la Dar es Salaam hukaa pembedi na watoto huombaomba. Adhabu ya sasa kwa wazazi ni ndogo, huchukuliwa kurudishwa kwao na wao hurudi tena, sheria kali ziwekwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Upinzani ameongea kuhusu miradi ya wajane, naomba niongeze kidogo, wanawake hadi sasa hawana chombo madhubuti kinachowasaidia pindi waume za wanapofariki. Bado kuna tatizo kubwa pamoja na jitihada kubwa za *NGO* za kutoa msaada wa kisheria. Ninapendekeza kiundwe chombo hasa cha kutoa msaada zaidi kwa kundi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake, chombo hiki ni muhimu na wananchi wamekipokea na kujiunga. Sasa kilichobaki zifanywe jitihada za makusudi kukieneza nchi nzima, ili malengo yake yakamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, utumikishwaji kazi kwa watoto. Pamoja na jitihada kubwa ya Serikali katika kulinda haki za watoto na kutoa elimu, bado kuna baadhi ya watoto wanafanya kazi tena ngumu za kugonga kokoto na kufanyishwa kazi katika migodi. Wizara iwe inavamia maeneo haya na kuweka wakala wa kuangalia udhibiti, haya ni maeneo sugu na ni rahisi kufatilia.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii na Jinsia na Watoto, Dada yangu mpendwa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Naibu Waziri, Mheshimiwa Daktari Lucy Sawere Nkya, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri, iliyandoaliwa kitaalam ikiwa imizingatia vipaumbele vyote walivyovainisha kwa lengo la kuboresha Wizara hii hususani sekta ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, pia ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu awape Baraka tele ili wapiga kura wao wawape kura za kishindo ili dada yangu Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Waziri mwenye dhamana na Mheshimiwa Daktari Lucy Sawere Nkya, Naibu Waziri, warudi Bungeni kuendeleza mikakati yao ndani ya Wizara yao kama walivyoandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuombea pia Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Tanzania ili arudi kwenye nafasi yake kwa kishindo, naye aweze kuwateua tena dada zangu hawa wachapakazi.

Mheshimiwa Spika, vile vile niwapongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Haroub Masoud pamoja na wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa kazi kubwa waliyofanya kuishauri Wizara hii. Hivyo basi, endapo

watachukua fomu tena kugombea, wapiga kura wao wawapigie kura za kishindo ili warudi kuendelea kuisaidia Serikali pamoja na wapiga kura wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake Tanzania, napenda kuipongeza sana Serikali kukubali kuanzisha Benki ya Wanawake ambayo imekuwa ni ukombozi sana kwa wanawake na jamii kwa ujumla. Ninasema hivi kwani nina uhakika wataweka fedha zao na pia watakopeshwa fedha kwa ajili ya miradi yao mbalimbali ya uzalishaji mali kwa maslahi ya familia zao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba viongozi wa Benki hii watoe vitambulisho kwa wanachama wenye hisa mapema mfano hata mimi nina hisa bali sina kitambulisho chochote. Ninaomba Serikali kupanua huduma ya Benki hii kwa kufungua matawi Mikoa mbalimbali ili wanawake na wananchi kwa ujumla wapate huduma hii. Ninaomba Serikali itafute njia bora ya kuinadi Benki ili ipate wateja wengi hasa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Serikali kwani imekuwa makini katika kuboresha sekta mbalimbali za Serikali kwa kuhamisha watumishi kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyingine, mfano Walimu waliokuwa chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu wakaajiriwa na Maendeleo ya Jamii kwa ajili ya kufundisha Vyuo vya Maendeleo. Kumekuwa na tatizo la Walimu hawa kuchelewa kupanda madaraja pamoja na kurekebishiwa mishahara yao. Hivyo ninaomba Serikali kuititia madaraja ya Walimu wote wanafundisha Vyuo vya Maendeleo amba walitokea Wizara zingine mfano wapo Walimu wa aina hiyo katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuikumbusha Serikali kuwa bajeti wanayopeleka Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, ni ndogo sana kwani vyuo vingi vinaendesha shughuli zake kwa vyanzo vyao wenyewe ama kutafuta wahisani. Hii nimeona kwenye Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Singida. Ninaomba Serikali kuongeza bajeti kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vikiwemo Chuo cha Maendeleo cha Singida na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Msingi, Wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mwalimu Mlade, Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Mjini Singida, kwa juhudhi zake kubwa za kukiendeleza Chuo hiki, kwa ubunifu wake akishirikiana na watumishi walioko chuoni hapo. Ninaomba Serikali itambue juhudhi za Mwalimu Mlade kwa kutamka hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuikumbusha Serikali ombi langu la gari kwa ajili ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Singida. Ni muda mrefu sasa tangu nilipowasilisha ombi langu la gari kwa ajili ya Chuo hiki. Inasikitisha sana Wizara imeshindwa kuona uwezekano wa kukipatia Chuo hiki cha Singida gari ukizingatia Chuo hiki kimekuwa kikubwa sana kwa juhudhi za Chuo chenyewe kuongeza majengo na huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu asilimia hamsini ya wanawake katika vyombo vya maamuzi, ninapenda kuipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa wanawake kuingia kwenye vyombo vya maamuzi. Hivyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudzi zake kubwa za kuwaweka wanawake kwenye vyombo vya maamuzi mfano Majaji, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na wajumbe wa Bodimbalimbali za Mashirika ya Umma. Ninaomba wote wenye dhamana za uongozi kwenye taasisi za Serikali, kuteua au kuajiri wanawake kwa kuunga mkono juhudzi za Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete. Vilevile Serikali kusaidia kuhamasisha wanawake kugombea nafasi mbalimbali pamoja na kuelimisha wanaume kuacha mfumo dume sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya watoto wenye mazingira hatarishi pamoja na yatima, ni ukweli usiofichika kuwa bado kuna tatizo kubwa la watoto kutangatanga mijini na kuendelea kukosa malezi mema ambayo ndio msingi wa maisha bora ya maisha yao. Napenda kuiomba Serikali kuwa ni vyema kuanzisha Kituo cha Watoto wenye mazingira magumu kila Mkoo kwani tatizo hili ni kubwa na halikwepeki kwa sababu ya kuwepo wazazi maskini, wazazi walevi, wazazi walemvu na ama watoto kushindikana nyumbani. Endapo kila Mkoo utakuwa na Kituo cha Serikali na ambacho kitatengewa bajeti, itasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mikoa mingine inavyo vituo vya watoto ambavyo vilianzishwa na wahisani/wageni na tayari walisharudi kwao basi Serikali ivichukue vituo hivi na kuvitengea bajeti kuliko kuviacha vikiendeshwa kwa kusuasua, mfano Kituo cha Kititimo kilichopo Singida Mjini ambacho hakina mmiliki kinategemea wasamaria wema mfano, Ndugu Husein Nagji, mfanyabiashara wa Kihindi anayeishi Singida Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake kushikamana, ni ukweli usiofichika kuwa wanawake sasa hivi wamebadilika sana tofauti kabisa na miaka iliyopita kwani walikuwa hawapendani na walikuwa na tabia ya kukatishana tamaa hata kupakana matope. Inatia moyo sana sasa hivi wanawake wanapendana na kuungana mkono sana bado wapo wachache ambaowakuwa wanasiwa wanapata madaraka kwa kubahatisha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara itengete fedha za kutosha kutoa elimu kwa wanawake na wanaume pia kuacha mfumo dume na kuacha kuwanyanya wa wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zinalinda wanawake na watoto kurekebishesha, ninapenda kuikumbusha Serikali kuwa bado sheria zinazomlinda mwanamke na mtoto nyingi zimepitwa na wakati. Ninaomba mchakato ufanyakie haraka, ziletwe hapa Bungeni kufanyiwa marekebishesha ili ziwalinde wanawake na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea na kusoma taarifa ya Wizara hii kwa umakini wa hali ya juu na kuipongeza kwa dhati Wizara hii chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Margaret Sitta, Waziri akisaidiwa na Naibu wake na Katibu Mkuu kwa taarifa nzuri na kutia moyo. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndiyo kwa miaka mingi ilikuwa kiungo muhimu (*linking pin*) kwa Wizara zote za maendeleo ya wananchi wetu. Wizara hii ndiyo yenye taaluma za kutafsiri na kuelekeza kwa lugha rahisi mipango mbalimbali ya Serikali lakini ndiyo Wizara inayotengewa fedha kidogo. Lazima mtazamo huu uangaliwe upya. Nalisema hili kwa sababu mafanikio ya sera mbalimbali yanatarajiwa yawe katika midomo ya Maafisa wetu wa Maendeleo ya Jamii, kwa mfano, sera ya Kilimo Kwanza unategemea viperi kuenezwa bila Wizara hii kuhusishwa? Tuipe fedha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kuanzisha Benki ya Wanawake lakini ni budi Serikali iamue kwa dhati kuisaidia benki hii kwa kuwapa baadhi ya shughuli kama upendeleo wa kupitishia baadhi ya fedha zake, mishahara na fedha za JK au wajasiriamalli zipitie huko. Bado watu wengi wataendelea kuona kuwa hii ni benki ya wanawake tu na siyo ya wote. Elimu bado inahitajika. Nawapongeza kwa kuanzisha benki hii kwa kuweka uongozi mahiri wa wanawake wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitamwomba Mheshimiwa Waziri aone namna ya kuimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili utekelezaji majukumu yao magumu, vyuo hivi tunavyovitegemea sana lakini kiasi cha fedha zinazotengwa hazilingani na hali halisi ya majukumu yao, Waziri alifafanua suala hili maana chimbuko la mafanikio ya kupunguza umaskini nchini utategemea sana jinsi vyuo hivi vitakavyoandaa wananchi kutekeleza sera mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kasi ya ongezeko la watu, tofauti na ukuaji wa uchumi ni mambo ambayo Wizara hii kupitia vyuo hivi, lingeshughulikiwa ikiwa ni pamoa na afya ya mama na mtoto, kupewa uzito unaostahili katika kupunguza kasi ya ongezeko la watu, ukatili unyanyasaji kwa wanawake kunahitaji mpango kabambe wa kweli na siyo wa kulifanya mzaha. Naomba Wizara ieleze hatua ambayo imefikia katika kulitatua suala hili zito na mbinu ambazo zinaandaliwa ili wanaume wawe sehemu ya tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zinazofanywa na Mheshimiwa Mama Salma Kikwete ni budi ziungwe mkono ili hapo baadaye ziundwe taasisi za *WAMA*, Mikoani ili kuwepo na uendelevu rasmi wa kazi nzuri anazozifanya na zisiwe tu wakati yupo madarakani bali hata akistaifu kazi nzuri hiyo iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na kumtakia Mheshimiwa Waziri na Naibu kheri kwenye kinyanganyiro cha uchaguzi mkuu ujao. *Best wishes.*

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kuwa kuandaa hotuba nzuri. Vile vile nampongeza Waziri na watendaji wake wote kwani tangu niingie

madarakani, Wizara imechangamka inafanya mambo mazuri yanayoonekana. Hongera sana. Nipende kuipongeza Wizara yako kwa yafuatayo:-

- Kutunga Sheria moja ya Watoto kitu kilichokwuwa kimeshindikana.
- Kuanzisha Benki ya Wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Rais kwa utashi wake wa kuridhia Benki ikaanza, Benki hii itakuwa mkombozi wa wanawake na Watanzania walio wengi. Watanzania walio wengi wana hamu ya kupata huduma kutoka kwenye Benki hii. Ili isije ikaonekana kama ni Benki ya watu wa Dar es salaam tu, je ni lini matawi yatafunguliwa mikoani hususani Mkoa wa Kagera?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo makubwa kwenye jamii, Watanzania walio wengi hawapendi kufanya kazi vya kutosha, wengi wanashinda kwenye vijiwe vijijini kazi za kilimo wanaachiwa wanawake na wasichana. Wizara ya Maendeleo ya Jamii wanalo jukumu la kubadilisha *attitude of mind* au *mind set* za hawa wananchi ili wajifunze kujali muda, wajifunze kufanya kazi vya kutosha, waache uvivu, waache kubagua kazi eti hizi ni za wanaume na hizi ni za wanawake tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni kwa kiasi gani Wizara hii imeweka mipango ya kubadilisha mtazamo wa wananchi, bila mabadiliko hatuwezi kupata maendeleo ya jamii ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza juhudzi zinazofanywa na Serikali juu ya kukataza mila zenyekuleta madhara kama vile ukeketaji ndoa za utotoni. Elimu inatakiwa itolewe kwa kiasi kikubwa kwani baadhi ya jamii na hasa wanawake wenyewe huamini katika mila zao, hivyo kuona umuhimu wa kutekeleza mila hizo mfano ukeketaji, wapo baadhi ya wanawake wenyewe huona ulazima wa kukeketwa ili wajione wamekamilika kuwepo katika jamii yao. Serikali iendelee kufuutilia na kutoa elimu ya kutosha kwa jamii ili mila zote potofu au zenyekuleta madhara zitokomee kwa kushirikisha jamii yenyewe na hili litakuwa rahisi tu kama wananchi wameelimika vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu na mafunzo, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ni vichache na bado vilivyopo havipatiwi pesa ya kutosha. Vipo pia vyuo vingi vilivyotelekezwa, nashauri Serikali ivifufue na udahili wa watu wengi amba watasaadida jamii kulingana na ujuzi uliopatikana. Vivyo hivyo ujuzi unaopatikana ungepunguza umaskini kwani kwa ufundi stadi mbalimbali unaweza kusaidia kujajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vifo vya wanawake katika uzazi. Bado wanawake wengi wanakufa wakati wa *process* nzima za uzazi. Katika wanawake mia moja wanaojifungua wanawake hamsini na nane hufa. Bado idadi hii ni kubwa, Serikali

iangalie hili suala kama vita ili ichukue haraka hatua madhubuti ya kupunguza na kutokomeza kabisa vifo vyta uzazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifo vyta watoto wachanga, sababu za vifo hivi ni nyingi, wapo wanaokufa mara baada ya kuzaliwa, wengi hufa kabla ya kufikia miaka mitano kwa kukosa lishe, chanjo mbalimbali na ugonjwa wa malaria. Juhudi ziongezwe ili kunusuru maisha ya watoto ambao ndio Taifa lijalo la Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mimba za utotoni. Natambua Wizara imejitahidi kuhakikisha kuwa mimba za utotoni zinakomeshwa lakini tatizo bado linaendelea na matokeo yake watoto wengi huacha shule. Hivyo ni vema Serikali ione umuhimu wa kuwaacha watoto wanapojifungua warudi shulen. Binti akielimika atamtunza vema mwanae na si rahisi arudie kosa. Hivyo hata watoto wa mitaani watapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie Taasisi za wake wa Marais. Imekuwa ni kawaida kuwa Rais anapoingia madarakani, Mke wa Rais huanzisha taasisi ambayo anaitumia kupata fedha ambazo ni za kusaidia wanawake, watoto na jamii nzima. Lakini kasoro inaonekana pale ambapo kila mke wa Rais anapoanzisha taasisi yake. Kwa nini isiwepo taasisi moja ambayo itaendelezwa na kila mke wa Rais anapoingia madarakani. Tuangalie Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*), mke wa Rais aliyepita ameondoka na taasisi yake. Sasa mke wa Rais wa sasa nae ameanzisha Mfuko wake *WAMA*. Ni dhahiri naye akiondoka ataondoka na taasisi yake. Hii si sahihi, kama ni lazima wake wa Marais wawe na taasisi zao basi iwe taasisi moja endelevu ikirithiwa na kila *First Lady* atakayeingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ianzishe *Bureau of Gender* kama zilivyo *Bureau of Standards*. Ambapo kazi ya taasisi hiyo ya kujitegemea iwe ikisimamia masuala ya usawa wa kijinsia katika sekta zote na nyanja zote. Hii itasaidia kuondoa aina yoyote ya ubaguzi wa kijinsia na itahakikisha usawa (wa namba) idadi ya wanawake na wanaume katika nafasi mbalimbali za kazi katika sekta zote.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazo zuri kuamua kuwa na sheria ya mtoto, ambayo kwa kiasi kikubwa itasaidia kuangalia watoto hasa haki zao, lakini mpaka sasa kanuni bado. Kwa nini ionekane ni muhimu kuanzisha, kuleta sheria Bungeni na kuitishwa lakini kanuni zichelewe. Serikali iharakishe kanuni ili sheria ikamilike na ianze kutumika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukatili na unyanyasaji bado ni tatizo Tanzania, bado watoto wanabakwa, wanawake wanapigwa na wengine kukosa viungo mwilini, wengine hipoteza maisha kwa vipigo. Jamii ya wale mavu nayo inapitia hatua ngumu kuishi kwa kukata tamaa na woga, hasa wenye ulemavu wa ngozi. Napongeza hatua zinazofanywa na Serikali kuzima ukatili kwa watoto wenye ulemavu na wale wenzetu wenye ulemavu wa ngozi, sheria ichukue mkondo wake ili jamii ikome tabia ya unyanyasaji wa kijinsia, ukatili na uuaji wa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kipato cha mtu katika kila kaya ni kidogo sana. Hivyo husababisha watoto kutopata lishe, malazi, mavazi, matibabu na malezi bora kwa ujumla, mbaya zaidi baadhi ya wazazi hutumia watoto wao kuombaomba mitaani. Matokeo yake watoto wadogo wanakosa haki ya elimu, wengine hujiingiza kwenye biashara za ukahaba, madawa ya kulevyta na wengine kufanya kazi mbalimbali katika umri mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya ndoa yanayopelekea wazazi kutengana husababisha watoto kuathirika, Sheria ya Ndoa imepitwa na wakati, iletwe ili irekebishwe, mfano matunzo ya mtoto, kipengele hicho kinasema baba atatoa matunzo kwa kutoa shilingi mia moja kwa mwezi, hiki ni kiasi kidogo sana kimepitwa na wakati iletwe ifanyiwe marekebisho. Ili watoto wapate mafunzo kulingana na wakati uliopo, ili tupunguze madhara ya kuongezeka kwa watoto wa mitaani na madhara mengine yawezayo kuwapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya wanawake, nafurahi wanawake wana benki yao sasa, lakini Serikali ina mikakati gani kuhakikisha benki hii itawanufaishaje wanawake wa vijiji?

Mheshimiwa Naibu Spika, *Presidential Trust Fund*, Mfuko wa Rais wa kuwawezesha wananchi, Mfuko huu bado haujamnufaisha Mtanzania, bado Mfuko huu unatoza riba kubwa kuliko hata benki, kiwango cha riba ni 30% kwa mwaka ikiwa ni 2.5% kwa mwezi. Serikali iangalie jinsi gani itapunguza riba hiyo ili waweze kukopa, watu wengi jinsi gani itapunguza riba hiyo ili watu wengi waweze kukopa bila kuogopa riba ili wajikwamue kimaisha na kujipatia maisha bora.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii na kuwasilisha kwetu. Serikali inatambua asilimia kubwa ya Watanzania zaidi ya nusu ni wanawake na watoto. Wizara hii imepangiwa bajeti ndogo sana ambayo haiwezi kukidhi mahitaji makubwa sana kwa makundi haya. Inasikitisha kuona kwamba bajeti ya mwaka huu 2010/2011, ni pungufu kwa zaidi ya bilioni 3.1 ya bajeti ya mwaka 2009/2010. Wakati watoto wanaongezeka kila leo, matatizo ya wanawake yanaongezeka kila kukicha, mahitaji ya huduma yanaongezeka tena kwa *speed* kubwa kwani idadi ya watu inaongezeka kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa mitaani ni tatizo kubwa hapa Tanzania na linaongezeka kila siku. Inasikitisha maisha wanayoishi watoto hawa huko mitaani, ni lazima Serikali ichukue juhudhi za dhati kupambana na hali hii. Watoto wa mitaani wanakosa malezi na maadili ya kijamii, wanajifunza tabia za kinyama na baadaye tunapata wezi, wavuta bangi, wabakaji, wauaji na kadhalika. Usiku wanafanyiana vitendo vichafu ambavyo havifai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri atueleze uongozi wa Serikali za Mitaa kuanzia Vitongoji, Vijiji, Kata na kadhalika, wanashirikishwaje kwenye suala zima la kuondoa watoto wa mitaani?

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wanaofanyiwa matendo ya kinyama kama ya kubakwa kuuawa na kadhalika inasikitisha sana sana. Tabia hii inayofanyiwa na wanaume wasiokuwa na maadili na wengine kwa tamaa za kutaka utajiri kwa imani za kishirikina, Serikali ionyeshe nguvu yake na mkono wake wa kuondoa kabisa matukio haya. Watoto wasiokuwa na hatia miaka mitatu, miaka mitano, miaka saba, miaka nane anabakwa kwa kweli inaumiza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana Serikali inapitia mlolongo mrefu kuchukua hatua kwa wale wanaofanya matendo hayo. Watoto sita wamebakwa na kuuawa, leo ni mwezi wa tatu bado suala liko Mahakamani hadi lini? Hili lilikuwa suala la *emergency case*. Suala la mtoto siyo suala la kufuata mlolongo mrefu kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kwa haraka kuweka utaratibu wa kumaliza kwa haraka *case* za watoto kwa kupitia Mahakama maalum kama iliyoshughulikia mauaji ya albino hapa nchini. Watuhumiwa washughulikiwe haraka ili kutoa mfano kwa wale wengine wote wanaowaza upuuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazazi na walezi wanaowanyanya watoto wao, matukio ya watoto wanaonyanya na wazazi, walezi yanaongezeka kila siku, jambo la ajabu mengi yanaibuliwa na vyombo vyahabari, swali la kujiuliza hadi atokee msamaria mwema atoe taarifa katika vyombo vyahabari inakuwa ni muda mrefu na watoto wanakuwa tayari wameathirika, kwa maana hiyo wapo watoto wengi wanaoteseka bila kutambuliwa huko waliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iandae utaratibu wa kila Mwenyekiti wa Kitongoji kuratibu habari za watoto, Maafisa Maendeleo ya Jamii waongezwe katika kila Kijiji waweze kuwa jirani na watoto na akinamama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mzazi yejote au mlezi anayeonekana kutesa mtoto awe wake au siyo wake achukuliwe hatua zinazostahili haraka ili kukomesha tabia hizo kwa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Wanawake Wilayani umekosa ufanisi kwa sababu ya kukosa usimamizi mzuri kutokea kwenye Halmashauri husika. Fedha hizi zinapungua kila mwaka, mwaka 2006/2007 Wilaya 70 zilipata mfuko huu. 2007/2008 Halmashauri za Wilaya zilizopata ni 23 mwaka 2008/2009 Halmashauri za Wilaya zilizopata 19 na mwaka 2009/2010 Halmashauri za Wilaya zilizopata ni 28.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isaidie na kuwezesha mashirika yasiyokuwa ya Serikali yanayosaidia kutetea haki za wanawake na watoto, yapo mashirika yanafanya kazi kubwa sana mfano, *MEWATA, TAWLA, TAMWA, FEWATA*, pia *International* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua mchango wa mashirika haya kwa kuwasaidia wanawake, kuwaelimisha wajue haki zao, kufanya tafiti mbalimbali na

kuibua matatizo yanayoyakumba makundi haya, ili waweze kufanya zaidi na wasaidie kundi kubwa zaidi, Serikali iweke nguvu yake pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafuutiliae kuhakikisha vituo vya kulea watoto yatima vinatoa huduma nzuri kwa watoto hawa? Wapo watoto wanaokosa kusoma na huduma nyingine za msingi.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba yao nzuri iliyojaa busara na umahiri wa kiutendaji hasa katika kufanikisha malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze masikitiko yangu makubwa kutokana na matendo ya ubakaji na uuaji wa watoto, naelewa kwamba Serikali inajitahidi kupambana na ukatili huo lakini wimbi la matendo hayo linaongezeka siku hadi siku, kwani takwimu halisi zinaonyesha hivyo. Je, ni kwa nini ama adhabu zinazotolewa hazitoshelezi kuwafanya wahusika kukoma kwa kuogopa kuendelea na ukatili huu wa kinyama?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuongeza juhudhi za makusudi ili kukomesha matukio haya, kwani tegemeo kubwa la mzazi ni mtoto wake na mtoto ndio Taifa tunalotegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukura nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kusimamia mchakato wa uanzishaji wa Benki ya Wanawake ila naomba sana Benki hiyo ifungue matawi yake katika maeneo mbalimbali huko Mikoani na Wilayani ili kuwasogezea karibu wanawake walio vijijini huduma hii ili waweze kufaidika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali iendelee kutilia mkazo suala la watoto wa mitaani kwani badala ya kupungua linaongezeka siku hadi siku. Je, Serikali imefikia hatua gani katika kupambana na tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mimba za utotoni ni jambo ambalo bado linaendelea kukua kwa kasi kubwa pamoja na juhudhi zinzochukuliwa na Serikali. Hivyo nashauri kwamba, wanaopatikana na hatia kwa kuwapa mimba watoto basi wapewe adhabu kubwa ili vitendo hivi vya kuwadhalilisha watoto pamoja na kuwapa maambukizo ya UKIMWI. Jambo hili ni kubwa na ni tatizo kwani linachangia ongezeko la watoto wa mitaani na omibaomba, jambo ambalo linaliingiza Taifa letu katika fedheha.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni mionganini mwa Wizara muhimu sana kwa ustawi wa watu wa Taifa hili. Ni Wizara ambayo inasimamia utangamano baina ya jinsia mbili lakini pia malezi na maendeleo ya mtoto wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunapaswa kuelewa kwamba jukumu hilo si la Wizara hii peke yake bali ni jukumu la kila mwananchi wa Taifa hili, tuna wajibu sote kuona kwamba watoto wa nchi hii wanapata malezi yanayofaa na kadhalika ili kuleta usawa mionganoni mwa jinsia ya kiume na kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nigosie kidogo suala zima la malezi ya watoto yatima, watoto walio katika mazingira hatarishi na watoto wa wanaozurura mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya wananchi ambaao wana huruma juu ya watoto yatima na ambaao wanachukua hatua mbalimbali za kuwaenzi watoto hao, ni dhahiri pia kwamba kuna baadhi ya wahisani ambaao nao pia huchangia fedha kuwapa msukumo wale wananchi au *NGOs* ambaao wanajihuisha na ulezi wa watoto yatima. Lakini kumejitokeza baadhi ya watu na *NGOs* ambaao hawana nia njema juu ya suala zima la ulezi wa watoto yatima. Wamekuwa wanapokea misaada mbalimbali kwa ajili ya watoto yatima lakini wanaitumia misaada hiyo kwa shughuli zao binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, umefika wakati kwa Serikali sasa kufanya tathmini ya kina kubaini ni nani hasa analea watoto yatima kwa nia njema na kwamba misaada wanayoipata inatumika ipasavyo. Hawa wapewe kila aina ya msaada kuwapa nguvu na kuwatia moyo, lakini watakaobainika wanaitumia misaada ya watoto yatima kwa shughuli zao binafsi wachukuliwe hatua kali sana. Na zile *NGOs* zinavyofanya hivyo zifutwe kabisa na zenyewe kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa hasa katika miji mikubwa la watoto wa mitaani, sote tunafahamu sababu zinazopelekea kuongezeka kwa watoto hawa. Bahati mbaya watoto hawa wanakumbwa sana na matatizo kadhaa ya unyanyasaji. Aidha, watoto wa mitaani nao wamekuwa ni kero na adha kubwa katika miji yetu. Wamekuwa omboomba wakubwa wanaleta sura mbaya kwa wageni wanaotembelea nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiliangalia tatizo hili kwa undani zaidi utalionaa linamgusa kila mtu, mzizi mkubwa ni lile la familia husika kutokujibiki, jamii inayozunguka watoto hawa kujifanya hawawajibiki na Serikali nayo kwa upande mmoja kulifumbia macho kana kwamba haina wajibu juu ya suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ili kuondokana na tatizo la kuwepo kwa ongezeko kubwa la watoto wazururaji (watoto wa mitaani) lazima tuanzishe mjadala wa Kitaifa kubaini hasa changamoto zinazokabili tatizo la watoto wa mitaani kuainisha hatua za kuchukua na la msingi zaidi kubainisha kila mtu wajibu wake katika kulikabili tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Benki ya Wanawake limezungumzwa na wengi, ni jambo zuri sana katika ukombozi wa mwanamke wa Kitanzania. Lakini pamoja na kwamba ni muda mfupi sana tangu Benki hii imeanzishwa dalili za wazi zinaonekana kwamba inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kilio karibu kila mtu anataka Benki hii ipeleke matawi yake huko Wilayani na Vijijini. Hili ni jambo zuri na busara lakini naiomba Serikali kabla ya kusambaza matawi kila kona ya nchi hii, ni lazima tathmini ya kina ifanyike ili kuona kwamba ustawi wa Benki unaimarika kwa manufaa ya maendeleo ya Benki yenyewe lakini pia kwa manufaa ya mwanamke na Mtanzania kwa ujumla.

MHE. BAKAR SHAMIS FAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamii ya Watanzania kwa muda mrefu tulikuwa tunaishi bila matatizo ambayo kwa hizi siku za karibu pamezuka mambo mengi ambayo kwa kweli yaliitikisa nchi, mauaji ya watoto, wanawake nna kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto ndio viongozi, tegemeo na hata wazalishaji na kukuza uchumi wa nchi. Watoto wa mitaani wanazidi sana hasa ndani ya Miji kama vile Dar es Salaam na ndani ya Miji ya Mikoa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifarakano, mimba za utotoni, wazee (baadhi) kutojali watoto wao na hata baadhi ya mila na tamaduni za baadhi ya makabila ni chanzo na chachu ya kuzalisha watoto wa mitaani. Swali je, Serikali inao mpango gani mahususi ama wa muda mfupi au mrefu wa kuondokana na adha hii ya watoto wa mitaani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa jinsi gani Serikali itasaidia kuwakumbusha wazazi ambao wanakataa kubebe majukumu yao ya ulezi wa watoto wao.

MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuwapongeza tena Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampeni ya Kataa Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto: Je, lile gari linaendeleaje na matembezi ya Mkoa hadi Mkoa?

Mheshimiwa Spika, nilisahau kuliongelea nilipochangia kwa kuongea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gari la sinema, Wizara imekuwa ikitumia gari la Sinema kutoa mafunzo kwa njia ya sinema. Hivi karibuni lilitumika kutoa mafunzo kwa jamii ya kupinga ukatili wa kijinsia, watoto na albino katika Wilaya za Shinyanga, Bukombe na Bariadi. Aidha, limetumika katika kutoa mafunzo kama hayo kwa Wakuu wa Vituo vya Polisi kutoka Wilaya za Mikoa ya Kanda ya Ziwa inayojumuisha Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, na Viongozi wote wa Wizara hii na Taasisi zake, kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri na kukupa ufanuzi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, ninashauri Viwanda kuboreshwa kuwa na mfumo wa *VETA* Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imeahidi kuwa na vyuo vya *VETA* kila Wilaya na kwamba pale ambapo viro Vyuo vya Maendeleo basi vingewenza kuunganishwa na kuboreshwa kuwezesha kuwa *VETA* Wilaya: Je, ni maandalizi gani ambayo yameanza kufanyika ili kukiboresha Chuo hicho kufikia uwezo wa *VETA* Wilaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Maendeleo kutoka nchi ya *Sweden*, ilioa kwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Viwanda kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, mashine moja ya kuzalisha Umembe (*Windmill*) mwaka 2008. Kwa kuwa Chuo kilitakiwa kugharamia kuweka mfumo wa waya za umeme ndani ya Chuo na kufungwa kwa mashine hiyo ilitarajiwa gharama hizo ziwekwe katika Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Tatizo dogo lilijitokeza ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Muheza haikupokea kwa wakati *Battery* za *Solar* kwa ajili ya kuendesha mfumo huo na inawezekana kuwa ndio sababu ya kucheleweshwa kufungwa kwa mashine hiyo hadi sasa zaidi ya mwaka mmoja na nusu kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wahisani wa *Sweden* wanatushangaa sana kwa kuwa wazito kuwashaa mashine hiyo ya *Windmill* kuanza kufanya kazi na kutoa umeme ambao ungekuwa hauna gharama za ziada za uendeshaji wa kila siku kama vile ununuzi wa Dizeli kuendesha genereta zilizopo pale Chuoni. Je, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto itasaidia viro Chuo cha Maendeleo ya Jamii, kiwanda kutumia fursa hiyo ya msaada wa wa-Sweden? Mimi binafsi wakati huo *Sweden* wanatoa zawadi hiyo, nilinunua *Windmill* ya aina hiyo na nimeifunga Mbagala Zakhem Dar es Salaam na inafanya kazi kinyume na wengi wanavyodhani kwamba Dar es Salaam haina upemo wa kutosha kuendesha *Windmill*.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za *Battery* za *Solar* ni Sh. 300,000/. Ili uweze kuhifadhi nguvu za umeme wa kutosha unaweza kuweka *battery* kumi, hivyo gharama ni Sh. 3,000,000/. Gharama ya kujenga mnara wa kufunga hiyo *Windmill* ni wastani wa Sh. 2,000,000/ na gharama za maboresho ya *Windmill* kukidhi mazingira ya Tanzania ni Sh. 500,000/ na gharama za fundi kufunga *Windmill* hiyo haizidi Sh. 1,500,000/. Taa za *Solar power* kwa madarasa na mabweni (Wastani 20) Sh. 400,000/. Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ilikuwa tayari kusaidia kiasi kuwezesha kufungwa kwa *Windmill* hiyo ili pia iweze kutoa huduma katika Zahanati ya Kiwanda. Nashauri kuwepo na uhusiano wa karibu ili hayo yatekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima wa afya na kutujalia kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Timu yake kwa kazi nzuri na usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio rahisi wanawake kukaa sehemu moja kusitokee malumbano, lakini katika Wizara hii Watendaji Wakuu wote ni wanawake, lakini mambo yao poa na wanastahili pungezi na hakuna malumbano.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara muhimu na inamgusa kila mmoja weu tuliomo ndani ya ukumbi huu na walioko nje ya ukumbi huu lakini bajeti yake bado hairidhishi ni fedha kidogo sana imepangiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali katika bajeti zijazo kuipatia fedha zaidi hasa kwa vile Wizara hii ni mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika muhula huu imetuletea sheria ya mtoto na kufafanua vipengele mbalimbali vya kumlinda mtoto na kutoa vifungu vya adhabu kwa watakaokwenda kinyume, lakini hivi sasa kuna wimbi kubwa la watoto wa kike kubeba mimba wakiwa mashulen na kuwakatisha masomo watoto hao. Ninaimba Wizara ilete Muswada Bungeni au itungwe sheria kali ya kuwaadhibu wanaowapa mimba watoto ili kukomesha tatizo hilo, kwani idadi iliyopo inatisha na ikiachwa hivi hivi Taifa litakuwa na watoto wengi wa mitaani ambalo ni aibu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nizipongeze sana *NGO*'s zinazofanya kazi na Wizara hii kwa misaada ya hali na mali wanayotoa kwa kuisaida Wizara kutekeleza majukumu yake. Naiomba ziendelee kuisaidia Wizara ili ilete ufanisi zaidi. Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. MWANAWETU S. ZARAFI: Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Mheshimiwa Jakaya Kikwete naomba ziwafikie vikundi vidogo vidogo vya maendeleo Wilayani na hata Vijiji. Wizara iwe mbele juu ya usimamiaji na uhakiki wa fedha hizo kuwafidia wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, maafisa wa maendeleo ya Jamii wavezeshwe ili waweze kukaa katika Kata wanazopangiwa. Imekuwa ni desturi kwao kukaa mijini kusubiri wapangwe katika miradi tu inayoletwa ndani ya Halmashauri badala ya kwenda katika Kata zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana kwa kuvikumbuka vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, kwa ukarabati na hata kuviona na kuvifanya vionekane hai, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hongera Wizara, kwani kwa hakika vikundi vingi vya kimaendeleo vimeanzishwa kwa kipindi hiki.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipongeze kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa bajeti hii na kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Hata hivyo, nina maeneo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ni muhimu sana katika Sekta ya Maendeleo ya Jamii nchini. Vyuo hivyo ndivyo huzalisha wataalam ambao huenda Wilayani na Vijijini kusimamia sekta hiyo. Hata hivyo, Vyuo hivyo vinatengewa pesa ndogo sana kwa shughuli za maendeleo na hivyo kuvinyima fursa ya kufanya shughuli zake kwa ufanisi. Aidha, majengo ya vyuo vingi vya Maendeleo ya Jamii yako katika hali mbaya sana.

Je, Serikali kupitia Wizara hii itakuwa tayari kutenga pesa zaidi kwa shughuli za Maendeleo ya Vyuo hivyo? Pili, kuna mpango gani wa kukarabati majengo ya vyuo hivyo ili wakufunzi na wanafunzi wapate mahali pazuri pa kufanya shughuli zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili limeshatunga sheria inayosimamia haki za watoto. Napenda kujua kama Kanuni zinazosimamia utekelezaji wa sheria hiyo, zimeshatungwa. Nataka kujua hilo maana kuna tatizo la ucheleweshaji utungwaji Kanuni na hivyo sheria ambayo inakuwa imeandaliwa kwa muda mrefu, kushindwa kuanza kutumika mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutungwa sheria inayosimamia haki za watoto, lakini bado vitendo vya kuwanyanya watoto vinaendelea. Bado jamii haijatambua wajibu wake katika suala la kuwalinda, kuwalinda na kuwatunza watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba Wizara izidishe kasi zaidi ya kusimamia masuala ya watoto. Pili, Wizara iwe na mpango mkakati wa kuwa na vipindi mbalimbali kwenye magazeti, televisheni, mikutano ya kuelimisha umma ili ijue kwamba suala la kuhudumia, kusimamia na kulinda haki za watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu/hatarishi ni la Jamii yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado ziko mila mbaya nchini mwetu hadi leo. Mila hizo ni kama vile ukeketaji, kurithi wajane na wanawake kuoa wanawake, (wenzao hasa mkoani Mara). Mila ya kumkeketa mwanamke ni mbaya sana, kwani huhatarisha uhai wa mkekewaji na wakati mwingine kufa kwa kuvuja damu anapokeketwa.

Pili, ukekewaji humnyima mwanamke aliyeketwa kufurahia tendo la ndoa vizuri maana moja ya kiungo muhimu sana kinakuwa kilishaondolewa. Aidha, wanawake kadhaa waliokekewa hupoteza maisha wakati wa kujifungua kwa kuvuja damu nyingi kwa kuwa maumbile yake ya asili yanakuwa yalishaharibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kurithi wajane na wanawake kuoa wanawake wenzao ni mila za kizamani sana (*outdated cultures*). Mila hizo mbaya kwa sehemu kubwa sana husababisha maambukizo zaidi ya Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu hapa ni kwamba, Wizara iendelee na jitihada zake za kutoa elimu kwa umma kuhusu athari kubwa na mbaya sana kama nilivyoeleza hapo juu.

Pili, pale ambapo elimu inayotolewa inakuwa haizingatiwi, basi Wizara ichukuwe msimamo mkali wa kuwafikisha kwenye vyombo vyia sheria wale wote ambao hawataacha kuendela kuenzi mila hizo mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa hotuba nzuri yenyewe kueleweka. Kwa kweli kwa muda wa miaka mitano hii Wizara imeboreka na kuimarika, yakiwemo mambo yafuatayo, kama vile kuletwa/kupitishwa Muswada wa Sheria ya Haki za Watoto, Mkataba Itifaki uliotolewa wa nchi za SADC kuhusu wanawake, kama vile ubakwaji, unyanyasaji ambao uliletwa Bungeni na kuridhiwa pamoja na mikakati ya wanawake ya kuingizwa kwa asilimia 50 kwa 50 katika vyombo vyote vyaa maamuzi. Vile vile kwa kuboreshwa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii katika kutoa fani mbalimbali za mafunzo na ujuzi, pia na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunashukuru kwa miaka hii mitano kila mwaka bajeti inaongezwa. Hata hivyo kuna haja ya kuongezwa zaidi bajeti ya Wizara hii kwani ni Wizara ambayo inaunganishwa na masuala yote ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muswada wa Sheria ya Ndoa na Mirathi ufanywe haraka, uletwe Bungeni, pia Wizara izidi kuchukua hatua kali kwa wanaume ambaao wanawapiga wake zao mpaka kuwaua na pamoja na wazazi ambaao wanaua watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naitakia Wizara kila la kheri na mafanikio mema.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mama Sitta pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Nkya kwa kazi zao nzuri wanazozifanya, kwani hii ni Wizara nyeti sana na inayohitaji kufanya kazi bila kuchoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Wizara hii kuwa na mambo mengi, mimi napenda hasa kushauri, huu msongamano wa watoto ombaomba katika majiji yetu na miji pia hii ni hali mbaya na ni hatari sana, kwani wamo watoto ambao wako chini ya umri wa miaka 10, na wengi wao ni watoto wa kike, najua suala hili ni gumu, lakini ni vyema mkajipanga vizuri katika mpango mfupi, wa kati na mrefu ili kutokomeza hali hii ambayo haipendezi na wala haina tija kwa watoto wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni vizuri kama Mheshimiwa Waziri akajua pamoja na Bajeti ya akina mama wajawazito kupelekwa katika Wizara ya Afya, lakini watesekao ni wanawake ambao ndio kundi kubwa ambalo lina kazi ngumu kama sote tunavyozija.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la ubakaji wa watoto ambao unaendelea kwa kasi hasa katika Mkoa wa Morogoro, ambapo watoto 83 wamebakwa, hivi wabakaji hao wanatoka wapi? Ni kwanini kasi hii inaendelea? Ni lazima sasa tuchukue hatua na sauti ya Wizara, sauti ya Mheshimiwa Waziri ni sauti ya wazazi, nasi tuko nyuma yake. Maoni yangu ni kwamba wabakaji hawa ni bora wakahasiwa, kwani ni waharibifu sana, na kama tukisema tutakiuka haki za msingi, hata wao wabakaji wanakiuka haki za msingi kwa kuwabaka watoto na kuwalawiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tanaomba watu ambao wanawapa mimba watoto ambao ni wanafunzi ambao hawajafikia kujua lipi zuri na lipi bayu, nao wachukuliwe hatua kali ili tuweze kupunguza mimba za utotonu. Pia kuwaelimisha wasichana ambao wana miaka 18 ambao ni wanafunzi na wasio wanafunzi kuwa mimba kabla ya ndoa ni hatari, na wale wanafunzi wahamasishwe kusoma sana na kuja kuwakomboa wanawake waache kujishirikisha na ngono hasa ngono zembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu ni kazi kubwa na itachukua muda mrefu ili kutekelezeza, lakini Wizara na wazazi tukiwa wamoja tutafanikiwa. Ahsante.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto yatima Kongwa ni wengi na wanaongezeka kwa kasi. Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa na mimi Mbunge tunazidiwa. Ustawi wa Jamii hawana cha kufanya, naomba Maendeleo ya Jamii waliangalie suala zima la watoto waishio katika mazingira magumu, uyatima na umaskini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wajane, maskini vijijini, wana taabu kubwa sana ya kulea watoto na kuwasomesha elimu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza nafasi na fursa za wanawake katika uongozi, naomba suala hili lisiwe kwa Wabunge na Madiwani, na DC, Ma-RC na kadhalika. Naomba iwe ni *across the Board* kwa Serikali nzima. Kuanzia Watendaji wa Vijiji, Kata, Wilaya, Mikoa hadi Wakurugenzi wa Idara ndani ya mawizara.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri katika Wizara hii. “Kweli wanawake tunaweza. Tupeni nafasi.”

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuzungumzia kuhusu unyanyasaji wanaofanyiwa wanawake. Wanawake wananyanyasika kiasi kwamba wengine hupoteza maisha yao. Ni leo tu katika vyombo vyya habari tumesikia askari mwanamke amejua kwa kujipiga risasi kichwani baada ya kupoteza msafara wa Rais. Hivi kweli inawezekanaje mtuhumiwa anayeingizwa mahabusu akaingia na silaha? Ni dhahiri kuwa mtuhumiwa yejote anayeingizwa mahabusu huwa ananyang’anywa vitu

vyote alivyonavyo hata mkanda pia.
mpaka kufikia kujiua mwenyewe?

Iweje askari huyo aachiwe na silaha

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala lingine la wanawake kunyanyaswa na waume zao kwa vipigo na hatimaye kuuwawa. Hii hupelekeea hata mume mwenyewe kujiua kutokana na kifo cha mkewe. Serikali ichukue hatua madhubuti kwa ajili ya hawa wanaume wanaowanyanya wake zao hatimaye kuwasababishia vifo na mwisho kubaki na watoto wa mitaani wengi ambaa mwisho wa yote hugeuka vibaka, majambazi, kutokana na hali ngumu ya maisha kwa upande wao na pia kukosa malezi bora.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanywa. Pamoja na bajeti yake kuwa ndogo sana haitoshi kwa matatizo makubwa sana, naomba nami kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watoto wa shule mbili za walemavu, Nageza Viziwi pamoja na Mseto, wote wako sehemu moja, pamoja na Tumaini. Hawa watoto wana matatizo makubwa. Naomba Wizara ijitahidi kuwasaidia, kuwatemebelea mara kwa mara. Uwezo wa Manispaa peke yake haiwezi kusaidia kwa kuwa Wizara hii ina wamama, nina uhakika ombi langu litasikilizwa, tutaendelea kuwaomba kurudi nafasi hii kumalizia maombi yetu tunayoyaomba.

Matatizo ya watoto wanaozurura mitaani, kuna Mikoa mingine wanatia aibu, wanazagaa usiku hasa Mkoa wa Mwanza. Je, Wizara pamoja na Serikali inaonaje kuwajengea kituo rasmi kuwaweka sehemu wakapewa elimu kupunguza ujambazi na tabia mbali mbali wanazofundishana? Ni nyingi sana, mfano madawa ya kulevyta, bangi hata wafanyabiashara wanawatumikisha kuuza madawa ya kulevyta. Kwenye TV wiki iliyopita nimeona kuna shule ya watoto walemavu wa ngozi, ni taarifa ya kusikitisha kuwa wazazi wao wamewatelekeza kuanzia matumizi na kutowatembelea. Je, hilo Wizara inalijua au hapana?

Je, sheria ya haki za mtoto imeishasambazwa Mikoa yote? Kwa sababu vitendo vya ukatili vinazidi na wale wanaofanya vitendo hivyo sijasikia adhabu wanayoipata, tunaona kila siku kwenye TV mara mtoto anapigwa, mwingine anakatwa na viwembe, wanashindwa kwenda shule, vyombo vya habari wanaonyesha matukio hayo: Je, mbona hawaonyeshi mwisho wake wanaofanya vitendo hivyo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo wanavyofanyiwa wanawake huko vijijini wananyanyasika sana. Ofisi za Ustawi wa jamii rushwa imetawala, akifungua kesi mwanaume akiitwa anatoa pesa na mama huyo anabaki kupigwa danadana mwisho wake mama huyo anakata tamaa anaendelea kunyanyasika. Ombi langu ni kwamba watu hao wasiwe wanakaa kwenye kituo zaidi ya miaka mitatu, ni matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pamoja na kushauri kwamba benki zipelekwe kwenye Mikoa hasa matawi yake, kwani wanawake wengi wanajitahidi kufanya biashara hata wazazi wanajua. Wanaopata shida ni wanawake na wanaokuwa masikini zaidi ni wanawake. Ukiangalia asilimia kwenye mkopo wanaorejesha haraka ni wanawake, usione wanawanyanyapaa kuwakopesha mikopo ya JK wanawake kwenye Wilaya

hawakupewa, kila siku wanalamika, haziwafikii hata huko vijiji. Naomba Wizara ijitahidi kuzunguka kuwasaidia. Wanawake ukilinganisha na kwa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza na kuingia soko la pamoja, mategemeo mengi na mchango mkubwa ni wanawake. Nina uhakika tukiwa karibu nao kuwasaidia, nina uhakika hata uchumi wa nchi utakua kupitia kwa wananchi na kupunguza umasikini. Wanawake wanaweza.

Mheshimiwa Naiibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yake. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mikakati gani ya kuwaendeleza Maafisa Maendeleo ya Jamii hata kitaaluma na kuwapatia vitendea kazi pamoja na kuboresha maslahi yao na usafiri wa pikipiki na magari Wilayani Mpwapwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mikakati gani ya kuboresha mazingira ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chisalu Wilayani Mpwapwa kwa kupanua Chuo hicho (kuongeza majengo) ili kuongeza idadi ya udahili wa wanafunzi wa fani mbalimbali pamoja na kuanzisha mafunzo ya Diploma ya Maafisa Maendeleo ya Jamii ili kuongeza idadi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii kwenye Kata?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia gari jipya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chisalu Wilayani Mpwapwa? Pili, kupeleka Umeme katika Chuo hicho na kupeleka Kompyuta ili Wanafunzi wajifunze masomo ya Kompyuta? Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua trekta lililopo ili litumike katika kilimo Chuoni hapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chisalu Wilayani Mpwapwa? Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii ya bajeti na kwamba sambamba na hotuba hii, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Timu yake. Hata hivyo, ninaomba kupata ufanuzi juu ya masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake ni chachu muhimu ya kuwakomboa wanawake kiuchumi, hivyo, kusaidia kuleta maboresho na maisha bora kwa jamii ya Watanzania.

Je, ni kwa mpango gani Benki hii itawawezesha wanawake wanaoishi vijiji kupata fursa ya kusaidiwa kupitia benki hii au siyo mpango wa kuwawezesha zaidi akinamama wa mijini na kuwaacha wa Vijiji?

Mheshimiwa Naibu Spika, nini mkakati wa kumkomboa mwanamke na hasa wa kijijini kupitia Taasisi hii ya fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, wasichana wanaopata ujauzito wakiwa shulenii hawapewi fursa ya kuendelea na masomo. Je, ni lini Wizara hii itasaidia kuwapatia fursa wasichana waendelee kupata elimu kama Watanzania wengine pasipo kubaguliwa? Kwani ujauzito ni tendo lisilo la kutarajiwa au kupangwa na hasa kwa wasichana wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa kama nilivyosema tutawaita watoa hoja waanze kujibu baadhi ya hoja, kwanza namwita Mheshimiwa Naibu Waziri atapewa dakika zake 15 halafu Mheshimiwa Waziri dakika zake 25 na dakika hizo hatuzihesabu wakati wa kutaja majina. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha leo kuwa hapa katika Bunge lako Tukufu tukiwa na afya njema na wazima wa akili. (*Makofi*)

Pili, napenda nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ili nichangie hoja ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, aliyoiwasilisha leo hii asubuhi hapa Bungeni. Aidha, ningependa nikupongeze wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha Bunge hili na shughuli zote za Bunge hili kwa ufanisi mkubwa na kwa umahiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii nimshukuru sana Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani yake kwangu kwa kuwa aliniteua kuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Aidha, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuchukua fomu ya Urais, namwombea afya njema na ushindi wa kishindo. Napenda pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri ambaa amekuwa anatuongoza kwa mfano zaidi kuliko kutukemea. Mimi naamini kwamba nimejifunza mengi kwake kwa sababu kujifunza ni kuona na kusikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Margaret Sitta, Katibu Mkuu Ndugu Mariam Mwaffisi na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano walionipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Kwa njia ya pekee nawashukuru sana wapiga kura wangu ambao ni wanawake wa mkoa wa Morogoro kwa kunichagua kuwa Mbunge wa Viti Maalum. Ni matumaini yangu kuwa ninatekeleza majukumu yangu kwa ufanisi kulingana na matarajio yao.

Aidha, napenda kuwaambia kwamba nawashukuru sana kwamba nimewatumikia kwa kipindi cha miaka kumi nao wamenisaidia kuwatumikia na sasa hivi naingia

kugombea katika jimbo la Morogoro Kusini Mashariki. Naamini kwamba wanawake tunaweza, nawashukuru kwa kunipa *support* kubwa na naomba waendelee kuniombea na kunisaidia kama walivyoonesha moyo wao wa ushirikiano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia ya pekee namshukuru sana mume wangu Prof. Estomih Nkya na watoto wetu February, George, Jonas, Theresia na Petro pamoja na mjukuu wangu mmoja tu Talia ambao hawachoki kuniombea kila siku pamoja na kunipa ushauri ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa.

Napenda sasa nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao siku zote wamekuwa wanansaidia wakati nachangia hapa Bungeni, wakati ninajibu maswali na wengine wengi wamekuwa wameonesha upendo mkubwa sana katika kuisaidia Wizara yetu kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru wale wote ambao wamechangia hoja kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale ambao walichangia kwa maandishi. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto atawatambua wakati akihitimisha hoja basi mimi sitofanya hivyo kwa sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wa hoja yetu walikuwa wengi mno hivyo naomba nichukue nafasi hii kujibu baadhi ya hoja, majibu yangu yatalenga hoja zilizoelekezwa kwenye eneo la maendeleo ya mtoto. Kwa wale wote ambao sitawezza kujibu hapa kwa sababu muda ni mfupi basi watapata majibu yao kwa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutajaribu kujibu kwa kifupi tu. Hoja ya kwanza inatokana na Kambi ya Upinzani kwa Mheshimiwa Anna Maulidah Komu ambaye aliuliza ni kwa nini shughuli za watoto zinashughulikiwa na zaidi ya Wizara moja yaani Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba mtoto hataweza kushughulikiwa katika eneo moja kwa sababu mahitaji yake ni mengi mno. Ukitisema utamshughulikia kwenye eneo moja basi mahitaji yake mengine yatasahaaulika kwa hiyo utakuwa hujamtendea haki. Hivyo basi mahitaji ya mtoto yanayolenga katika shughuli zote za afya pamoja na lishe na mambo ya ustawi yatashughulikiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inashughulikia suala la kuanda sera, miongozo na mikakati ya utekelezaji kuhusu haki ya mtoto na kuratibu uandaaji wa ripoti za nje na za kikanda kuhusu utekelezaji wa hali za mtoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itashughulika na kuangalia haki ya mtoto ya kupata elimu kuanzia elimu ya awali mpaka elimu ya juu. Sasa hapo katikati kuna Wizara nyingine ambazo zinashughulikia yale mambo ambayo ni mtambuka. Kwa mfano Wizara ya Ulinzi ambayo inaangaliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani, mambo yote ya kisheria yanaangaliwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na

lishe ni ushirikiano kati ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilitoka kwa Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Ibrahim Sanya na Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha. Hoja yao ilikuwa inasema ni vizuri kukawa na mpango madhubuti wa kuwasaidia watoto waliopo mitaani na kuzuia wengine kutoingia katika hatari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusema kwamba suala la watoto wanaoishi mitaani ni tatizo la kijamii. Serikali imeandaa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 inayosisitiza umuhimu wa kuwalinda watoto walio katika mazingira magumu wakiwemo watoto wa mitaani. Hali kadhalika Serikali imeandaa mpango mkakati wa jamii wa kudhibiti tatizo la watoto wanaoishi mitaani na ambao tayari wapo katika mazingira hayo kwa kuwapatia elimu, matibabu, chakula, malazi na mavazi. Lakini msisitizo mkubwa unaelekezwa kwa jamii nzima ya Tanzania kusaidia kuondokana na tatizo hili. Naomba nimshukuru sana mwakilishi wa Kambi ya Upinzani aliyesoma hotuba leo, amesitisiza pamoja na Mheshimiwa Halima Mdee kwamba ni wajibu wa kila mzazi amlee mtoto wake, maana yake ni kwamba wajibu wa kwanza ni familia pamoja na jamii wa kuhakikisha kwamba watoto wanapata mahitaji yao, wasiende mitaani, naomba niwashukuru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu imetoka kwa Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge Jimbo la Fuoni anasema Wizara ilete Muswada Bungeni au itunge sheria kali ya kuwaadhibu wanaowapa mimba watoto ili kukomesha tatizo hili. Sheria ya Makosa ya Adhabu Sura Namba 16 iliyorekebishwa mwaka 2002 inasema; “Mtoto wa umri chini ya miaka 18 hawezi kuridhia tendo la ngono na adhabu inayotolewa kwa wanaume wanaokiuka sheria hii ni kifungo cha maisha au kifungo kisichopungua miaka 30 jela.”

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sheria ipo hapa tunasema kwamba sasa utekelezaji ndio unaotakiwa uwepo pamoja na jamii kufichua haya matatizo na makosa yanapotendeka. Tuache kuficha kwa sababu familia zingine zinaficha haya makosa. Hoja ya nne inatoka kwa Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji na Mheshimiwa Bernadeta Mushashu. Hoja yenewe inasema tatizo la ucheleweshaji wa utungwaji wa kanuni zinazosimamia utekelezaji wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni na taratibu za utekelezaji wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 zimeshaandaliwa na zinakaribia kukamilika. Lakini ningependa kusema kwamba kabla ya sheria hiyo haijatungwa kulikuwepo na kanuni ambazo zilikuwa zinatekeleza zile sheria ambazo zilikuwa zinampa mtoto haki. Hivyo basi ningependa kusema kwamba tunaposubiri ukamilishaji wa hizi kanuni kwa ajili ya hii sheria ya mwaka 2009 basi hizo kanuni ambazo zilikuwepo ziendelee kutekelezwa na ningependa

kusema kwamba Mahakimu wanafahamu na waendelee kutumia hizo kanuni wasiseme kwamba kwa sababu hizi hazijatoka basi wamnyime mtoto haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tano imetoka kwa Mheshimiwa Godfrey Zambi inayosema Wizara inaendelea na jitihada zake za kutoa elimu kwa umma kuhusu athari kubwa ya ukeketaji. Wizara ichukue msimamo mkali wa kuwafikisha kwenye vyombo vyanya sheria wale wote ambao hawataacha kuendelea kuenzi mila mbaya za ukeketaji na kurithi wajane. Ningependa kusema kwamba Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imefanya juhudhi kubwa kutokomeza mila zenye kuleta madhara hususan ukeketaji wa wanawake na watoto wa kike. Hivyo basi kuna mpango kazi wa Kitaifa wa kutokomeza ukeketaji pamoja na mila nyingine zenye kuleta madhara, mpango huu ulianza mwaka 2001 mpaka 2015 pamoja na kwamba tumetayarisha vitini pamoja na vipeperushi vingine ambavyo vinaeleza juu ya makosa ya jinai ambayo yanagusa matatizo yanayodhalilisha watoto wa kike pamoja na wanawake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine imetoka kwa Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah pamoja na Wabunge wengine ambao wamezungumzia ufahamu wa sheria, Serikali iongeze Bajeti ya Wizara ili kuongeza uelewa wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 kwa tafsiri ya Kiswahili na uenezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto kwa lugha ya Kiswahili. Naomba niseme kwamba Serikali imeshatenga Bajeti ya shilingi milioni 38 kwa ajili ya shughuli hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya saba ni je, ni kwa nini ama adhabu zinazotolewa kutokana na matendo ya ubakaji na uuaji wa watoto hazitoshelezi kwa kuwafanya wahusika kukoma kwa kuogopa kuendelea na ukatili huu wa kinyama?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamezungumzia hili, mimi naomba kusema kwamba haya yote yako chini ya Sheria ya Makosa ya Kujamiihana ya mwaka 1998 na napenda nichukue fursa hii kwa niaba ya Serikali niwapongeze viongozi wa dini zote wa Wilaya ya Rungwe kwamba waliandamana pamoja na kufanya sala na maombi maalum kwa ajili ya kupinga kitendo cha kudhalilisha watoto katika Wilaya ya Rungwe na Mkoa wa Mbeya ya kuwabaka watoto pamoja na kuwaua kwa sababu za kishirikina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuhusu watoto wenye ulemavu ambayo imetokana kwa Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji na Mheshimiwa Lucy Owenya inazungumzia kwamba watoto wenye ulemavu wanasaidiwaje ili wapate haki zao? Napenda kusema kwamba watoto wenye ulemavu wanajumuishwa kwenye kundi la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, kwa hiyo, tuna Kamati hizo katika kila kijiji Tanzania Bara kwa hiyo, wanahudumiwa kuititia Idara ya Ustawi wa Jamii ambayo iko chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia watoto ambao wanapata mimba ambao yamezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge watatu. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii iliunda Kamati, imezunguka nchi nzima kuchukua maoni na sasa hivi wameandika ripoti ambayo sasa hivi inasubiri maamuzi ya Serikali. Hoja nyingine inauliza je, Wizara ina mipango gani ya kuwasaidia watoto walio katika ajira?

Naomba kusema kwamba Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, kifungu 77 kinawakataza watoto kutumikishwa katika kazi za hatari hususan sekta ya uvuvi ikiwa ni mojawapo ya kazi za hatari sana na kwenye machimbo na katika shughuli za mashamba. Naomba niseme kwamba Serikali itatoa adhabu kali na naomba nichukue fursa hii niseme kwamba Serikali inatambua kwamba kuna *NGOs* ambazo zinashirikiana na Serikali kuondoa watoto katika ajira hizi ngumu na ajira chafu, nawapongeza na nawashukuru na naomba waendelee kutusaidia katika kazi hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ndoa imepitwa na wakati, hili amezungumzia Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Lucy Owenya. Wizara ya Katiba na Sheria inaifanyia kazi Sheria ya Ndoa ili iweze kurekeblishwa. Wizara hii inafuutilia utekelezaji wake na bado tuko kwenye hatua ya *White Paper*. Nafikiri sio muda mrefu hilo tatizo litakuwa limetatuliwa. Ninachotaka kusisitiza hapa ni kwamba mtoto ni wa kila mtu kama alivyozungumza Mama Salma Kikwete kwamba mtoto wa mwenzio ni wa kwako. Naomba kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba juzi tu tumezindua ajenda ya watoto na kwenye ajenda ya watoto hiyo mimi naomba kuwaambia kwamba tutawaletea nakala zake, watoto wameainisha maeneo kumi ambayo wangependa Waheshimiwa Wabunge watakapokwenda kwenye kampeni zao na Waheshimiwa watakaogombea Urais wasaini na waseme kwamba watawatetea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba sisi wote tunawajibika na naomba kuunga mkono hoja asilimia kwa mia. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, asubuhi hatukuwatambulisha baadhi ya wageni wa Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa hiyo ningependa kuwatambulisha hawa ambao asubuhi hatukuwatambulisha. (*Makofî*)

Kwanza kabisa tumekuwa tukiongelea hii Benki ya Wanawake lakini sidhani kama mlimtambua Mkurugenzi wa Benki hiyo naye anaitwa Bibi Margareth Chacha. Naomba Bibi Margareth Chacha kama yupo asimame au yuko kwenye kazi kule. Ahsante, hongera Mkurugenzi wa kwanza wa Benki ya Wanawake Tanzania haijawayi kutokea. Karibu sana. (*Makofî*)

Halafu tuna mwakilishi wa *Research and Poverty Alleviation (REPOA)* yaani Taasisi ya Utafiti wa Kuondo Umashini naye ni Bibi Zuki Mihiyo. Yeye yuko kule juu ahsante sana. Tunafurahi sana kuwakaribisheni na pia tunashukuru sana kwa kuja kuwaunga mkono Waziri na wasaidizi wao na tunaelewa kwamba ninyi ndio mnaowaunga mkono katika shughuli zao hizi. Mafanikio yao yote asilimia kubwa yanatokana na ushirikiano mlionao, kwa hiyo karibuni sana. (*Makofî*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama hapa kwa lengo la kuhitimisha hoja iliyanza kujadiliwa tangu asubuhi. Pia nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na

kunipa dhamana ya kusimamia Wizara hii nyeti ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Napenda kuamini kuwa sikumwangusha Rais, kama mwenyewe alivyotamka tarehe 8 Machi, 2010 Siku ya Maadhimisho ya Wanawake Duniani kwamba wanawake aliowateua hawakumwangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nachukua nafasi hii kuwashukuru wafanyakazi wa Tanzania ambao kwa kupitia Shirikisho la Wafanyakazi walioniwezesha kuwa Mbunge dhamana yao ndiyo iliyoniwezesha kuteuliwa kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na hivyo kuwemo katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kwa niaba ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kuwashukuru Wabunge wote kwa jinsi ambavyo wamechangia kikamilifu hoja niliyoiwasilisha asubuhi, wachangiaji kwa hoja yetu walikuwa ni wengi sana hivyo napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wote kwa kutoa ushauri maoni na mawazo ambayo kwetu sisi tumeyaona ni ya msingi sana na hakika tutayazingatia katika utekelezaji wa shughuli zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi na kwa kuongea. Jumla walikuwa ni Waheshimiwa Wabunge 35 na naamini muda huu hautahesabiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa kuongea ni Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, nadhani hawa ndiyo waliochangia kwa kusema na iwapo kama nimewasahau wengine kwa bahati mbaya naomba radhi lakini nikipewa kikaratasi naweza bado kuwatambua. Kwa kweli waliongea waliongozwa na Kiongozi wa Upinzani kwa Wizara hii Mheshimiwa Anna Maulidah Komu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa njia ya maandishi na kama nilivyosema hapo awali iwapo tumewaacha wengine bado mnawenza kunitumia karatasi nikawatambua kwa sababu mmechambua mambo ya msingi sana. Yupo Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Dr. Tarab Ali Tarab, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mwidini Abbas Jecha, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya na Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba radhi kwa wale niliowaacha lakini tafadhali nitumieni haraka haraka ili niwatambue. Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia

lakini naomba nitangulize kusema kwamba si rahisi kujibu yote waliyoyatoa kwa njia ya maandishi au kwa kuongea. Napenda niahidi mbele yako kwamba yote yaliyoandikwa na kuzungumzwa yatafanyiwa kazi na yatatolewa kwa njia ya maandishi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuanze na Kambi ya Upinzani. Kambi ya Upinzani imesema kwamba Serikali haijafanya chochote katika maendeleo ya jamii. Lakini nipende na niwakumbushe kwamba vigezo vya maendeleo ya jamii vinajumuisha katika upatikanaji wa huduma mbalimbali zikiwemo za elimu, afya, lishe, maji, nyumba, mavazi na kipato. Kwa hiyo, Bunge lako Tukufu limesikia mafanikio yaliyopatikana katika sekta hizo tangu Bajeti mbalimbali zilipokuwa zikiwasilishwa hapa Bungeni, mathalani vifo vya watoto vimepungua kutoka vifo vya watoto 68 kati ya 100,000 wanaozaliwa kwa takwimu za mwaka 2004/2005.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge wameshiriki kikamilifu katika kuongeza idadi ya shule za sekondari nchini na hivyo kuongeza idadi ya watoto wanaoingia na kumaliza elimu ya sekondari ukizingatia kigezo cha kipato cha mtu mmoja mmoja ambacho kwa sasa ni shilingi 693,185/= kutoka shilingi 628,259/= ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.3 si kweli kama ilivyoelezewa na wenzetu wa Upinzani. Tunawaomba pale panapokuwa na maendeleo wakubali kwamba CCM imefanya kazi yake kikamilifu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda niwakumbushe Kambi ya Upinzani kwamba kazi ya Serikali ni kuweka mazingira mazuri yanayotoa fursa kwa wananchi kujiletea maendeleo na ni jukumu letu sote hasa sisi Waheshimiwa Wabunge kuwashamasisha wananchi kutumia fursa hizo. Fursa hizo ni kama zile zinazopatikana kupitia *TASAF*, *PADEP*, *MKURABITA* na nyingine nyingi tu kama programu za maji vijiji, punguzo la bei za vyandarua ili kuwakinga wanawake na watoto dhidi ya malaria na kutoa dawa za kupunguza makali ya *UKIMWI*. Kwa hiyo, tunaomba Kambi ya Upinzani mtambue juhudhi zinazofanywa na Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani pia alitoa hoja kwamba Taasisi zinazoanzishwa na wake wa Marais ziwe chini ya Ikulu kama Taasisi maalum. Taasisi hizo zilizotajwa na Kambi ya Upinzani ni Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*) wa Mama Anna Mkapa na Mfuko wa Wanawake na Maendeleo (*WAMA*) wa Mama Salma Kikwete. (*Makofî*)

Napenda kuifahamisha Kambi ya Upinzani kuwa nafasi na kazi za kitaasisi za Mke wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hazikutajwa katika nyaraka yoyote rasmi katika muundo wa Ikulu. Hata hivyo taasisi hiyo huendesha shughuli zake bila kutumia fedha kutoka Bajeti ya Serikali ama fedha yoyote ya umma. Taasisi hizi huchangiwa na taasisi za hiyari na za kujitolea, Mashirika ya Kimataifa, sekta za hiyari na sekta binafsi ambazo huchangia au kuunga mkono shughuli za taasisi hizo baada ya kuridhishwa na matokeo mazuri ya kazi ya taasisi hizo kama alivyoshuhudia Mheshimiwa Fatma Mikidadi. Taasisi hizo hukaguliwa kila mwaka na wakaguzi wa kujitegemea ili kutekeleza sharti muhimu la uendeshaji wa taasisi hizo na taarifa za ukaguzi. Kwa hiyo, ningewaomba Waheshimiwa tuwapongeze Mama Salma Kikwete na Mama Anna Mkapa kwa kazi nzuri wanayofanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililozungumziwa lilikuwa ni kuhusu *NGO*'s kwamba kuna *NGO*'s ambazo hazitimizi wajibu inavyotakiwa kinyume na madhumuni ya kuanzishwa kwao. Lakini jambo la muhimu hapa tukumbuke kwamba *NGO*'s zinatoa mchango mkubwa sana, zipo chache kweli zinazokwenda kinyume na utaratibu lakini tutambue mchango wao mkubwa wa kuunga juhudzi za Serikali katika kuleta maendeleo nchini. Kwa mujibu wa Sheria ya *NGO* namba 24 ya mwaka 2004 *NGO*'s hutoa taarifa za kazi za mwaka na taarifa ya fedha kwa Msajili wa *NGO*'s ambaye ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. (*Makofî*)

Aidha ipo tovuti ya *NGO*'s kama nilivyosoma na iko kwenye kitabu chetu cha Bajeti ambapo wananchi wanaweza kutoa taarifa kuhusu *NGO*'s ambazo utendaji wao si wa kuridhisha. Kwa hiyo, natoa wito kwa wananchi wote ambaa mmeshuhudia kuwepo kwa *NGO*'s ambazo hazitimizi wajibu wao ipasavyo basi mtoe taarifa kwetu ili tuone hatua za kuchukua kwa mujibu wa Sheria ya *NGO*. (*Makofî*)

Aidha, kupitia utekelezaji wa kanuni za maadili za *NGO*'s Baraza la Taifa la *NGO*'s ndilo lenye jukumu pia la kuhakikisha kuwa *NGO*'s zote zinazingatia maadili ya kisekta. Nichukue nafasi hii kutoa wito kwa *NGO*'s pamoja na kutambua kazi zao nzuri wanazofanya lakini wajiepushe na yale ambayo yanaweza kuwatoa nje ya kazi zilizoandikishwa ambazo wanapaswa kuzifanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia na hoja kuhusu Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake. Kamati ya Maendeleo ya Jamii ilitoa hoja kuwa juhudzi za makusudi ziwepo za kuhimiza Afisa Maendeleo ya Jamii walioko katika Halmashauri ambaa wanasimamia mifuko hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunakubali kwamba hatua hii itahamasisha utekelezaji wa Waheshimiwa Wabunge kuwa karibu na wale wanaosimamia mikopo kwa sababu kwa ngazi ya Halmashauri mikopo inasimamiwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Wilaya. Kwa hiyo, kuwepo na ushirikiano kati ya Waheshimiwa Wabunge na Maafisa wale ili kusaidiana kuona jinsi gani wanavyoweza kufanikisha utoaji wa mikopo hiyo. Kwa hiyo, tunakubaliana na ushauri wa Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwepo pia na hoja kuhusu ufinyu wa Bajeti ya Wizara. Ni kweli Wizara imekuwa ikipata Bajeti finyu, lakini Wizara hiyo hiyo imekuwa ikijitahidi kujenga hoja kuongezewa kiwango cha Bajeti. Juhudi hizo zimeanza kuonyesha dalili nzuri, kwa hiyo, ni kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita Bajeti ilikuwa inaongezwa iangawa kwa kiasi kidogo lakini hatua zilikuwa zinachukuliwa. Ni mwaka huu ambapo kama mlivyosikia Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi alivyowasilisha kwamba yapo mambo muhimu mwaka huu ambayo imebidi mambo mengine Bajeti zipungue kama zilivyopungua. Lakini Wizara imekuwa ikiikumbusha Serikali umuhimu wa kuongeza kwa mwaka huu wa fedha 2010/2011, Bajeti ya Wizara imepungua kutokana na kama nilivyosema sababu nne za kimsingi zikiwemo mafao ya Wabunge, Vitambulisho vya Taifa, Uchaguzi Mkuu na mengineyo mengi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na hoja ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu uimairishaji wa Benki ya Wanawake Tanzania. Ni kweli Serikali inajua umuhimu wa Benki hii kama nilivyosema asubuhi wengi wamenufaika na Benki hii na Waheshimiwa Wabunge wengi tu wamezungumzia suala hili la umuhimu wa kuimarisha wakiwemo Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Fatma Othman Ali na wengi wamezungumzia umuhimu wa kuimarisha Benki hii na sisi tunakubali kwamba kuna umuhimu wa kuimarisha Benki hii. (*Makofi*)

Lakini nichukue nafasi hii kutoa wito kwa wananchi wote kuwa Benki inahusu wote wanaume na wanawake. Kwa hiyo, natoa wito kwa wananchi kununua hisa na kufungua akaunti kwenye Benki hii kwa sababu tukinunua hisa, tukifungua akaunti nyingi itakuwa ni njia mojawapo ya kuimarisha Banki hii ili ienee kwenye maeneo mengine ili wanawake wengine pia si wa Dar es Salaam tu wanufaike na huduma za Benki hii. Kwa hiyo, kama tulivoona takwimu asubuhi wanaume wengi hawajajiunga, wengi ni wanawake, natoa wito kwa wanaume kuijunga na benki ya Wanawake kwani Benki hii ni ya wote yaani wanaume na wanawake na kweli kama wanaume mna nia nzuri na wanawake, ili huduma hii isaidie wanawake, basi jiungeni kama kwenye kitabu inavyoonesha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mama Salma Kikwete wamefungua akaunti ili kutoa mfano kwamba si wanawake tu ila ni wote wanaume na wanawake na mimi naomba wanawake muwaaulize viongozi wenu hasa wa kiume kama kweli wanania ya kuwaunga mkono wafungue akaunti na wanunue hisa ili Benki ikomae. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ila kama mlivysikia tulitahadharishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania wakati anaizindua Benki hii kwamba ni vizuri isambae kwa taratibu baada ya kuongezeka nguvu isiwe haraka haraka zikawa hazina baraka. Lakini pia kulikuwa na suala ambalo lilizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba viongozi wa Benki watoe vitambulisho kwa wanachama. Ni kweli vitambulisho vinahitajika lakini Benki ya Wanawake itaweza kufanya hivyo baada ya kuandikishwa katika Soko la Mitaji na kuandaa waraka wa matarajio yaani *prospector* ya Benki hiyo. Kwa hiyo, nawaomba wote mlionunua hisa mvute subira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililojadiliwa na Waheshimiwa Wabunge wengi wakiwemo Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Kiumbwa Makame, Mheshimiwa Savelina Mwijage na Mheshimiwa Nuru Bafadhili, walizungumzia kuhusu umuhimu wa kuacha ukatili dhidi ya wanawake na watoto. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, suala la vita dhidi ya ukatili wa wanawake na watoto na wenzetu wenyewe ulemavu wa ngozi (albino), inahitaji umahasishaji wa hali ya juu. Serikali peke yake haiwezi ila ni jamii nzima ya Tanzania. Natoa wito kwa wananchi wote wa

Tanzania sisi sote tuhamasishane, tukumbushane umuhimu wa kathamini utu wa mtu, kuthamini haki za binadamu hasa ya kuishi ili tusijiingize katika mila zilizopitwa na wakati kwa ukatili kwa wanawake ambavyo tunesikia sasa hivi kila siku sisi wote tuhamasishane ili watu waviache vitendo hivyo. Kama mlivyoona juzi tulizindua mpira maalum ambao juu ya mpira huo yameandikwa maneno yafuatayo; “usimpige mwanamke, piga mpira (*don't kick her, kick the ball*).” Wametumia nafasi hii ya wanaume wengi, hasa wanaume wanaoangalia michuano hii ya *World Cup* basi tunawakumbusha kwamba piga mpira usipige mwanamke. Hakuna sababu yoyote ya kufanya mwanaume ampige mwanamke. Bado mwanamke anaweza kuonywa. Mbona wanaume na wenyewe wakikosea hawapigwi? Kwa wale wanaume wanaopigwa na wanawake tunaomba m jitokeze na sisi tuwaonye hao wanawake wanaowapiga. (*Makofu/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge pia wamezungumzia suala la Wabunge wawezeshwe kwa kuona Bajeti zinaandalika kwa mtazamo wa kijinsia. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto imelivalia njuga suala hili kama mnavyofahamu. Waheshimiwa Wabunge wameunda kikosi maalum ambacho tunaamini kitakuwa kinaangalia Bajeti zinazowasilishwa hapa Bungeni kama kweli kila Bajeti ina mtazamo wa usawa wa kijinsia. Lakini pia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ilianda semina maalum kwa ajili ya Makatibu Wakuu wa Wizara zote kueleweshwa umuhimu wa kuandaa Bajeti zinazozingatia usawa wa kijinsia ili wote, wanaume na wanawake basi wafaidi matunda yao katika mipango inayowekwa au katika kugawa rasilimali. Haya yamezungumzwa na Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Diana Chilolo na wengine wengi na pia wamehimiza kwamba Wizara itilie mkazo dawati la jinsia katika Wizara ili kuhakikisha kweli kwamba Bajeti zote zinazoandalika zinazingatia usawa wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako masuala mengine ambayo yamezungumziwa hasa suala la Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa alilotaka kwamba kwa nini Halmashauri ya Kwimba haikupewa fedha kama ilivyoomba za kuwezesha wanawake kukopa ili kuweza kujiendezea katika masuala ya ujasiriamali. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Bujiku Sakila kwamba suala hili tumelichukua na tunakwenda kulifanyia kazi tuone sababu yake ni nini. Pia kulikuwa na suala la Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi anazungumzia vikundi vya wajasiriamali 36 walioko huko kwake Rorya ambao waliomba fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie kwamba suala hili tumelichukua na tunalifanyia kazi. Sasa kabla ya muda haujaisha kama nilivyoomba radhi kwamba mengi yatajibiwa kwa maandishi nataka nitoe wito kwa mambo haya yafuatayo:-

Kwanza, kuhusu haki za mtoto wa Tanzania. Ni kweli tumepitisha Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambayo inahimiza au inataka watoto wapate haki zao zote za msingi ambazo ni za kuishi za kutunzwa za kulindwa, za kuendelezwa, za kushirikishwa na kutokubaguliwa. Natoa wito kwa wananchi na wazazi tuwajibike. Wazazi wengine hawawajibiki ndiyo maana tunasema watoto wa mitaani wanaongezeka. Mtoto umemzaa wewe wenyewe tena kwa kupenda wewe wenyewe, hakuna mtoto ye yoyote aliyezaliwa

kwa kuomba, tumewazaa sisi wenyewe watoto wote tuwajibike. Natoa wito kwa wazazi, walezi na jamii kwa ujumla wawajibike. Suala ambalo limezungumziwa pia na Waheshimiwa Wabunge ni suala la watoto yatima. Mimi natoa wito kwa Watanzania wote turudie utamaduni wetu. Utamaduni wetu ni kwamba mtoto si lazima atunzwe na baba yake na mama yake tu, anaweza pia kutunzwa na ndugu. Kwa hiyo, tunashangaa kuona kwamba nyumba za kutunzia watoto yatima zinazidi kuongezeka, kwa nini? Maana yake ni kwamba Watanzania tumeacha utamaduni kwamba mtoto asiyekuwa na baba na mama si lazima akatunzwe kwenye nyumba ya kutunzia watoto yatima, anaweza kuchukuliwa na ndugu zake akatunzwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natoa wito kwa Watanzania kuwa turudi kwenye utamaduni wetu, tusiache watoto wakachukuliwa na kutunzwa kwenye nyumba za kutunzia watoto yatima wakati ndugu wapo. Ndugu wawachukue watoto wale waliofiwa na wazazi wao kwa sababu ndiyo utamaduni wetu, tafsiri ya familia kwa Watanzania na utamaduni wetu ni baba, mama, watoto waliowazaa na watoto wa ndugu yaani *extended family* wanassema familia tanda hatung'ag'anii tu kwamba wale uliowazaa ndiyo ukae nao. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nawaomba sana Watanzania tusitegemee sana nyumba za kutunzia watoto yatima, kule mtoto hapati maisha halisi. Hapati raha ya kusikiliza hadithi anazoweza kupata kutoka kwa bibi yake, hapati raha ya maisha ya kifamilia, tuwatunze watoto wa ndugu zetu waliofariki ili wale watoto wanaokaa kwenye nyumba za kutunzia watoto wale ambao kweli kabisa wamejaribu kutafuta ndugu na hakuna lakini mimi ninaamini wengi wao wanandugu hapa Tanzania, tusitegemee nyumba za kuwatunza watoto ambazo ni za kufadhiliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningeongeza palepale kwamba Sheria ya mwaka 2009 hii ya haki ya motto, naomba wazazi mzisome, sisi kwa sasa tunazitafasiri kwa lugha nyepesi, msome, wewe kama mzazi uwajibike sheria ya sasa hivi inamruhusu Afisa Ustawi wa Jamii yaani Kamishna wa Jamii kushtaki na ukanyang'anywa wale watoto, unashangaa sasa hivi wanateswa na wazazi wao hata kama umemzaa mtoto yule siyo wako ni mali ya Taifa, kwa hiyo, unaweza ukanyang'anywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba msome zile sheria, hii sheria ya mtoto utakuta wengine mnanyang'anywa, msishangae kwa sababu sheria ndiyo hiyo na sheria bado inatumika hata kama kanuni bado sheria inatumika ikishasainiwa, inatumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nimeona ni la muhimu sana ni suala la wanawake, mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi. Wanawake jitokezeni mgombee na kisha mpige kura kwani mna uwezo, gombeeni wale ambao wanaona wako tayari wagombee lakini hata wale ambao hawako tayari lakini sisi kama wanawake tunawaona kwamba wanafaa basi tuwaunge mkono, wagombee watuwakilishe ili nao waingie kwenye vikao ambavyo vinaweka mipango, lakini pia kushiriki katika kugawa rasilimali za nchi hii ili wote wanawake na wanaume tufaidi matunda ya nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa natoa wito tu kwa wanawake wenzangu wa Mkoa wa Tabora, mwenzenu mimi nakuja huko kugombea naomba mnikubali, uzoefu ninao, nia ninayo, uwezo ninao, naomba wanawake wa Tabora mnipe ushirikiano. Baada ya kusema hivyo, narudia kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano ambao mmenipa toka nimekuwa Waziri hapa nikiwasilisha hotuba nyingi, ninawaombeeni Wabunge wote kama mlivyo mrudi *Inshaalah*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, ndugu zangu ninawashukuru sana baada ya kusema hivyo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono sasa tunaingia hatua inayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 53 - Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

Kifungu 1001 – *Administration and General*Sh. 2,083,922,671

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kufahamishwa sina shida na mshahara wa Waziri. Lakini napenda kumshukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Mpwapwa na watumishi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Nsalu tarehe 3 Mei, 2010 Waziri alitembelea Chuo na kuona mazingira ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Nsalu na katika hotuba yake namshukuru sana kwamba Chuo cha Maendelo ya Wananchi Nsalu watapatiwa trekta kwa ajili kilimo, lakini hali ya gari la chuo ni bovu na hii ni zaidi ya miaka mitatu, minne nimeshalalamika sana, sasa je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu usafiri wa gari la Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Nsalu?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kuwa gari nimeliona na jambo hili tulikuwa tunalifanyia kazi katika mwaka huu wa fedha.

MWENYEKITI: Yaani mnalitengeneza. (*Makofi*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote, pia nilimpongeza Mkuu wa Chuo cha Maendeleo Singida Mjini Mwalimu Mlade kwa juhudhi zake kubwa za kupanua hicho Chuo kwa kutafuta pesa yeye mwenyewe kwa jitihada zake na kushirikiana na uongozi wote wa chuo hicho, lakini Mheshimiwa Waziri alishawahi kutembelea hicho Chuo na jitihada hizo ameziona tena akaniahidi hata vyuo vingine atawatuma wakuu wa chuo waje wajifunze pale lakini Mkuu wa Chuo huyo anakabiliwa na tatizo la gari, Chuo kimeshakuwa na wanafunzi

wengi wanaenda kusaga wanachuo, wanafunzi wakubwa wadada wanabeba mahindi kichwani hivi ni vitu vilivyopitwa na wakati nimeimba suala la gari sasa ni miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi huko Wizarani hakuna gari ambalo limefikia miaka mitano utaratibu wa Wizarani ni kuwa baada ya miaka mitano gari linatolewa. Hivi limekosekana hata gari ambalo limetumika huko, wamelichoka likaenda pale ili huyu Mkuu wa Chuo tumtie moyo kwa kazi kubwa anayofanya chuo hicho kimekuwa ni chuo cha mfano kwa kweli. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kuwa Mkuu wa Chuo huyo anafanya kazi nzuri sana na anastahili pungezi na niliahidi kuwa patakapokuwa na uwezo wa kifedha, Wakuu wa Vyuo vingine wakajifunze kwa sababu ni mbunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiit, tatizo ni kuwa kama walivyochangia wenye we Waheshimiwa Wabunge katika hoja nilizofafanua mojawapo ni ufinyu wa Bajeti wa Wizara hii jambo ambalo hata ye ye mwenye we Mheshimiwa Mbunge analifahamu kwa hiyo, inakuwa vigumu sana kutoa magari ya kutosha, tuna vyuo 53 kwa hiyo kutokana na ufinyu wa Bajeti mara nyingi tunaangalia vyuo vilivyoko mbali sana na mji ndiyo tunavipa kipaumbele kwa hiyo, mimi ninachoomba tu ni kwamba Mheshimiwa Mbunge vuta subira, tunatambua juhudini nzuri za Mkuu wa Chuo lakini tunaomba uvute subira tu kwa kweli.

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Waziri na Meneja wa Benki ya Wanawake ambayo iko Wilayani Kibaha, Mkoa wa Pwani. Ninawaambia wananchi kule ni Benki ya Wanawake na siyo Benki ya Dr. Gama kama hao wanaotaka kugombea wanavyosema sasa Mheshimiwa Waziri naomba unisaidie na kidogo nitakuwa mkali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *FDC*'s ni vyuo vinavyosaidia sana vijana wetu wa darasa la saba mpaka 12 na vyuo hasa kuliko *VETA* vinavyofika hata kule kijijini. Lakini hivi sasa vinatia aibu, havina vifaa yaani viko katika *technology* ya zamani, watoto wetu wanamaliza wakiwa wadogo darasa la saba, je, Mheshimiwa Waziri ukisema Bajeti ndogo Waziri Mkuu ainuke anafikiria nini hamvipi kipaumbele?

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nimjibu Mheshimiwa Dr. Zainab Gama kama ifuatavyo, Serikali inatambua umuhumu wa *FDC*'s kwa jinsi ambavyo wanafunzi wengi sasa hivi wanamaliza kidato cha nne pamoja na darasa la saba kwa kweli jawabu mojawapo hasa kwa kuwapa ufundi ambao unaweza kuwasaidia kuijari au kuajiriwa Serikali inatambua na ndiyo maana iliunda kikosi kazi ambacho kinaangalia ni jinsi gani ambavyo wanaweza kuunganisha na Mamlaka yaani *VETA* ili wasaidiane katika kuvimaarisha kwa hiyo, minakubaliana na wewe lakini Serikali inalifanyia kazi kwa hiyo, naomba tu mvute subira, Serikali itakuja na jawabu ya jinsi ya kuvii marisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukiangalia jedwali ambalo linaonyesha matengenezo ya vyuo hasa kwenye *Development* Serikali imekuwa ikitoa fedha ili kutengeneza. Sasa hivi kati ya vyuo 53 tayari 33 vimekwishatengenezwa na tukitengeneza tunatengeneza kikweli siyo chini ya shilingi milioni 200 ili ifikie lengo hilo la kutoa ufundi ili vijana wajajiri au kuajiriwa, Serikali ina masikio hata hawa waliopo meza kuu hapa mbele hapa, wameshasikia wanalfanyia kazi, ahsante sana.

MWENYEKITI: Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni mzigo mzito mpe Mnyamwezi haya. (*Makofi*)

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge Waziri Mkoo asimame, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkoo hayupo basi tuna mhakikishia kwamba tutaliwasilisha suala hili kwa Mheshimiwa Waziri Mkoo ili alielewe umuhimu wake. (*Makofi*)

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti Wizara ya Maendeleo Jamii, Jinsia na Watoto wanasema ni Wizara mtambuka, kuwa ni Wizara zote zinahusika. Sasa nataka nielezwe suala la maji, maji limekuwa ni tatizo kubwa sana kwa wanawake katika swali langu nilisema kwamba je, mnalionaje suala hili la maji, Wizara ya Maji na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto mnalipangaje suala la maji? Je, mmeweka mikakati kwamba kama kilimo kwanzza kwa nini maji yasiwe pili kwa sababu maji ni chakula vilevile kwa sababu wanawake wanapata matatizo makubwa sana katika kutafuta maji sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za sasa nataka nielezwe suala la maji, maji limekuwa ni tatizo kubwa sana kwa wanawake katika swali langu nilisema kwamba je, mnalionaje suala hili la maji, Wizara ya Maji na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto mnalipangaje suala la maji? Je, mmeweka mikakati kwamba kama kilimo kwanzza kwa nini maji yasiwe pili kwa sababu maji ni chakula vilevile kwa sababu wanawake wanapata matatizo makubwa sana katika kutafuta maji sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali za kusaidia kuendeleza maji nchini, tunaomba sana tusaidiwe maji, ahsante.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sekta ya maendeleo ya jamii ni mtambuka maana yake ni kwamba wale Maafisa Maendeleo ya Jamii wanahusika na kuhamasisha watu popote walipo katika sekta zote yaani masuala yanayohusu afya, maji, miundombinu kuhamasisha watu ili watumie mazingira yao katika kuijendeze kwa njia ya kuchangia, kwa njia yoyote ile lakini kuamsha ari kwa wananchi ya kujiletea maendeleo wao wenywewe kwa hiyo, kama ni suala la maji Maafisa Maendeleo ya Jamii huhamasisha watu ili kama yapo yale ambayo wanaweza kufanya kutokana na uwezo wao katika eneo lao ili wapate, basi wanafanya kwa kushirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosikia Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya alipokuwa akizungumza asubuhi ni kwamba Serikali imeahidi kuongeza Bajeti ya maji kipindi kijacho tena maradufu kwa hiyo, hapo tujipe moyo. Lakini la pili ni kwamba nilipokuwa nikihitimisha nilizungumzia kwamba tulikuwa na semina ya Makatibu Wakuu lengo lake ilikuwa ni jinsi gani ambavyo Makatibu Wakuu wanawenza kupanga Bajeti zao kwa kuzingatia suala la jinsia mojawapo ni hilo, kama Waziri wa Maji anapoandaa Bajeti yake aweze kuangalia ni jinsi gani hili suala la maji linaweza kuwafikia akina mama kwa sababu wao ndiyo wengi wanaojishughulisha na maji kwa hiyo, nilitaka kumuambia Mheshimiwa Mbunge kuwa ni kweli kabisa Maafisa Maendeleo ya Jamii ambaa ndiyo taaluma tunayoitoa sisi wataendelea kuhamasisha watu katika maeneo yao waone jinsi ya kujiendeleza au kuchangia ili wapate maji lakini pia Serikali imeshasema kuwa suala la maji ni muhimu na litazingatiwa katika Bajeti ijayo. (Makofi)

MWENYEKITI: Halafu inawezekana pengine maji yalipo siyo safi na salama, Maafisa Maendeleo ya Jamii watawahimiza watu kuchemsha maji kabla ya kunywa kwa hiyo ni vitu kama hivyo vidogo lakini vya maana. (Makofi)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa kabisa. (Makofi)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 465,647,662
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Sh. 407,405,903
Kifungu 1004 - <i>Internal Audit</i>	Sh. 157,107,422
Kifungu 1005 - <i>Information, Education and Communication Unit</i>	Sh.101,372,553
Kifungu 1006 - <i>Procurement Management Unit</i>	Sh. 239,862,045
Kifungu 2001 - <i>Training and Folk Development Colleges</i>	Sh. 3,769,864,056
Kifungu 2002 - <i>Community Development</i>	Sh. 1,714,670,853
Kifungu 2003 - <i>Community Development College- Tengeru</i>	Sh. 1,206,647,185
Kifungu 3001 - <i>Gender Developments</i>	Sh .683,218,196
Kifungu 3002 - <i>Children Development</i>	Sh. 461,163,431
Kifungu 4001- <i>Non-Government Organization</i>	Sh. 315,479,023

(*Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote*)

Fungu 53 – Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto

MIPANGO YA MAENDELEO

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i>	Sh. 1,021,546,728
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planing</i>	Sh. 1,049,326,685
Kifungu 2001 - <i>Training and Folk Development</i>	
<i>Colleges</i>	Sh. 2,573,417,304
Kifungu 2002 - <i>Community Development</i>	Sh. 477,424,315
Kifungu 2003 - <i>Community</i>	
<i>Development College- Tengeru</i>	Sh. 301,937,968
Kifungu 3001 - <i>Gender Development</i>	Sh. 2,297,770,000
Kifungu 3002 - <i>Children Development</i>	Sh. 556,900,000

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko
yoyote)
(Bunge Lilirudia)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto taarifa.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa ruhusa yako kabla sijatoa taarifa kuchukua nafasi hii kuwashukuru wafanyakazi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, wadau wote wa maendeleo ya jamii tunaofanya nao kazi kwa karibu, wenzetu katika maendeleo yaani *development partners* wanaotunga mkono ambao wako hapa nawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo imetusaidia sisi kumaliza kuwasilisha hotuba yetu siku ya leo, nawashukuru sana wafanyakazi na Mungu awalinde, muendelee na moyo huo wa kufanya kazi kwa bidii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi na Makadirio ya fedha za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2010/2011 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote hivyo, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofi*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wote wameafiki, napenda kuwapongeza kwa namna ya pekee Waziri na Naibu wake, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kwa maslahi ya wanawake, watoto na jamii nzima ya Tanzania na kama alivyosema Waziri pia tumefarijika sana kuona wale *development partners* wenu wamekaa hapa toka asubuhi yaani siku nzima

wakisikiliza majadiliano haya, ni jambo ambalo hatujawahi kuliona. Siku zingine wanakuja pale na kuondoka lakini ninyi mmebakia mpaka jioni tukiwa tunaahirisha kikao, kwa hiyo, tunawapongezeni sana na tunaomba muendelee kuisaidia Wizara hii kama mlivyosikia Bajeti yake ni ndogo, vyuo vile vilianza mwaka 1975 kwa lengo la kuwawezesha wananchi wa ngazi za chini kutambua namna ya kuboresha maisha yao pale walipo.

Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa muda mrefu sana vyuo vile vimekosa usafiri kama alivyosema Waziri vilianza kukosa wakati mimi nikiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii na mpaka leo vimeendelea kukosa. Lakini kwa hali ya sasa ya kuboresha maisha hizi *millennium goals* kuondoa umaskini, kupunguza vifo vya watoto na akina mama vyote hivi vinahitaji shule kama zile kwa sababu unamfundisha mtu katika eneo lake kwa hiyo, tunaomba sana katika mipango ninyi pamoja na Wizara vitu kama hivyo siyo vibaya tukaanza kuangalia. Kwa mtindo huu mimi ninaamini kabisa vikisaidiwa vinaweza kufanya kazi vizuri sana ya kuamsha moyo wa kujitambua wana hali gani wananchi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, sisi tunawashukuru sana kwa kuwepo siku nzima na mtupelekee salamu zetu hizo, naomba niwapongeze tena Wizara nzima kwa kazi nzuri. Tunayo taarifa ndogo hii ambayo ni mazungumzo maalumu kati ya Wabunge na Taasisi ya Walimu Viziwi na Wasioona yaani tuna walimu hapa walipenda kuongea na sisi kwa hiyo, ofisi wanaeleza kuwa wanaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa kutakuwa na mazungumzo maalumu kati ya Wabunge na Taasisi ya Walimu Viziwi na Wasioona ipo kesho tarehe 6 Julai, 2010 kuanzia saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa na itifaki itazingatiwa na Ofisi ya Bunge, hata mimi nitakuwepo kwa sababu ni mlezi wa shule yangu ya viziwi ile ya Njombe kuna wakati walikuja hapa kwa hiyo, Waheshimiwa mkipata nafasi tafadhali mkazungumze nao muwasikilize wana yao ya kusema. (*Makofi*)

Wabunge wao ni ninyi wenyewe kwa hiyo, ni vizuri tukawasikiliza jamii mojawapo ambao ni watoto viziwi. Kwa hiyo, kesho saa saba mchana baada ya kuahirisha hapa tutakuwa na hayo mazungumzo katika Ukumbi wa Pius Msekwa, sina tangazo lingine naomba niwashukuru sana kwa siku ya leo tumefanya kazi vizuri wote kwa usalama naomba niwatakie jioni njema na muendelee na shughuli zingine zilizoko huko kwa hiyo, ninaahirisha mpaka kesho saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

(*Saa 12.30 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 6 Julai, 2010 saa tatu asubuhi*)